Je Wakristo Wa Kweli Wasimame?

MAURICE BARRATT

TRANSLATED FROM THE ENGLISH BY

ELVENIA NEKESA WAFULA

Je
WAKRISTO WA KWELI
wasimame?

Je
WAKRISTO WA KWELI
wasimame?

na
MAURICE BARRATT

Mfuatano wa kiini cha Ukristo toleo la 1
KIMECHAPISHWA NA HUDUMA YA BARRATT
Manchester M14 5QH England

JE WAKRISTO WA KWELI WASIMAME?
na Maurice Barratt

First printed in England 1998 naUchapishaji wa Huduma ya Barratt
114 Daisy Bank Road, Victoria Park, Manchester M14 5QH, UK.

YALIYOMO

Utangulizi 7

Sehemu ya 1: Mwito

1. Kujiita Wenyewe 13
2. Toboa Sikio Angu..... 19
3. Mwito wa Petro 29

Sehemu ya 2: Gharama

4. Kanuni..... 45
5. Jikane 51
6. Chukua Msalaba Wako 63
7. Nifuate 79
8. Musa 87
9. Danieli 93
10. Yesu 97

Sehemu ya 3: Funguo

11. Nia ya Mungu 105
12. Njia ya Mungu 117
13. Tabia ya Mungu 131
14. Namna Mbili..... 137
15. Yote Akilini..... 153

Utangulizi

Maelfu ya watu walimfuata Yesu katika miaka yake mitatu ya huduma, lakini hakupendezwa na wafuasi. Alikuwa akitafuta wanafunzi-watu ambao angefunza, kwa njia ya kuficha (hadithi) siri za ufalme wa Mungu utakaokuja.Ufalme huu uko ndani ya mtu, na kama vile Yesu asemavyo, Haiji kwa kuangalia kwa makini .Huwa ni sharti kutoka moyoni.

Wakati Yesu aliwasihi watu wamfuate, ilikuwa baada yake kuwaeleza gharama(Ambayo ilikuwa kuyaacha yote, kujikana, na kuuchukua msalaba wao), na baada yao kuelewa gharama hiyo kabisa. Wanafunzi ambao Yesu mwenyewe alifunza walielezwa gharama, kwa sababu waliyaacha yote, na katika Matendo ya mitume sura ya 6 ilidaiwa kuwa watu hawa walikuwa wamebadilisha dunia "juu chini". Hii haikuwa majivuno ya mitume, lakini kauli kutoka kwa maadui zao.

Jamii yetu ya magharibi ina mamilioni ya Wakristo

wainjilisti wanaonena kwa ndimi.Wanadai kuwa na nguvu sawa na Mungu ambazo hawa mitume wa kwanza walikuwa nazo,na bado jamii hizi zinakuwa kafiri zaidi. Kanisa inaonekana kupoteza nguvu zake za kukomesha fujo hii.

Singekuwa na shida na hali hii kama kanisa ingeteswa. Kanisa ni mwangaza wa Mungu, na dunia iko kwa kweli gizani-kinyume na na kanisa kwa hali yote. Kwa hali yote, makanisa yanaonekana kuwa katika Baraka, kujihusisha sana na njia za kidunia, na kukubalika sana katika dunia.

Nimekuwa chini ya mafunzo ya kipentekoste na kiinjilisti kwa miaka arobaini na tano tangu nilipomsikia John Nelson Parr, mtangulizi wa pentekoste,nilipokuwa na miaka saba hadi kufanikiwa, udhibitisho halisi, na ufalme sasa kanuni. Lakini katika miaka tisini tangu miminiko huu wa kipentekoste, jamii zetu zimehalalisha utoaji wa mimba, basha,uchawi na serikali zetu zinaonekana kukosa majibu kwa vurugu, ponografia na madawa ya kulevya.Hizi ndizo vitu ambavyo Mungu huhukumu nchi.

Kwa kweli ni wakati wa kuangalia Ukristo wetu na kuelewa kuwa karama za Roho mtakatifu haziwezi weka mtu au watu takatifu.Ni tunda tu la Roho mtakatifu(Tabia ya Mungu) ambalo linaweza kutenda hivi na kubadilisha tabia yetu kutokana na ile ya Adamu hadi kwa ile ya Kristo.Tumekuwa tukikuza karama zetu huku tunda letu limekuwa likioza.Siamini adui wetu shetani ni muoga wa nguvu

ispokuwa ikifuatanishwa na tabia. Tabia ndio kitu cha pekee ambacho hawezi nakili.Wakati Yesu alitembea kwenye dunia hii mashetani walilia kwa uwepo wake, lakini hawakusema, Wewe ndiye mwenye nguvu. Walilia, Wewe ndiye uliye mtakatifu

Ninaamini kunao watu ambao bado wanatafuta Ukristo wa kweli, lakini ni wapi watakapoenda kuona Wakristo ambao kwa kweli wanaishi mafunzo ya Yesu, kama inavyofunzwa katika mahubiri mlimani?Haitakuwa ngumu katika China au Cuba, ambapo kanisa linateswa, lakini Magharibini inakaa imeadimu kweli.

Hakuna kivuli cha shauku akilini mwangu kwamba Ukristo wa kweli ni njia ya kimapinduzi, vita dhidi ya falme za dunia hii. Pia nimeridhishwa kuwa vita ni vya kiroho na vya kindani.Ikiwa tutaweka mapinduzi yawe ya kiinje na tujaribu kupigana dhidi ya na kupindua mtindo,siasa,biashara na hata dini za dunia hii, basi tumeshindwa vita vya mtu wa ndani, na pia kujikinga na silaha za kuangamiza na kuanza vita vitakatifu kama mababu zetu waliopotoka,wenye vita vya dini.Historia inadhibitisha kwamba hii ni upuuzi, kinyume na mapenzi ya Mungu, na shahidi wa dunia ya ukafiri wetu.Tunatenda makosa yale yale tu ambayo wanafunzi walitenda Yesu alipokuwa duniani humu. Walitaka ufalme wa kidunia kabla Yesu arudi tena mara ya pili kutawala kama mfalme duniani.

Kwamba kutakuwa maumbile,udhihirisho wa kiinje wa vita vya kindani sina shauku; lakini kazi

hizi za nje au Matendo lazima ziwe matokeo ya mabadiliko ya kindani.Tunaposahau tu tamaduni zetu,kanuni zilizotengenezwa na watu na ukawaida wetu, na kuuchukua sura mpya ya ukweli katika mafunzo rahisi na halisi ya Yesu,tutaona ukosefu wetu mkubwa leo. Wazo kuu hilo, kwamba Tunaweza kuwa huru kutoka kwa miaka elfu mbili ya ufarakano, majadiliano ya kanuni,mageuzo,na uasi,na kukaa uupya miguuni mwa mkubwa wetu ,kuamini na kutenda alichosema!Ni yeye anayeweza kutufunza maadili haya;na yeye pekee anayeweza kuondoa utando machoni mwetu.

Ninawezaje hisi kuhitimu ili nikabiliane na suala hili, au kusudia kutenda kile wasomi maarufu au wanateologia wamejitahidi kutenda kwa karne nyingi? Kinachoniwezesha tu cha kweli yaweza kuwa uhusiano wa kibinafsi na Mungu. Ingawaje nimeishi miongo miwili ya maisha yangu nikisoma mafunzo ya Yesu ninatambua hii haitoshi pekee. Kujua kitambo ni muhimu lakini kujua mwandishi ni muhimu zaidi.

Nimeishi pia miaka ishirini zilizopita nikikuza uhusiano wangu wa binafsi na Mungu, na nimetambua kuwa hauwezi kuwa na uhusiano na kanuni za kidini, hata ile sawa .Kanuni hazina mihemuko au hisia;Mungu anazo.Kanuni haiwezi kuwa na hasira au huruma .Mungu, mwenyewe,ana sifa,na hii ndio utofauti wa maana sana. Siri ya kuelewa neno la Mungu ni kumuelewa Mungu.

Ukuaji wa uhusiano wowote ni uwiano na wakati na nguvu zilizotumika.Nilipoanza kuzoea mahubiri

mlimani badala ya kuiamini tu, maisha yangu ilibadilishwa.Iliathiri kazi yangu, familia na kila mtu niliyekutana naye.

Nimeridhika kuwa kila aliye tayari kupokea mafunzo haya atapata changamoto kwa tabia yao, kanuni na hali ya maisha katika kitabu hiki.Nniatumai itakuwa mfano wa kuvutia kuwacha msalaba ufanye kazi maishani mwao,ili maisha ya ufufuo ya Yesu udhihirike ndani na mwao.

Sehemu ya 1

Mwito

Wakristo na kanisa wametaka ushirikiano na kila kitu kinacholeta nguvu duniani.Kwa ukweli hii imesimama kwenye imani kuwa, Ahsante kwa roho mtakatifu, Nguvu za dunia hii zimetiishwa kwa kazi ya injili, kanisa na misheni. Lazima tutumie nguvu zao kwa faida ya uinjilisti.Utajiri na mamlaka mbalimbali yanajulikana kwa njia hii na yamewekwa katika ibada ya kanisa.

Lakini kinachotendeka ni kinyume zaidi. Kanisa na misheni yamepenywa na nguvu na kusonga kando na ukweli kwa ufisadi wa nguvu. Yesu anaposema kuwa ufalme wake sio wa dunia hii, anasema kwa uwazi anachokusudia kusema.hamaanishi ufalme wa dunia hii(Hata ikiwa anayetawala ni mkristo). Anatuweka tayari kutokana na kutafuta ufalme mwingine ila ile ya Roho mtakatifu.

Jaques Ellul

SURA YA 1

Kujiita Wenyewe

Kauli ya kwanza ambayo nataka kuweka kuhusu ufuasi ni kwamba hatuwezi kujiita wenyewe. Tunaweza amua kumfuata Yesu kwa hiari yetu, lakini hatuna uwezo au haki ya kujiita wenyewe ufuasi sio "wazo njema".

Wala sio kitu ambacho kanisa limelazimishwa kutenda.Historia imedhibitisha bila shaka kwamba wakati kanisa linapojaribu kuleta wafuasi kupitia sheria na nidhamu,huleta kinyume.Wafarisayo katika enzi za Yesu walikuwa mfano mwema wa watu kama hao.Yesu alisema kuwa walitenda kila kitu sawa kulingana na barua ya sheria,lakini ndani yao walikuwa wamejaa na uchafu na unafiki.

Mungu hufanya kazi kwa undani, kwa ubadilisho wa moyo, sio ubadilisho wa tabia.Ajabu ya kutosha, mfuasi wa kweli wa Yesu hafungwi na kanuni za nje

za urekebishaji, yeye ni mtu huru.Paulo alisema katika Wakorintho wa kwanza 6:12 kwamba vitu vyote ni halali na katika Tito 1:15 kwamba vitu vyote ni safi kwa hao walio wasafi. Huo ndio uhuru wa kweli, lakini lazima itokee moyoni.

Wacha tuangalie vile Yesu alivyo alivyowachukua wale watu waliojitoa kwake kama wafuasi.Ungefikiria kwamba Yesu alikuwa akijaribu kuwazuia.Ninaamini kwamba hicho ndicho kwa usahihi alichokusudia. Katika Luka mtakatifu 9:57 Tunasoma; Nao walipokuwa wakienda njiani, mtu mmoja alimwambia Yesu, Bwana, nitakufuata kokote utakakokwenda.

Ni nini mbaya nana kauli ya mtu huyu? Ningependekeza kuwa ni kwa kiburi, kwa sababu alikuwa hajui Yesu alikokuwa akienda.Hata wafuasi wake aliowachagua hawakuwa wanajua.Hawakutarajia kuwa Yesu angekufa kifo cha mkufuru kwenye msalaba wa kirumi.Hapa pana "mtu fulani" asiye na mwito,akifikiria kuwa angemfuata Yesu popote angeenda.Hii sio tu kiburi ,ni ujinga.Alifikiria kwa udhahiri kwamba kulikuwa na gharama kidogo au hakukuwa na gharama yoyote ,na ikiwa kulikuwa nayo,angeweza kugharamia,alidanganywa.

Hakuna kitu ambacho kimebadilishwa

Hali hiyo leo ni sawa na wafuasi wengi wa kisasa wa Kristo na lazima niweke lawama kwa huu udanganyifu katika mlango wa kanisa, kwa kuogopa kuwa watawapoteza washirika kwa kuwaeleza ukweli

kwa nguvu za changamoto ,ni zaidi ya walivyojiandaa kufanya na kwa huzuni hawaleti wafuasi wao wa uongo.

Ni jibu lipi Yesu alilipa kujitoa kwa huyu mfuasi ambaye angekuwa? Mbweha wana mashimo, na ndege wana viota: lakini mwana wa mwanadamu hana pahali pa kulaza kichwa chake.

Yesu alikuwa akisema kuwa hakuwa na popote pa kuita kwake, na kwamba lazima angewaamini watu wengine ili apate chakula, nguo na mahali pa kujikinga, lakini alikuwa pia akiona zaidi .Ndege na Mbweha hujenga vyumba vyao zaidi ya hii.Ujenzi wa nyumba ni sehemu ya kumchagua mume au mke na kujenga familia. Kuna gharama ya juu zaidi hapa kuliko kwa ukawaida hapo kujitokeza mara ya kwanza.

Kati kupita kwa Luka kuna mifano mingine miwili ya wanaume waliotoa utumishi kwa Yesu kama wafuasi, lakini katika kila mmoja jawabu ambalo Yesu anawapa ni sawa .Hatusomi kwamba yeyote katika watu hawa watatu alikuwa mfuasi.Naogofia kuwa, kama Yule mtawala mdogo tajiri,walienda kwa huzuni.Je Yesu alikuwa mkali sana kwa hawa watu?Hata alikuwa mkarimu sana.Alikuwa anawaokoa kutokana na kushindwa na

Fikiria maelezo ya ajabu ambayo Yesu anaweka katika Luka 14:26 Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake,na mama yake ,na mke wake,na mwanawe, na ndugu zake waume na wake ;naam na hata nafsi yake mwenyewe hawezi kuwa mwanafunzi

wangu. Kauli hii inakaa haiwezekani kutenda,na bado haikuambiwa wafuasi,bali ni kwa umati,pengine wale ambao walikuwa wameona miujiza na kufikiri kuwa maisha ya mfuasi ilikuwa nzuri na rahisi.

Wakati wa kuzingatia

Tukikubali kuwa Yesu alimaanisha hasa alichosema, basi gharama ya kuwa mfuasi ni kubwa kweli, na si kwamba mtu achukuliwe kwa haraka au bila kujadiliana kifikira. Yesu alimaanisha kwa usahihi kuwa kunapotokea na hali ambayo tunatakiwa kuchagua kati ya baba na mama au Kristo, tunapaswa kumchagua Yesu. Tunaweza badilli kamili mtu yeyote au umiliki katika mlinganisho huu kama vile mke, watoto, kazi, kanisa, huduma, au maisha na jibu huwa ni sawa.Haitawahi lingana.Inafaa sasa iwe dhahiri kuwa yeyote anayekataa uamuzi huu utakuwa wazi kwa mashtaka kwamba wanamchukia mtu au kitu ambacho wamekidharau kwa ajili ya Kristo. Lakini hilli ni neon lile ambalo hutumia. Kwa kujua gharama kuu, Yesu anakuwa katika kauli yake, Kwa sababu hataki sisi tushinde Kwa sababu ya ujinga au kutokuelewa. (Tubaposhinda Kwa sababu ya unyonge, hilo ni jambo tofauti kwa uzima).

Mifano ya Yesu

Soma kwa utaratibu mifano miwili ambayo Yesu anapeana sasa, ya mtu anaye jenga nyumba na

mfalme anayeenda kupigana,na utakubali kuwa Yesu anataka yeyote anaye linganishwa na mfuasi kuhesabu gharama kwanza.Luka 14:28-32 Maana ni nani katika ninyi, kama akitaka kujenga mnara ,asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kwamba anavyo vya kuumalizia, asije akashindwa kuumaliza baada ya kuupiga msingi, watu wote waonao wakaanza kumdhihaki, wakisema, mtu huyu alianza kujenga , akawa hana nguvu za kumaliza.

Au kuna mfalme gani, akitaka kuenda kupigana na mfalme mwingine , asiyeketi kwanza na kufanya na kufanya shauri,kwamba yeye pamoja na watu elfu kumi ,ataweza kukutana na Yule anaye kuja juu yake na watu elfu ishirini? Na akiona kuwa hatashinda, hutuma mabalozi na ujumbe kutaka sharti za amani.

Kwa kweli Yesu hangekuwa tena wazi katika mifano yake au kusema zaidi kuzuia wafuasi ambao watakuwa wake ili wasidanganywe? Kwa kweli ameshawaonya kwa uwazi na kwa maneno ya nguvu? Kwa kumaliza, Yesu anarudia tena kauli yake ya kufungua katika sura ya 33: kama ilivyo kwenye mifano hii miwili, yeyote ambaye hawezi kana yote aliyo nayo hawezi kuwa mfuasi wangu.

Kuwa katika huduma, nakutana na watu wengi ambao kanisa imeshindwa kuwa kweli, na wana maumivu, uchungu na wanahisi kudanganywa. Mara nyingi hawana maumivu au uchungu na Mungu, bali na kanisa na mfumo wake.

Hawakuelezwa gharama, na zaidi ya hayo walielezwa kuwa hakutakiwa na gharama yeyote na

kuwa yote ilikuwa imelipwa Kalvari.Gharama ambayo ililipwa na Yesu kule Kalvari ilikuwa ya dhambi zetu, na Hakuna kitu chochote ambacho tungechangia katika lile dhabihu.Lakini kuna gharama ambayo Wakristo wanatarajiwa kulipa,na hiyo ni gharama ya wanafunzi.

SURA YA 2

Toboa Sikio Langu

Ninaamini kuwa mwito wa kuwa mfuasi ni wa kibinafsi kutoka kwa Kristo mwenyewe, na uamuzi wetu ni daima wa kufahamu, ambao huja baada yetu kuelewa gharama na matokeo.Ni uamuzi ambao hauko chini ya mhemuko au hisia,bali chini ya ukweli. Hili haliwezi kutendeka mwanzoni mwa mwendo wetu wa Kikristo wakati tunapoanza kumfuata Yesu.

Ni kama tu upuuzi na jambo lisilo na busara kutarajia kuwa mtoto angeweza kukubali Kuajiriwa kwa masaa kamili kabla yake kukua,kuwa na nguvu, na kuelewa masharti ya uajiri.Siamini kuwa inawezekana kwa mtu kuwa mwanafunzi mara moja.Uanafunzi ni mtindo.Kwa kweli kunao wafuasi wanaokua kwa mara moja.Unaweza weka uamuzi wa kumfuata Yesu baada ya kukutana naye kwa mara ya kwanza. Lakini huu sio uanafunzi.

Uamuzi mgumu

Wakati wana wa Israeli wallipopewa fursa ya kumfuata Musa kutoka Misri,haukuwa uamuzi mgumu kwao baada ya miaka mianne ya utumwa,utolewaji wa uhuru ulikuwa chaguo rahisi sana.Walifurahi kutoka kwa haraka.Uamuzi mgumu kwa wanaisraeli ulikuja baada ya Mungu kuwaeleza waende kwenye nchi ya ahadi.Wakati wana wa Israeli walipotoka Misri walikuwa na wazo wa nchi yenye mtiririko wa maziwa na asali. Hii haikuwa mtungo kwenye mawazo yao. Ilikuwa ahadi ya Mungu kwao. Lakini kitu ambacho Mungu hakuwaambia Wanaisraeli walipotoka Misri ni kwamba nchi hiyo ilikuwa imemilikiwa na majitu, na walikuwa wapiganie kila ardhi ya nchi hiyo.Miji ilikuwa imezingirwa na kuta hadi mbinguni.Na tunajua kutoka utambuzi ya kwamba kuwa kwenye kambi kulimaanisha kuwa wangewakimbia adui zao sio kuwaangamiza.

Kushindwa kwa israeli

Ilikuwa wakati ulipofika wa kupigana na majitu ndipo Israeli iliposhindwa.Paulo, katika barua yake kwa Wahebrania, anatueleza kuwa walikataa kutii kwa sababu ya kutokuamini.Kwa ajabu –ama tuseme kwa uoga-Mungu hakuwapa nafasi ya pili, hata walipotubu.Aliwaeleza kuwa watakufia jangwani, na walikufa. Je hii inamaanisha kuwa mipango ya Mungu hushindwa tunapokosa kutii? Hapana inamaanisha

kuwa tumeshindwa.Mpango wa Mungu hautawahi shindwa, Lakini haimaanishi kuwa Mungu anafaa amfunze mtu mwingine ili kuutimiza mpango wake.

Hata hivyo, Mungu alivunja ahadi yake kwa Israeli kwa sababu ya kiburi chao.Hiki ndicho chanzo cha neno halali "Uvunjaji wa ahadi" Mungu alisema katika kitabu cha Hesabu 14:34,Baada ya hesabu ya hizo siku mlizoipeleleza ile nchi, yaani siku arobaini,kila siku kuhesabiwa mwaka,mtayachukua maovu yenu, ndiyo miaka arobaini,kila siku kuhesabiwa mwaka, mtayachukua maovu yenu , ndiyo miaka arobaini, nanyi mtakujua kufarikana kwangu.Kilikuwa kizazi kilichofuata cha Israeli ambacho kiliingia kwenye ardhi yenye mtiririko wa maziwa na asali, kiliwashinda majitu,kuumiliki ardhi na kuutimiza ahadi ya Mungu.

Je unaona usambamba katika maisha ya mkristo? Kuuacha ulimwengu na kumfuata Yesu. Si uamuzi mgumu, mara tu magamba yanapoanguka kutoka kwa macho yetu. Neema, huruma, upendo, msamaha na uzima wa milele –kwa kweli, hii ni ahadi ya maziwa na asali. Si uamuzi mgumu kumfuata Yesu tunapogundua kuwa Tunaweza kuwa huru kutokana na utumwa wa kidunia, kutoka utumwa hadi uovu na kutokuwa na hakika kwa baadaye milele.

Tatizo letu linakuja baada ya –tunapokumbana na changamoto la kutii, la kuuchukua msalaba na kujikana mwenyewe. Hapa ndipo mara kwa mara kanisa hushindwa kushindana nasi, na badala ya hiyo hutufanyia rahisi, kwa kutupa uchaguzi rahisi kutuambia kuwa "Yesu anaelewa" na kuwa "Aina

hii ya maisha huvutia tu wachache hasa ambao wameitwa"

Toboa sikio langu

Ninaenda kuangalia kanuni katika Agano la kale ili kuegemeza kauli yangu. Katika kutoka 21,mistari sita ya kwanza inazungumzia kummiliki mtumwa. Kauli ya kwanza isio kawaida katika mstari wa pili. Mungu hasemi "Huwezi kumnunua mwanadamu mwingi" au "Unafaa tu kuwanunua watumwa wa mataifa mengine wala sio watu wa taifa lako". Anasema, unapomnunua mtumwa mhebrania.

Kauli hii inaweza enda kinyume na hukumu ya maadili.Kama vile uhuru wa kibinafsi na imani kuwa Mungu aliumba wanadamu wote sawa. Lakini hasa katika sura hii ya kufungua tunafaa kuamua ikiwa tunaenda kuamini na kukubali neno la Mungu, au kuibadalisha na kuiwezesha kutoshana na mawazo yetu ya kanuni za desturi. Tutapitia uamuzi mara nyingi tunaposoma mafunzo ya Yesu. Ninaenda kupendekeza kuwa tutupilie mbali namna yetu ya kufikiria na kukubali neno la Mungu.

Kwa kweli, katika neno la Mungu hapa katika Kutoka tunaona kwamba Mungu hayuko kinyume na maadili ya kumnunua mtu. Mungu yuko kinyume na Mabwana wabaya,wale ambao ni wakatili na hutumia uongozi vibaya .Katika sura ya tatu, Mungu anaweka sharti muhimu sana, yakwamba mtu anaweza kumnunua mtumwa kwa muda wa miaka

sita pekee, na sio milele. Katika mwaka wa saba, Bwana anapaswa kumueka huru. Katika sura ya 16, Mungu alianzisha adhabu ya kifo kwenye kosa la kumuiba mwanamme au mwanamke.

Utumwa ni uhuru

He tuangalie hali ya utumishi kwa ufupi na tusahau fikira zetu za magharibi za haki na nafasi ya usawa. Katika hiki kipindi cha historia ya israeli, watu maskini walikufa kwa kukosa chakula katika kipindi cha njaa au mahitaji makubwa. Kujitoa katika utumwa ilikuwa njia ya kuokoa maisha yako na familia yako. Utumwa haukuwa jambo mbaya sana. Katika sura ya 4 kuna masharti yaliyo hakikisha kwamba utumwa ulitendwa kwa haki, kisha tunapatana na kauli ya ajabu-Ajabu kwenye masikio yetu-Katika sura ya 5:Ikiwa mtumwa atasema kwa wazi, nampenda Bwana wangu. Ni ajabu kwetu kwa sababu sisi hushirikisha utumwa na ukatili na utumizi mbaya wa uongozi. Wazo la mtu kupenda.Wazo kuwa mtu anaweza penda Bwana wake inamaanisha kwamba Bwana wake ni mzuri, na kwamba kuwa mtumwa wake ni jambo la kutamani na la kufaa.

Fikiria jambo la mtumwa na Bwana mwema. Ningependekeza kuwa mtumwa huyo ana uhuru kumliko Bwana wake. Kwa nini? Kwa sababu hana mzigo wa uwajibikaji ambao Bwana wake anao. Bwana hujikimu kwa vyakula na mavazi, hulipa bima, hukimu mahali pa kuishi na huwajibika kwa

ustawi wa utumwa.Hugharamia mzigo wa fedha na uangalifu unao ambatana na uwajibikaji huu. Mtumwa huwa huru kutokana na mizigo ya kifedha na wasiwasi za maisha.

Watumwa hawana haki

Jambo la kuogopesha kuhusu kuwa mtumwa ni kwamba hawana haki, hawawezi kuwakataa mabwana wao.Tatizo ambalo mtumwa hupata na bwana mwema ni moja, ya kutii vikamilifu.Ninasema "ugumu" lakini kwa kweli katika jamii yetu ni zaidi sana kuliko "ngumu". Haikubaliki kabisa hata kulifikiria, acha hata kutenda.

Fikira nyingine ni kwamba watumwa hawana haki ya kuwachagua mabwana wao. Mtumwa yupo kwa kutolewa, ni chaguo la Bwana. Hapa tena tunaona usambamba na maisha yetu. Soma maandiko yafuatayo kutoka kwa Injili ya Yohana, ambayo yote ni kauli kutoka kwenye mdomo wa yesu mwenyewe: Yohana 15:16, Hamkunichagua lakini mimi ndiye niliyewachagua…Yohana 6:44, Hakuna anayeweza kuja kwangu, isipokuwa Baba ambaye amenituma...Yohana 6:65, Hakuna mtu awezaye kuja kwangu isipokuwa amejaliwa na Baba yangu. Ninasikia wasomi wengine wakisema hapa "Tulikuwa watumwa wa dhambi na shetani, lakini si Yesu alikuja kutuweka huru?" Ni kwa uhakika ukweli yakwamba Yesu alikuja kuharibu kazi ya Shetani na kuvunja mshiko wake kwetu- Lakini kwa hiyo yote

ili tuwe huru. Tumenunuliwa kwa bei(damu ya Yesu), na sisi sio wetu wenyewe. Tumekombolewa kutoka kwa mwajiri wetu wa kale,shetani, na sisi ni bwana mwingine. Paulo katika Wakorintho wa kwanza 6:19 inasema Nini? hamjui ya kuwa miili yenu ni hekalu la Roho mtakatifu aliye ndani yenu,mliyepewa na Mungu? wala ninyi si mali yenu wenyewe.Kwa kuwa mmenunuliwa kwa gharama: kwa hivyo mtukuzeni Mungu kwa miili yenu, na kwa nafsi zenu ambazo ni za Mungu.

Hii inaonekana kama utumwa kwangu. Tunapomfuata Yesu yote tunayofanya ni kuwabadilisha waajiri. Yesu alisema katika Mathayo6:24, Unaweza tu kumtumikia mwajiri mmoja kati ya wawili. Pengine tungehisi furaha ikiwa kungekuwa na maamuzi matatu yetu kuzingatia, Mungu, Shetani, na sisi wenyewe, Lakini hii si ukweli; kwa kweli ni uongo mkubwa. Kujifurahisha ni kwa kweli kumtumikia shetani, Na kumpenda Mungu ni kuuchukua kila kitu, hata sisi wenyewe.Hatufai kuiwezesha au weka kwa kiroho maneno ya Yesu. Kwa kuwa ni ya kweli na ya kutiiwa;na utiifu ndiyo ushahidi na dhibitisho pekee ambayo tunaamini.

Mstari wa mwisho tunaangalia katika Kutoka 21 na kauli ya mwisho kuhusu utumwa ni labda kanuni yenye maana sana kuliko yote. Mstari wa 6 unasema hivi: Ikiwa mtumwa anampenda Bwana wake na hataki kuwa huru baada ya miaka sita ya kazi yake, ndipo hapo huyo Bwana wake atamleta mbele ya Mungu na kumleta mlangoni, au penye mwimo wa

mlango; na Bwana wake atalitoboa sikio lake kwa umma; ndipo atamtumikia siku zote.

Tiwa alama ya milele

Ni kwa nini Mungu Anasema kwamba mtumwa lazima abaki mtumwa milele? Kwa nini maandiko haisemi "Kwa miaka sita zijazo?" Kwanza, hii inakaa ya kutoeleweka. Lakini tunapoiangalia kwa makini, ni yenye maana. Miaka sita ya kwanza ni ya uamuzi wa mwajiri, wala si ya mtumwa. Mtumwa anaweza kuwa aliachwa kwa njaa. Kwa kweli mwajiri wake alimuokoa kutokana na ukosefu wa chakula na msiba, lakini sasa, baada ya miaka sita, anaweza weka uamuzi muangalifu na wenye akili.-Je anafaa akae na mwajiri wake, au amuangalie mwajiri mwingine?

Kama ungemfanyia kazi mwajiri mmoja kwa miaka sita ungekuwa kwenye msimamo mwema wa kujua ikiwa alikuwa mwajiri mwema au la: Hangeyajua haya kwenye mahojiano, au hata wiki chache baada ya ajira. Inachukua muda na mazoea kwa walinzi na unafiki wa tabia zetu kuja chini na kujionyesha wenyewe.

Hii ndiyo maana Mungu alisema kuwa mtumwa lazima atiwe alama. Ilikuwa kuonyesha yeyote aliyejali kuona kuwa mtu huyu, kwa uchaguzi wake, hatawahi kuwa huru, Alikuwa na nafasi ya kuchagua uhuru na akaamua kubaki mtumwa. Ni uamuzi wake, na kwa hivyo ni ya maana kwamba inafaa kutiiwa. Yesu alisema katika Luka 9:62 kwamba kuuchukua

jembe kwa hiari yako, kisha kuangalia nyuma, yaani kuwa na wazo la pili au kubadilisha akili, inakuweka asiyestahili kwenye ufalme wa Mungu.

Yakobo

Kanuni hii ni dhabiti kote Bibliani na katika shughuli za Mungu kwa wanadamu. Nitachukua tu mfano mmoja wa mengi katika Biblia.

Yakobo aliamini na kumfuata Mungu wa baba zake kutoka ujana wake. Kuna ushahidi mkubwa katika maandiko ya kutudhibitisha ukweli huu. Na hata tabia zake kama vile jina lake linaonyesha, ilikuwa bado ile ya mlaghai. Yakobo aliweka mapatano na Mungu. Katika Mwanzo 28:20-21 Tunasoma Yakobo akaweka nadhiri akisema, Mungu akiwa pamoja nami, akinilinda katika njia niendayo, na kunipa chakula nile, na nguo nivae. Nami nikirudi kwa amani nyumbani kwa baba yangu, ndipo Bwana atakuwa Mungu wangu…na katika kila utakalonipa hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi.

Kupatana na Mungu

Wafuasi wengi wa Yesu wa kisasa wanafikiria sawa na Yakobo na hufanya mapatano kama hayo na Mungu. Wanataka Mungu awabariki kwa njia ambazo wanataka kuenda, kama malipo ya zaka na sadaka. Lakini haihusu kufuata lakini inahusu kifo kwa mwenyewe na kubadili kwa tabia, na Mungu

mwishowe alimkabili Yakobo na hii. Mwanzo 32:24-32 inarekodi kuwa Yakobo alipigana mwereka na malaika.Hii ilikuwa tukio la "kutoboa kwa sikio" kwake. Baada ya tukio hili, jina lake lilibadilishwa, na pia tabia yake, na alitiwa alama ya maisha.Alikuwa akitembea kwa kuchechemea , kuonyesha dunia kuwa hakuwa wake mwenyewe. Yakobo sasa alikuwa na alama ya Mungu katika maisha yake.

Wakristo wengi amabao wanaamini kwa vita vya kiroho kwa bidii ya maombi huongea kuhusu Yakobo na maombi yake ya ushindi, jinsi alivyong'ang'ana na malaika na kupata nguvu na Mungu.Hii kwa kweli ni ya kusifika; lakini hawafikiri sana matokeo ya kung'ang'ana huku na Mungu –alama ya kudumu inayoacha maishani mwako.

Nionyeshe mtu mtakatifu nami nitakuonyesha mtu aliye na alama ya Kristo kwake. Paulo anasema katika Wagalatia 6:17. "Tangu sasa mtu asinitaabishe; kwa maana ninachukua mwilini mwangu alama zake Yesu."Hakusema alama za Kristo zilikuwa katika nafsi au akili yake, lakini katika mwili wake. Alama za Kristo huwa haziko kwenye nyama yetu iliyokufa; zinaweza kuwa alama za kiakili au kiroho;lakini huwa dhahiri, kutofautisha alama za maisha yetu, na wazi kwa mengine.

SURA YA 3.

Mwito Wa Pwtero

Imani sio kipofu, inafaa iwe kitu ya maana ya kutenda –sio kwa sababu tunaelewa yajayo, au hali yetu, lakini kwa sababu na wakati tumekuja kuelewa tabia za Mungu, kwamba Mungu ni mwajiri mwema ambaye anastahili kutumikiwa milele, sio uamuzi ghafla ni katika msingi huu, na katika msingi huu tu, ndipo tunaweka uamuzi wetu. Ninaamini kuwa sababu nyingine ya kuwa mfuasi sio imani bali ni kiburi, na hatari sana.

Hakuna wafuasi wa mara moja

Ninatumia Petro kama mfano wa ukweli kwamba Hakuna kitu kama ufuasi wa mara moja. Petro anaweza onekana mfano geni wa kutumia, kwa sababu watu wengi wanaamini kuwa Petro alikuwa

mfuasi wa mara moja.—kwamba alipoitwa na Yesu aliyaacha yote mara moja na kumfuata. Lakini Yesu hangeulizia hayo Petro bila yeye kwanza kumfuata, na kuelewa gharama ya matokeo ya uamuzi wake.

Niruhusu niwaeleze kitu ambacho nimejifunza katika miaka ambazo Nimekuwa nikisoma Biblia. Ikiwa muujiza, fumbo, au tukio linatendeka kwa injili zaidi ya moja basi tunaweza pata tu ukweli wote kwa kuweka hesabu pamoja kama rekodi moja mzima. Biblia imetiwa motisha na Mungu, na Hakuna kilichowekwa kwa bahati. Kila jambo ndogo ni la maana sana. Mfano wa Petro umetumika vyema kama kielelezo cha hii.

Historia ya Petro

Katika Mathayo 4:18-20 tunasoma, "Naye Yesu alipokuwa akitembea kando ya bahari ya Galilaya, aliona ndugu wawili , Simioni aitwaye Petro, na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa wavuvi. Akawaambia, Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu.Mara wakaziacha nyavu zao,wakamfuata.

Hadithi hii inakaa kwanza kuwa jambo nzuri kwa mfuasi wa mara moja.Lakini hatuwezi sema hivi hadi tuangalie injili hizo zingine mbili ambazo zimeandikwa mwito wa Petro. Kwa kweli, tutagundua kuwa Mathayo anaandika hatima ya mwito wa Petro kuwa mfuasi. Lakini Luka na Yohana wanatupa matendo dhahiri na kinaganaga kuhusu tukio

lililotendeka vyema kabla ya Andrea na Petro”

Yohana 1:35 inasema kuwa Yohana mbatizaji alisimama na wafuasi wake wawili na kutangaza kuwa yesu, ambaye alikuwa tu amembatiza, ndiye mwanakondoo wa Mungu. Yohana alikuwa akisema kwamba yesu ndiye Masiha. Tunapata mistari michache baadaye. Mmoja wa hawa wafuasi wa Yohana alikuwa si mwingine bali Andrea, nduguye Petro.

Mstari wa 41 unasema, Andrea kwanza alimpata ndugu yake, na kusema, Tumempata Masiha. Ni wazi kutokana na hii kuwa Andrea na Petro wote walikuwa wakingojea ukombozi wa Israeli na kukuja kwa Masiha.Waliposikia hili tangazo la Yohana, walianza kumfuata Yesu. Andrea na Petro walikuwa wanafunzi wa Yohana, lakini bado hawakuwa wanafunzi wa Yesu –walikuwa tu wafuasi.

Kutokana na kauli hii, Tunaweza amini kuwa Petro hakuwa mvuvi mwenye kulaani na kafiri wa kisasili chetu. Ikiwa alikuwa mwanafunzi wa Yohana mbatizaji basi tuna hakika kuwa alikuwa ametubu dhambi zake na kubatizwa, kwa kuwa hii ndiyo Yohana alihubiri na kuwatakia wafuasi wake. Mstari wa 41 inatueleza Andrea na Petro walikuwa wakimfuata Masiha, na Matendo ya mitume 10:14 inasema wazi kuwa Petro hakuwahi kula kitu chochote cha kawaida au kisicho kisafi. Alikuwa Myahudi mwema akimgonjea Masiha na kumfuata nabii wa Mungu, Yohana mbatizaji.-Nabii pekee ambaye alikuwa wakufuatwa kabla Yesu kuanza

huduma yake.

Petro kutoka kwa kuwa mwanafunzi wa Yohana, alikuwa sasa mfuasi wa Yesu, Tunahitaji sasa kuangalia Luka 4:37 hadi 5:11kupata kila kitu cha ni wapi na ni aje Petro alikuwa na hili “Kutoboa sikio”. Mstari wa 38 inasema kuwa Yesu alimponya mama mkwe wa Petro katika nyumba yake. fahamu kuwa haikuwa ndani ya nyumba ya mama mkwe . Yesu alikuwa ndani ya nyumba ya Petro, kwa hivyo Petro alikuwa bado na nyumba yake wakati huu-hakuwa bado ame “yaacha yote.” Siku hiyo Yesu aliponya kundi la watu wa magonjwa ya aina yote, na mapepo yalitolewa kwa wengi :Petro alikuwa hapo na Yesu kama “mfuasi”, Yesu aliponya na kuhubiri katika miji ya Galilaya.

Sio hapo hasa

Katika Luka 5:1-3, Tunasoma kuwa Yesu alitumia mashua ya Petro na aliwahubiria makundi ndani yake. Ni wazi kuwa Petro alikuwa bado haja “yaacha yote” hapa, alikuwa bado mfuasi. Baadaye aliacha nyumba yake, uvuvi wake na yote yake.

Hakuna kitu kibaya na kuwa kwenye hii “ufuataji”. Mungu alitumia shughuli za Petro kwa manufaa. Mashua yake ilitengeneza jukwaa bora. Mungu pia atatutumia katika shughuli zetu, hali ya familia zetu, au vyovyote hali yetu inaweza kuwa; lakini lazima tugundue kuwa hii tu ni “kufuata” na wakati wa mashindani, lazima na itakuja kwetu sote. Hata

hivyo, kwa sababu ya uoga, ambayo ni kutoamini Wakristo wengi hawawezi na hawatalipa gharama ya uanafunzi, na wanabaki kwenye jangwa katika maisha yao yote, wakila chakula cha ulimwengu wa kiroho, Mungu akiwapa mahitaji ya kimiujiza, wakishindwa na majitu na kumiliki nchi ya ahadi. Kwa hivyo mara nyingine lazima Mungu atakingoja kizazi kijajo ili kuleta ukombozi kwenye ardhi yetu maskini.

Muujiza

Injili ya Luka inatupa utondoti wote wa mwito wa Petro kwa uanafunzi, na Tunaweza jifunza masomo kutoka kwa hiyo sisi wenyewe, kwa sababu njia haibadiliki kamwe. Mungu atabadilisha tu hali ili kuwadanganya wasio na imani. Katika sura ya 5:4, Yesu alimwambia Petro, Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki. Petro alikuwa hajavua lolote usiku wote, lakini wakati huu aliona kuwa nyavu zilikuwa zinararuka.Waliyajaza mashua yote na samaki hadi walianza kuzama.

Muujiza usio wa kawaida; sio rahisi kuelewa kwa nini Yesu alitenda yote haya. Tunaweza elewa kwa nini aliwaponya watu au aliwalisha watu elfu mia tano wenye njaa; lakini miujiza huu ulitimiza nini? Huu ulikuwa miujiza wa utoaji.

Petro hakuwa mkusanyaji aliye weka samaki kwenye tangisamamaki, wala hakuwa mvuvi wa mshipi ambaye aliyarudisha mara tu alivyoyavua. Petro aliuza samaki. Uvuvi kwake haukuwa tu jambo

la kupenda au kupitisha wakati, ulikuwa uzima wake .Aliona samaki kama pesa.

Kabla tuangalie majibu ya petro kwenye huu utoaji wa ajabu, lazima tusimame na tufikirie majibu yetu yatakuwaje katika hali hiyo au tutakosa somo la muhimu sana.

Wacha tufikirie kuwa tumekuwa tukimfuata Yohana mbatizaji na kumtafuta Messiah, na kwamba sasa tumempata na tunamfuata. Tuko katika huduma ya kiulimwengu, tukiona ishara na miujiza, Wakati mara tu Yesu anafanya miujiza wakibinafsi wa utoaji. Pengine miujiza huu unatoa ijara ya wiki nyingi kwa mara moja. Majibu yetu yatakuwaje? Tunaweza kuwa tumeona haya kama ishara ya yale tumekuwa tukingojea. Wacha nifafanue. Wafuasi wengi wa kisasa wangependa kuenda "kamili." Tatizo tu ambalo linawasimamisha ni lile la itoaji. Nani atakayelipa gharama yote? Wataendeleaaje kuishi bila mapato ya mara kwa mara na pensheni? Wana majukumu mengi na wanajua kuwa ni wabaya zaidi kuliko kafiri wasipowatolea familia zao. Lakini hapa kuna Yesu akitoa pesa kwa mapema. Ni nani ambaye hataenda "kwa ukamili" ikiwa pesa ililipwa kwenye akaunti yao ya benki kwa mapema kila mwezi?

Jibu geni

Hata kama hatukuona hii kama ishara ya kutoa kuenda kwa saa kamili, tutafurahi kwa miujiza huo mkubwa wa baraka. Kwa kweli, tungekuwa tumejawa

na shukrani na sifa kwa Yesu. Majibu ya Petro yalikuwa kwa hivyo ya kushangaza, na bila shaka yasiyotabirika.

Alijibu kwa njia ya kinyume na kile nitakachoonekana kuwa chenye maana. Petro alimwambia Yesu katika mstari wa 8, siwezi kukufuata tena,ondoka kwangu.

Chochote kilichomsababisha Petro kunena kauli hii ya ajabu? Jibu liko katika nusu ya pili ya sentensi ya Petro: Mimi ni mwenye dhambi. Je muujiza wa utoaji ungeweza jionyesha kwa Petro dhambi zake? Sina ufafanuzi, kwa sababu Mungu hatumii hali sawa na sisi sote; lakini naamini naweza kufafanua kanuni.

Kanuni

Ili kuwa mfuasi wa Yesu tunafaa kumuona Mungu; tabia zake zinafaa kudhihirika kwetu – huruma yake, neema, msamaha, ukweli, utoaji, maisha ya milele. Hata hivyo hii haiwezi tendeka kwetu bila miujiza kutendeka, kwa sababu, Mungu wa dunia hii amepofusha macho ya wale ambao hawaamini. Roho mtakatifu anafaa kuondoa hiki fungakidoto kwa ufunuo wa Kristo kuonekana, basi ni rahisi kufuata, wakati magamba yanaanguka kutoka kwa macho yetu na tunaona mshangao wa tabia ya Yesu.

Uanafunzi, kwa hali yoyote, ni tofauti sana. Kabla tuwe wanafunzi, fungakidoto kinafaa kuondolewa, na tena hatuwezi toa wenyewe. Linafaa kuwa tendo la Mungu, lakini wakati huu tunafaa kuona wenyewe.

Mungu anafaa kutuonyesha tabia zetu wenyewe, tabia ya Adamu ambayo bado iko ndani yetu hata badala ya sisi kupokea msamaha. Hii haipendezi, kwa kweli ni uchungu kabisa.

Isaya alikuwa na uzoefu huo huo. Alikuwa na maono ya Mungu katika sura ya 6.ukuu na kuinuliwa juu kwa sifa na ukuu wa enzi. Lakini Isaya alijiona na kusema Ole wangu kwa kuwa nimepotea. Hakuna njia nyingine inayowezekana kuliko hii. Kumuona Mungu kwa ukweli ni kujiona kwa ukweli. Naogopa, kwamba watu wengi huona tu Mungu wa imani yao. Kwa bahati mbaya, mafunzo ya dini hayawezi kutuonyesha hali yetu ya dhambi. Hatuhitaji ufafanuzi wa tabia ya Mungu; Tunahitaji Mungu mwenyewe.

Petro alijiona mwenyewe, na hakupenda vile, alijihisi kuwa hastahili. Lakini hiki ndicho kilichokuwa kabisa kile Yesu alikusudi, na kwa sababu hiyo atatutendea hayo. Ni mtu ambaye anajiona tu jinsi alivyo anaweza kuwa mwanafunzi. Petro alijihisi asiyestahili kwa sababu aliona utenda dhambi wake; lakini Yesu hakufikiri Petro alikuwa hastahili. Inaonekana kwa Yesu kuwa Yesu alikuwa na furaha sana na Petro akijua kuwa alikuwa mtenda dhambi. Yesu alikuwa akimwelezea "Usiogope Petro-nimekuwa nikijua jinsi ulivyokuwa wakati huo wote. Najua hata kuwa utanikana na kusema hunijua. Ninataka tu wewe uijue sasa kwa kuwa unaijua, ninaweza kukutumia sasa ninaweza kukufanya mvuvi wa watu."

Enye manufaa kwa Mungu

Petro alipokuwa mfuasi, Yesu alikuwa mtumizi wa maana sana kwake. Alimponya mama mkwe wake, alimpa huduma Petro kuhusika ndani-Lakini Petro hakuwa wa maana yoyote kwa Yesu.

Lakini baada ya Yesu kudhihirisha kwa Petro hali yake ya dhambi, na Petro kukubali ukweli wa ufunuo huu, kisha papo hapo akakuwa wa maana kwa Yesu. Aliyaacha yote, na kubadilika kutoka kwa kuvua samaki (kuangalia mapenzi ya ufalme wa Mungu.) Hapa kuna kauli nyingine: Mungu ni wa utumizi mzuri kwa wafuasi, lakini wanafunzi ni wa matumizi mazuri kwa Mungu.

Kitu halisi hatimaye

Luka inasema katika sura ya 5:11 jambo sawa ambalo Mathayo alisema katika kauli yake fupi: Hata walipokwisha kuviegesha pwani vyombo vyao, wakayaaacha yote na kumfuata Yesu. Cha ajabu, matokeo ya Petro kwa muujiza wa utoaji ulikuwa kuyaacha mali yote. Wakati huo ambao angeona katika muujiza ule jibu kwa mahitaji yake yote—badala yake alikabiliwa na mahitaji ya roho yake. Aliona kuwa, utoaji au bila utoaji, hakuwa anastahili, hangeweza kumfuata Yesu. Lakini Yesu alipomtia moyo, alijua angeyaacha yote, na kuyaacha makubwa aliyo yakamata ambayo yangempa pesa nyingi, baada ya hayo na kumfuata Yesu.

Uanafunzi wa kweli

Huu ni uanafunzi. kufuata bila kuyaacha yote sio uanafunzi. Ninawezaje kuwa mwenye elimu ya imani sana kwa kusema hivi? Nitakurudisha tu kwa kauli ambayo Yesu alinena kuhusu mada. Itakubidi uamue ikiwa utayakubali kama kauli ya kweli, au kama mifumbo mengine, akili ya kiroho yaliyowekwa ambayo yatatekeleza mtindo wako wa kimaisha. Katika Mathayo 7:24-27 Yesu anaeleza fumbo, mwishoni mwa mahubiri katika mlima, kuhusu ujenzi wa nyumba kwenye mwamba au mchanga. Imesemekana kwamba Yesu ndiye mwamba ambao tunajenga juu yake, lakini si jambo hilo kamwe. Unapoangalia hadithi, Yesu anatuambia kile ambacho mwamba na mchanga kinamaanisha. Wale ambao wanajenga kwenye mwamba ni wale ambao wanaamini kwenye mlima na wanayatenda. Wale ambao wanajenga kwenye mchangani wale ambao wanaamini mahubiri kwenye mlima na hawayatendi.Hii kwa dhahiri inamaanisha kuwa ni kutenda na sio kuamini ndilo jambo muhimu—Tunawezaje dhibitisha tunaamini isipokuwa imani yetu inapokuwa na maonyesho mengine wazi? Hatuwezi jificha nyuma ya imani yetu ikiwa hatutekelezi yale imani inataka katika Biblia yote—kutii.

Soma kwa makini kauli za Yesu kuhusu uanafunzi, yazingatie, kwa kuwa ni ya msingi kuliko chochote ambacho nimetaja.

Wakristo wa kweli

Yesu anafafanua katika mahubiri yake katika mlima kwamba sisi ni chumvi, na kwamba sio ubora kiasi tu ndio tuna nyunyuza kwenye jamii. Ni maisha yetu wenyewe. Ukristo wa kweli sio kile tunachoamini lakini vile tunavyoishi. Yesu anliita "maisha" wala sio "imani". Kuna Wakristo ambao wanaamini na kuidhibitisha katika maisha yao, na kuna wale ambao wanaamini tu kuwa wanaamini, kwa sababu yote iko kwenye kanuni na mawazo yao.

Luka14:34-35 Chumvi ni kitu chema: lakini chumvi ikiwa nimeharibika, itiwe nini ikolee? Haifai nchi wala jaa; watu hutupa nje. Ni nguvu gani pale iko katika kauli hii ya Yesu—Na ni shtaka gani anaposema kwamba kupoteza au kukosa maisha hii inatutoa wasio stahili hata katika ncha ya taka. Tunakuwa bure.

Tumeshaangalia kanuni ya utumwa katika sura ya 2, ununuzi wa watu ni dhahiri kutokana na wetu kwamba mwajiri wetu mwema, Mungu hatatukabili na changamoto la uanafunzi hadi tunapopata wakati wa kufikiria gharama. Tunahitaji wakati kufikiria ikiwa Tunaweza aminia maisha yetu mengine kwa huyu mwajiri.

Changamoto letu linaweza kuja baada ya miaka sita au miezi sita au Pengine miaka ishirini, Nimeridhika kuwa kila mfuasi ana angalau mwito mmoja kuwa mwanafunzi. Israeli ilikuwa tu na nafasi ya kuingia kwenye nchi ya ahadi, lakini Petro alipata mwito wa

pili kutoka kwa Yesu—na hasa muujiza sawa.

Sijui itakuwaje kwako, kwa sababu Ukristo ni uhusiano wa mwenyewe na Mungu. Unaweza kuwa na bahati kumi, au unaweza kuwa tu na moja. Ninachosema tu ni kuwa itakuwa upuuzi kudhania kuwa utapata bahati zaidi ya moja. Ninajua kuwa kanuni hazibadiliki.

Makabiliano

Tukio langu ni kwamba nilimfuata Yesu tangu nilipokuwa na miaka sita. Baada ya miaka ishirini na nne nilipokuwa na miaka thelathini, nilikabiliwa na changamoto la kukataa maisha yangu kabisa bila ya kuwa na neno lolote kwa ukumbusho wote, na kumfuata Yesu popote atakaponiongoza.

Hii ni hatua ya kuogopesha, kwa sababu Hakuna anayeweza kukueleza mahali ambapo Yesu atakapotembea Ungeweza kumfuata hadi kwenye mateso au mashaka, hadi kwenye upweke au kukataliwa na watu. Haidhibitiki kabisa, na ni hili jambo ndilo wafuasi wengi hawawezi kukabiliana nalo. Wanataka pia kuwa na neno katika maisha yao ya usoni.

Hii ndio maana tunahitaji kumfuata Mungu kwa uhusiano wa kibinafsi, na kuzoea mamlaka yake katika maisha yetu, kabla hatuja chukua hatua nyingine. Kuitenda kwanza itakuwa upumbavu mkubwa.

Kutoka wakati nilipokuwa na miaka thelathini, sijawahi angalia nyuma, na kwa neema ya Mungu sitawahi rudi nyuma. Ushuhuda wangu kwa miaka ishirini zilizopita ni kwamba nimempata Mungu kuwa Bwana mwema ambaye ana ustawi wangu moyoni. Licha ya feli zangu nyingi, sijapata nafasi ya kumlipa Mungu na chochote bali uaminifu.

Ni nini kinachotendeka kwa wafausi

Unaweza kuwa unauliza, "Je tabaka hizi mbili za Wakristo basi ni wafuasi na wanafunzi?" tumeona kuwa kuna uendeleaji dhahiri katika maisha ya mkristo, na haiwezekani kuanza kama mwanafunzi.

Lazima, kwa hali yote tufukuze wazo kuwa Mungu angetaka tabaka mbili za Wakristo. siwezi pata andiko lolote la kuunga mkono wazo hili. Hata hivyo nimeridhika kuwa wengi wa watu wanaojiita Wakristo ni wafuasi tu. Wengi wao hawajapata bado wakati wa kudhibitisha Mungu na kwa hiyo bado hawajapata changamoto kuyaacha yote; lakini Ninaamini kuwa wengi ni wale ambao wamepata changamoto, na wamekataa kulipa gharama. Pengine mwito ulikuja tu kwa mara moja, labda kwenye mkutano wa misionari au kutoka ya pekee, au wakati wa ugonjwa, au baada ya msiba. Kama kuna hali milioni ambayo Mungu anaweza tumia, lakini ninadhibitishia kuwa atapokea kwa wakati mwingine mwito mmoja kwa uanafunzi.

Mabaki pekee

Je ninakuwa mwenye kiburi, mlokole au mwenye kujidai kwa kudai kuwa wengi wameukataa mwito? Ninaweza sema tu kuwa sijatia mkazo makadirio yangu kwenye mipaka na hukumu ya mapendeleo yangu, Lakini katika maarifa yangu ya Biblia na ripoti aminifu ya Mungu na Matendo yake na watu wake.

Huwa kila mara ni mabaki, uchache mdogo, ambao wameokolewa, Nuhu na familia yake waliokolewa, na dunia yote ilizama majini. Uwiano unaogopesha. Lot na familia yake waliokolewa, na sehemu yote ya mji iliangamizwa.

Pengine ungetoa hoja kuwa watu ambao waliangamizwa kwenye kadhia hizi walikuwa watenda dhambi. Ukweli, lakini sio tofauti na watu wa Mungu. Nchi yote ya Israeli waliokolewa kutoka Misri kwa ishara ya miujiza, na walikuwa kwa dhahiri "Wakimfuata Mungu" na bado ni wawili tu pekee walioingia kwenye nchi ya ahadi-wawili kati ya milioni mbili! Katika hadithi ya bikira wakumi, na wengine nusu walifungiwa nje.

Maelfu ya watu walimfuata Yesu alipotembea duniani, na bado ni mia moja ishirini tu ambao walikuwa kwenye chumba cha juu, wakingoja kama vile Yesu alivyoamuru. Maelfu ya watu aliwaponya na kuwalisha kwenye jangwa walikuwa wapi? Ni nini kilitendeka na umati uliopiga kelele "Hossana" Yesu alipokuwa akiingia Yerusalemu, walipokuwa wakifikiria ataenda kufanywa mfalme? Nitawaambia.

Walikuwa wakimfuata Mesiha ambaye angeiweka maisha yao rahisi, na kuwatendea miujiza, kulisha miili yao yenye njaa; lakini kumfuata mtu kwenye msalaba—huo ulikuwa gharama kubwa sana.

SEHEMU YA PILI

Gharama

Hakuna tena zaidi
Imetosha ninalia
Siwezi vumilia aibu mbaya
Macho yangu hayaangalii tena sawasawa
Yanaingia ndani
Ninajiona
Giza
Dhambi

Mwili wangu hauwezi tena simama
Magoti yameinama chini ya mzigo
Mwili umelala chini
Limekufa
Limetulia
Lakini ni nini kilicho kwenye nyusi zangu
Ninahisi tone la maji likianguka
Na kwa nguvu nyingi nikapindua kichwa change
Na kuangalia sura hii ya ajabu
Ya mikono inayotoka damu na miguu ambayo imeumia
Na kwa upande wake mto unatiririka
Ambao unanifunika
Na mengine kando
Moyo wangu na nafsi yangu imesafishwa
Hakuna uoga mwingine wa shauku na aibu
Moyo wangu ni mwepesi
Nafsi Yangu huru

Lakini bado mtumwa
Kumtumikia zaidi.

Maurice Barratt

SURA YA 4

Kanuni

Kuna gharama kubwa ya kulipwa mtu anapokuwa mwanafunzi, na tunafaa kufikiria gharama hii kabla tutoe uamuzi ambao utaathiri hali yetu yote ya maisha. Nataka kuangalia gharama hii kwa ukaribu, kwa kuwa Yesu aliweka masharti kwa uwazi sana.

Maagizo ya kigeni

Katika Mathayo 16:16 tunasoma kuwa Petro alikuwa na ufunuo kuwa Yesu alikuwa Kristo, mwana wa Mungu anayeishi. Yesu anasema kuwa hatima hii yeye mwenyewe, lakini kuwa ilikuwa ufunuo takatifu. Sasa kwa kuwa Petro na wafuasi wengine walijua haya, itakuwa ya maana kutazamia kuwa Yesu angewatuma kutangaza habari hii njema, kwamba Mesiha waliokuwa wakimngoja amefika

sasa. Wangetangaza sasa ufunuo huu kwa dunia kwa mamlaka na ujasiri.

Lakini katika mstari wa 20, Yesu anasema jambo lililo kinyume. Ndipo Yesu alipowakataza sana wanafunzi wake wasimwambie mtu yeyote ya kwamba yeye ndiye Kristo. Kwanini Yesu angeipa amri hii ya kigeni wanafunzi wake? Kwa nini angetaka ukweli huu ufichike? Siri iko katika mstari wa 21; Tangu wakati huo yesu alianza kuwaonya wanafunzi wake yakwamba imempasa kuenda Yerusalemu, na kupita mateso mengi, na kuuawa.

Mabadiliko ya huduma

Unaposoma injili ya Mathayo kutoka mahali hapa, utapata kwamba huduma ya Yesu inabadilika. Isipokuwa tukio moja ambalo Yesu anamponya kijana ambaye wanafunzi walikuwa na ugumu kumponya, Hakuna uponyaji mwingine uliandikwa. Yesu sasa anaanza kujiandaa na wanafunzi wake kuutimiza nia yake duniani, ambayo ilikuwa kuteseka, kufa kifo cha kulipia kosa, na kufufuliwa kutoka kwa kifo. Hii ndio ilikuwa sababu ya kweli Yesu alikuja duniani. Miujiza na uponyaji ilikuwa tu nya kuonyesha tabia ya baba yake – upendo, huruma, rehema na neema. Miujiza haikuwa dhibitisho ya uwezo wa Yesu, wakadhibitisha kuwa alikuwa Kristo. Kama yangekuwa dhibitisho la ushahidi, basi Yesu angeshindwa, kwa sababu watu hawangemuamini,

alisulubiwa kama mkufuru.

Petro hangeelewa mabadiliko hii ya mwelekeo katika huduma ya Yesu. Kama Wakristo wengi leo, alikuwa akitafuta falme wa nje kudhihirishwa mara moja duniani. Yesu kwa hivyo alikemea Petro kwa lugha yenye nguvu zaidi. Alitumia maneno kamili kwa Petro ambayo alitumia kuongea kwa shetani baada ya majaribio kwenye jangwa – Rudi nyuma yangu shetani. Mbona lugha yenye nguvu kama hiyo? Ilikuwa kwa sababu Yesu alikuwa anapewa falme za dunia hii, mara moja, na bila msalaba. Huu ndio "ufalmewa kisasa sasa" Kanuni ambayo inatoa ufalme bila msalaba. Petro hakutaka kuenda kwenye msalaba kwa sababu aliutaka ufalme mara moja, na bila mateso au taabu yoyote. Ninaamini kauli "Hakuna msalaba, Hakuna taji" Ni ya kweli na hutumika.

Hatua tatu rahisi

Yesu kwa kuweka imara njia ambayo lazima aende, inaweka wazi sana kuwa hii pia ni njia ambayo wanafunzi wake lazima waende. Mstari wa 24 unasema: Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake,na anifuate, maagizo tatu rahisi – na bado haya ni mengine ya maneno magumu zaidi ambayo Yesu aliwahi nena, na lazima tuyachunguze kwa utondoti, kwa kuwa hatua hizi tatu ndizo siri ambazo zina asili ya maisha yote ya mkristo.

Katika uchunguzi wa kwanza, itaonekana kama Yesu ameweka maagizo haya matatu kwa mipango mbaya. Kwa kweli, kufuata inafaa kuwa hatua ya kwanza kisha, wakati tupo mbali na njia, huenda tungefikiria ikiwa tungejikana kidogo. Msalaba inaonekana ya kuogopesha sana kwamba kwa Wakristo wengi ni kwa usalama sana kuiweka mwisho katika orodha, na kutamani kwamba isiwahi kuja.

Tunajua kuwa Yesu alikuwa mwalimu mwajiri, kwa hivyo nia yake ilikuwa nini kutoa hali ya maisha ya mwanafunzi kwa mpango huu? Angemaanisha tu kuwa isipokuwa tu tukijikana na kuuchukua msalaba wetu, basi hatutakuwa tunamfuata Yesu, kwa kweli. Labda tunalifuata kanisa letu, au madhehebu yetu, kanuni zetu, wainjilisti bora au dhamira yetu, lakini tunajidanganya ikiwa tunafikiria kuwa tunamfuata Yesu. Kufuata ni matokeo ya kawaida tu ya kuutimiza masharti mbili za kwanza.

Ninaamani kuwa kauli hizi tatu za Yesu zinahusika na mambo matatu ambayo tunajua vyema maishani mwetu, mambo matatu yanayotuzuia sana katika matembezi yetu ya Kikristo: dunia, mwili na shetani. Ninaamini kwamba kujikana ni njia ya kuhusika na dunia, kuuchukua msalaba ni njia ya kupambana na mwili (Hali yetu ya kawaida ya Adamu), na kumfuata Yesu, matokeo ya kawaida, ndio njia ya kupambana na shetani. Mara tu tunapo pambana na dunia na mwili, tutapata uwezo juu ya ibilisi – lakini tu wakati huo.

Kuharibu kazi ya shetani

Katika waraka wa kwanza wa Yohana 3:8 tunaelezwa kuwa Yesu alidhihirishwa ili azivunje kazi za Ibilisi. Kazi ya Ibilisi ni gani? Kinyume cha kazi ya Mungu. Kazi ya Mungu ni gani? Ni kuwafanya wanadamu watakatifu. Kazi ya Ibilisi ni kinyume – kuwasababisha wanadamu kumuasi Mungu na kuwa kama yeye, Muovu. Kuharibu kazi ya shetani, basi, ni kuharibu au kupindua mtindo huu na kuwarudisha watu kwenye ushirika na utiifu wa Mungu, ili tabia zao ziwe kama za Mungu. Hiyo ndio sababu kamilifu ya kanisa, kuwafanya watu watakatifu.

Ikiwa hatujaacha dunia, na ikiwa hali yetu ya kawaida ya kitambo haijakabiliwa, yaani kusulubiwa, tunawezaje kuwa watakatifu? Kuharibu kazi ya shetani ndio hatua ya tatu na ya mwisho, kwa hii tunahitaji tabia ya Kristo, sio tu uwezo wake, kwa kuwa ibilisi haogopi tu nguvu isipokuwa inapofuatwa na utakatifu. Anaweza badilisha nguvu zote na vipawa vyote, lakini hawezi kuwa mtakatifu au kuonyesha tabia za Kristo.

Wacha sasa tuangalie kwa ukaribu haya masharti matatu ambayo Yesu anatuonyesha.

SURA YA 5

Jikne

Kujikana haina uhusiano wowote na dhambi. kwa wale ambao ni Wakristo damu ya Yesu iliyo lipa makosa imelipwa matakwa halali ya dhambi zetu zote na, kama vile sheria ya kiingereza inadhibitisha, kosa linaweza lipwa tu mara moja. Yesu alilipia bei kosa letu na sasa tuna utakatifu wa Kristo sio utakatifu wetu wenyewe. Hakuna kitu kinachoweza kutuweka watakatifu zaidi au kidogo kuliko tulivyo chini ya damu ya Yesu Kristo, na utakatifu wetu katika Kristo haubadiliki kwa ajili ya hali yetu au udhaifu wetu, ni hali isiyobadilika. Kifo cha Yesu kilipokamilifu cha kosa.

Kwa hali yoyote, nina hakika kuwa mkristo yeyote mwaminifu atapitisha kwamba waendelee kutenda dhambi hata baada ya kukubali upatanisho huu, kwa kuwa dogo lolote zaidi na ukamilifu ni dhambi.

Tofauti ni kuwa sasa hatuwajibiki tena na dhambi zetu. Kama vile Paulo anasema katika Warumi 8:1 Sasa, basi, Hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, ambao hawatembei katika mwili lakini katika roho. Na katika Wakolosai 1 mstari wa 21 na 22, Paulo anasema, Na ninyi…amewapatanisha sasa; katika mwili ya nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama machoni pake. Kama vile Martin Luther alivyosema, sisi sote ni watenda dhambi na bado tumedhibitishwa.

Wacha ninene kutokana na tukio langu, nina amini kuwa yako pia ni sawa, kitu cha mwisho ambacho ninataka kufanya ni kutenda dhambi, na bado ninaweza sema maneno ya Paulo na kusema kuwa ninatenda dhambi licha ya tamani zangu. Ninatamani kuwa kama mkombozi wangu, na kamili katika kila njia, lakini katika mazoezi ninatenda dhambi kila siku kwa sababu ya hali yangu ya kawaida ya Adamu. Kwa hivyo, Kujikana dhambi haitakuwa kujikana mwenyewe. Itakuwa furaha yangu!

Kukana vitu halali

Ikiwa hii ni ukweli, basi kujikana kunaweza maanisha tu jambo moja. Inamaanisha kujikana vitu ambavyo ninapenda kutenda, furaha ambayo ni halali, vitu ambavyo si vya dhambi kwa vyenyewe. Hii ndio sababu Yesu na mitume waliongea sana kuhusu dunia, na hatari zake.

Tunafaa kuwa dhahiri hapa kwamba wakati Biblia inazungumzia kuhusu "dunia" haimaanishi nchi uumbaji wa Mungu. Nchi ni ya Mungu na vyote vilivyo ndani yake, lakini mungu wa wakati huu ndiye mungu wa ulimwengu, Ibilisi. Mbali na nchi ambayo ni maumbile yaliyoumbwa, dunia haipo katika hali ya maumbile. Ni mfumo wa kiroho, njia ya kufikiria. Iko pamoja na tamaduni, siasa, biashara na dini.

Katika Wakorintho wa pili4:4 Paulo anasema kuwa Mungu wa dunia hii amepofusha macho ya watu. Huyu anaweza tu kuwa Ibilisi. Dunia yetu ya sasa, tangu dhambi ya kwanza ya Adamu, haijawahi milikiwa na yeyote isipokuwa ibilisi, na haitawahi milikiwa na yeyote isipokuwa ibilisi. Hali hii ya mambo haitawahi badilika hadi unabii katika Ufunuo wa Yohana 11:5 utimie, wakati ufalme wa dunia hii utakuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake.

Tunapozingatia maandiko yafuatayo kuhusu dunia, inafaa kuwa dhahiri kuwa, kama Wakristo, tunafaa kujikana na kujitenga kutokana na dunia

Mathayo 16:26—Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupita hasira ya nafsi yake? (Tunachukua andiko hili kama muktadha tunapolitumia kama ujumbe wa injili kwa watenda dhambi. Imenenewa wanafunzi wa Yesu.)

Marko mtakatifu 4:19 –Na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine zikiingia, hulisongesha lile neno likawa halizai. Hili ni andiko linguine ambalo linatumika kwa watu ambao wamepokea neno la Mungu na wameshazaa

matunda.

Yakobo 4:4 – Hamjui yakwamba kuwa Rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu na hii ni uzinzi wa kiroho? Tena neno hili, limenenewa Wakristo.

Waraka wa kwanza wa Yohana 2:15-16 – Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda baba haiko ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, ,yaani tama ya mwili, na tama ya macho, na kiburi cha uzima, havitoki kwa baba, bali vyatokana na dunia. Mara nyingine andiko lilinenewa kanisa.

Kuiacha dunia

Ni rahisi kwa wakristo kuzungumza kuhusu kutokuwa wa dunia hii, lakini tuna husishaje kwa ukweli huu katika maisha yetu ya kila siku, kazini, au katika hali ya familia zetu? Ninatoa maisha yetu ya kanisa, kwa kuwa Ninaamini kwamba kwa jumla ni hali ya uongo. Ukristo wetu ni vile tunatenda na kuishi katika maisha yetu nje ya kanisa, na vile tunatenda ndani ya kanisa. Mimi ningali mkristo ninapomkasirikia mke wangu, ninapomwambia bwana wangu kuwa sijihisi vyema ili niipambe nyumba yangu, au ninapokuwa na mawazo mabaya kanisani wakati kila mtu anamsifu na kumwabudu Bwana.

Ukristo ni kile mimi niko kwa kweli, na vile Mungu ananiona. Sio kile Ninaamini niko, au kile ninatabiri niko. Ukristo ni kutenda na moyo; vingivyo ni dini

ya uongo, na majivuno.

Wakristo wengi wainjilisti wangekubali kuwa kuiacha dunia na mwili na kuenda kwenye nyumba kubwa ya utawa sio kile Yesu alikusudia wengi wa wafuasi wake. Alisema kuwa tunafaa kuwa ndani ya dunia lakini sio wa dunia. Hata kama, hatufai kuwa wahakiki sana kwa watu ambao huenda kwenye nyumba kubwa ya ustawa kuikimbia dunia. Isipokuwa tunaweza ishi maisha ya utawa katika dunia, basi tunafaa kuwapenda hawa watu ambao wana ujasiri kurekebisha hatia yao.

Dunia ikituacha

Yesu kwa dhahiri alisema kuwa dunia ni ya Ibilisi na hatufai kuipenda, kutenda hivyo ni uzinzi wa kiroho na hatari kwa ukweli kwa ufupi tunaweza sema hivyo. Tukitaka kuwa wanafunzi, ama tunafaa kuiacha dunia, au dunia inafaa kutuacha.

Maandishi ya Yohana na Charles Wesley yamejawa na habari hii. Je walikuwa wamepotokwa na wamepitwa na wakati? Historia imedhibitisha kwa kweli kinyume; kwa kweli wasomi wengine wametafuta viini vyote vya kipaji cha mzunguko wa kipentekoste wa kisasa kwenye hiki kipindi cha historia ya kanisa, kwa hawa watu wawili.

Kile jamii yetu inahitaji leo sio watenda miujiza zaidi, au wainjilisti wakubwa (ambao watalilia nafsi kwa malipo),lakini watu watakatifu wa Mungu – Watu ambao kama Paulo huhesabu vitu vyote kama samadi

ili kushinda Kristo. Hakujawahi kuwa, na hakutawahi kuwa, njia nyingine kwa ufufuaji wa ukweli.

Wacha nidondoe kutoka kwa mume na mke wake wa nyimbo za kidini za Wesley ambao walizikwa chini ya maridhawa ya nyimbo za sifa na kuabudu za kisasa.

Wacha roho yangu isigawanye chochote
Kwani na wewe nimesulubiwa
Na kuishi kwa Mungu ndani yako
Kufa kwa dunia na wanaserere wake wote
Ufahari usio na kazi na kufufusha furaha
Yesu sifa yangu iwe

Moto takatifu ikienda ndani ndoyoni moyoni mwangu
Angaza nafsi yangu
Tawanyisha maisha yako kwa kila sehemu
Na usafishe yote

Ni dhahiri kwa kila mtu anayeenda kuishi kwenye nyumba kubwa ya ustawa, au mahali pengine pia pa kutengwa ameacha dunia; lakini ni ngumu sana kutambua ikiwa dunia imewaacha. Ni rahisi sana kujidanganya. Tunawezaje jua, au kujidhibitisha, kwamba dunia imetuacha? Yesu alisema kabla tu hajasulubiwa, Mwana mfalme wa dunia huja, lakini hana sehemu ndani yangu. Alimaanisha nini? Kwa urahisi hivi: kwamba hakukuwa na sehemu yoyote ya Yesu ambayo ilitaka chochote ambacho Ibilisi angetoa. Biblia inatueleza katika Yakobo 1:13-14

kuwa Mungu hamjaribu mtu… tunajaribiwa na tamaa zetu. Kwa hivyo ikiwa tamaa zetu ni safi, hatuwezi kujaribiwa.

Hapa kuna mtihani kwa sisi kutumia. Chochote basi ambacho hatuwezi ishi bila lazima kiwe na mshiko juu yetu, na kikiwa na mshiko juu yetu, basi hii inaweza maanisha tu kuwa hatuko huru kabisa.

Ikiwa unahisi kuwa hauwezi ishi bila pesa, gari, mke au mume wako, afya yako, muziki au michezo, basi hauko huru. Wacha tujikumbushe tena kwamba kujikana ni kama kukana vitu halali. Hakuna atakayependekeza kuwa familia, muziki au michezo ni vitu vya dhambi. Lakini acha tusisahau kuwa yeyote ambaye ni wako ambaye hayakani yote aliyonayo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.

Kokote katika historia ya kanisa wakristo wamelipata wazo hili kuwa ngumu sana kuelewa, na hubembea siku zote kutoka kiasi kimoja hadi kingine. Mifani miwili ifuatayo inafafanua ninachosema.

Televisheni

Wakati televisheni ilipopatikana kwa watu wote, wahubiri wengi huwa hawa "hellivisheni" na bado hawa wahubiri sasa wanavyo televisheni katika nyumba zao. Je walikuwa sawa kwa mara ya kwanza, na je sasa wamerudia mazoea yao mbaya, au je wako sawa sasa na walipotoshwa na kujibu zaidi kabla? Lazima tuwe waangalifu ili tusiangukie upande mmoja au mwingine; yote zaidi ni mbaya. Televisheni

ni chombo kinachosaidia upande wowote, lakini ujumbe wako hausaidii upande wowote. Dhambi ni ile ya mtengeneza programu, sio chombo chenyewe. Inaweza tumika kuhubiri injili. Televisheni imekuwa na athari ya kuogofya katika jamii yetu na athari yake imeathiri kanisa, na sio kwa uzuri.

Nafikiri unafaa kuwa mkristo imara kuwa na televisheni na kutoathiriwa nayo, Hiyo ni kuweka sharti kwa hali ya kufikiria ya kidunia. Millioni ya pauni iliyotumika kutangaza dhibitisho kuwa marudio ya ujumbe huo, faida hiyo hiyo, maadili hayo hayo ya jamii yatatuathiri kwa au bila ridhia yetu. Kuwa katika dunia na sio wa hiyo si rahisi. Kuwa na televisheni na kutoathiriwa ni ngumu sana kweli.

Pesa

Pesa ni mfano mwingine mzuri wa kanuni hii, ingawa hiyo itakuwa ukweli kwa kila nguvu za dunia hii.

Fedha ina nguvu ya kivyake. Biblia inaiita fedha iliyopatikana kwa njia mbaya na utajiri usio takatifu. Haya ni maneno yenye kushusha heshima, Mwanafunzi ni yule ambaye amenyanganya pesa nguvu zake ili isiwe ya kupenda na ambayo inaweza tumika kama ile ya ufalme wa Mungu. Pesa basi haina nguvu juu ya mtu huyu. Yeye haitegemei kwa kujiridhisha, usalama au maisha. Ana furaha bila pesa kama vile anayo. Usalama wake unatoka kwa Mungu pekee. Katika mahubiri katika mlima, Yesu

alisema, Usifikirie chakula, mavazi au hata maisha. Tia maanani alisema "usifadhaike." Anamaanisha "usisumbuke." Usiwache vitu hivi viwe na nguvu juu yako.

Yesu alikuwa na mweka hazina kati ya wanafunzi wake, Yuda ambaye "alikuwa na mfuko", Lakini inaonekana kwangu kuwa pesa haikuwa ya kumkimu kwa chakula na mavazi, au wanafunzi wake (na ni rahisi kusahau kuwa watu kumi na wawili wenye njaa wanafaa kula) Ninaamini alimtegemea Mungu kwa vitu hivi, na tunajua kuwa Mungu alitoa wanawake matajiri kuwapa mahitaji yao katika eneo hili.

Pesa kwa ushuru? Hakukuwa na lolote. Walihitaji miujiza. Yesu alikuwa na pochi ya mahitaji ya watu wengine. Mkoba ulikuwa wa kuwalisha maskini .Je Yuda mwenye tama alisema nini kuhusu lihamu ya bei ya Maria iliyofikiriwa kuwa Haifai? Hakusema "pesa hii ingetuvisha na kutulisha kwa wiki chache."Alisema kwa nini hii haikuuzwa na kuwapa maskini? Hata Yuda mlafi alijua kwa nini walikuwa na fedha na vile ingefaa kutumiwa. Yesu hakujali na pesa kana kwamba alimruhusuYuda ambaye alijua kutoka Mwanzo kuwa alikuwa mwizi, kuwa mwekahazina. Katika Mathayo 10, katika maagizo yake kwa wanafunzi alipowatuma nje kuhubiri na kuhudumu, aliwaamuru kuwa wasitume pesa. Huu ndio msingi na kwakweli ndio, lakini kwa sababu dunia kushika kwa uovu kama huo kwamba Tunahitaji kukaribia kiini kuweka huru ushikano wake kwetu.

Hakuna atakaye toka Misri bila kung'ang'ana

Wasomaji wengi wa Biblia wanakubali kuwa katika andiko, Misri ni mfano katika dunia. Misri ilihitaji tauni kumi ya kuteketeza kabla Farao hatimaye akubali watu wa Mungu kuenda; na si tofauti leo katika maisha yetu na katika mtindo wa dunia hii. Dunia haituwachi kwa urahisi. Ikiwa usalama wako kama mkristo ni sawa na zile za dunia, basi utakuwa na wakati mgumu kunidhibitishia kuwa Ukristo wako ni chochote zaidi ya wazo akilini mwako. Kusema kuwa unamwabudu Mungu anayeishi, aliyeumba vyote, na kuwa yeye ni kama baba kwako; kusema kuwa wewe ni mgeni, na nyumbani kwako kwa kweli sasa ni mbinguni, ni rahisi inakuwa dhihaka na matusi kwa mafunzo ya Yesu na mitume ikiwa hauishi hali tofauti ya maisha.

Ukweli ni kwamba wakristo wengi, hawaamini katika mbinguni. Kitu cha mwisho ambacho wangetaka ni kuruhusiwa kuwa katika maisha haya. Wanaifurahia sana, na hazina yao imewekwa kwa usalama kwenye nchi hii, sio mbinguni kamwe. Ninaweza taja siasa, mtindo, bima, burudani, michezo na maeneo mengine ambayo wakristo wamefuata, mafikirio na masharti ya dunia, bila kufahamu kuwa kwa kutenda hayo huwa siku zote na kwa udhabiti "wana weka hazina yao nchini", kitu kile kile ambacho Yesu alitueleza tusitende.

Historia imeonyesha kuwa kanisa limefanya enyeji mtindo wa akili ya dunia. Katika enzi za ufalme, makanisa yaliunga mkono ufalme, na chini ya serikali ya kidemokrasia, makanisa yanaunga mkono demokrasia na

kuongoza muundo wao kidemokrasia kama kwamba huu ulikuwa utaratibu ambao Mungu alichagua kwa serikali. Chachu kidogo husambaa bonge lote na ufisadi hungia kwa haraka. Chumvi kwa haraka hupoteza ladha yake.

Ukristo wa kweli lazima uwe wa kisiasa, na wakristo wanafaa kuwa tisho kwa mifumo yote ya kisiasa. Kwa kweli ufalme kweli wa Mungu ni uchaguzi badilli wa kweli kwenye mfumo wowote ambao mungu wa dunia hii anaweza toa.

Mateso au ulinganifu

Historia imeandikwa kuwa kanisa ya mapema ilifikiriwa na warumi kuwa tisho la kuangamiza kwa miundo yenye kuhusu raia na siasa, na waliwatesa sana. Mateso yaliisha tu wakati Constantine alikubali Ukristo na kuiweka dini rasmi ya ufalme wa kirumi, Tuliwekwa basi kwenye miaka elfu moja ya kutuama na duni katika historia ya kanisa. Hii inafaa kutajwa kama miaka ya giza.

Kitu hicho hicho kingetendeka leo kama kanisa lingetawala mifumo ya dunia, kwa kuwa wengi wa manabii wetu wanapendekeza kuwa inafaa na ita—Nina maanisha kusukuma kuelekea kwa kinachoitwa kuweka sanaa, utamaduni, siasa na mengineo kwa Ukristo, kana kwamba nguvu za kidunia zinaweza kwa njia zingine za kifumbo "kukombolewa."

Mwisho wa njia hii itaona kanisa ikiwekezwa na nguvu za kisiasa na wanasiasa wakiwekezwa na nguvu za kidini – kinyume kamili na kile Yesu alifundisha kwa dhahiri. Ninaweza angalia tu makosa mabaya ya

historia ya kanisa na kusema, Mungu apishie mbali kwamba isiwahi tendeka kabisa tena.

Lazima tuishi duniani, na lazima pia tufikirie na tutende tofauti na dunia, kukombolewa kutokana na nguvu zote ambazo ni za mfumo wa dunia. Lazima zivuliwe kwa athari yao kwetu ili badala yao kuwa tisho kwetu, tunakuwa athari kwao.

Ukristo wa kawaida

Tunapo angalia kwa ukaribu mafunzo ya Yesu hatutaachwa na shaka kuwa hii ndiyo anatarajia kwa wanafunzi wake. Hakuna mengi kuliko maisha ya Ukristo wa kawaida. Kwa nini hii inatoa hofushauri sana kwa watu wengi? Yesu alisema mara nyingi vitu kama Nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi… sijakuja kuwa shutumu, lakini kuwapa maisha tele. Kwa nini watu huunga mkono upande mmoja ua mwingine? Wanafukuza changamoto ya msalaba kama isiyopatikana na kujikana sana kwa jamii na kisiasa, au wananata kwenye "barua iliyokufa" ya sheria na kuwa mnafiki anayejifanya mtakatifu—watu wa dini walio maskini sana.

Nimekuja kwa hitimisho kuwa aina yote ya watu wamepotoshwa kwa sababu hawaelewi njia. Wanakosa furaha kubwa ambayo inatokana wakati utakatifu sio dhania na sio jambo la utashi. Katika sura zifuatazo ninatumai kuwa ninaweza kukuridhisha kuwa njia hii ni rahisi sana na yenye uhalisi kabisa, na moja ambayo inahitaji kuogopwa.

SURA YA SITA

Chukua Msalaba Wako

Umati ulikuwa unaimba "Nena Bwana wangu, Nena nami, Nena na nitakusikia kwa haraka"—na Mungu alinena. Sauti yake ilipasua mbingu na kunguruma ndani ya kanisa nilipokuwa nimeketi na umati huu wa watu. Miguu yangu ilitetemeka kama jeli, sauti ya Mungu ilikuwa yenye nguvu sana. Alisema, " Nenda juu ya mlima, ujitenge na ujitakase." Mungu amenena, nilijua ilifaa nitii. Mwili wangu ulisimama mwenyewe na kutoka nje ya kanisa na kusafiri kuelekea mlimani. Mwili wangu ulipokuwa unatembea, nafsi yangu ikauacha kwa dakika kuangalia nyuma mahali nilipokuwa nimetoka. Nilitarajia kuona umati uliobaki ukitembea pia kuelekea mlimani. Nilishangaa kwa kuwa Hakuna mtu mwingine aliyesikia sauti ya Mungu, au ikiwa walisikia, hawakulijibu. Ilikuwa ya sauti kubwa sana, na bado Hakuna liyesikia.

Nilifika chini ya mlima na kuangalia juu."Bwana," niliuliza "Je hii ni lazima, inakaa ovyo? nikienda juu mlimani nitarudi chini tena." Mungu amenena na niliogopa sana kutotii, kwa hivyo nikaenda juu mlimani. Mara ya kwanza, ilikuwa imefunikwa kwa kuvumwani, lakini ilibadilika na kuwa mwamba mgumu ambao ulipasua viatu vyangu na kuwariboni na kuvifanya bure. Usiku ulifika, na niliangalia mahali ambapo ningelala, lakini hakukuwa na kitanda au foronya laini ya kulalia. Tena nafsi yangu ikauacha mwili wangu na nikaangalia nyuma ya mahali palipoinuka ambapo nilikuwa ili kuangalia mahali nilipotoka. Niliwaona watu wakitoka kanisani na kuenda nyumbani kwa starehe za nyumba zao, vitanda moto na foronya laini, na nikasema, "Bwana, Je hii ni lama?" Lakini Mungu amenenana lazima nitii. Nilipoamka asubuhi nilikuwa na njaa sana. Nilitembea mbali juu ya mlima na bado sikupata chakula. Ilikuwa kama kufunga kwa kulazimishwa. Nafsi iliuacha mwili wangu tena na kuangalia nyuma na niliwaona watu wakila na kunywa vyakula vyao vya thamani, wakioa na kuolewa, na nikagundua nilichoacha nyuma. Nikauliza tena "Bwana, je hii ni ya maana?" lakini Bwana amenena na lazima nitii. Mwishowe Nilifika kileo, lakini sikuwa nimejitayarisha kwa kile nilichoona pale. Hili lilikuwa jaribio kubwa sana la utiifu wangu. Mwili wangu nayo kwa nguvu "Bwana, je hii ni ya maana?"mbele

yangu niliona madhabahu ya sadaka ya jiwe baridi na kando yake kisu ambacho kingeua sadaka. Nilitaka sana kukata tama katika hatua hii lakini nilikuwa Nimekuja umbali huu na ilikuwa mbaya zaidi kuliko kifo kutotii sauti ya Mungu. Maandiko katika Warumi 12:1 ilikuja akilini mwangu, itoeni miili yenyu iwe dhabihu iliyohai, takatifu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Kwa hivyo nikalala chini kwenye ubamba na kuingiza kisu mwilini mwangu. Nilipofanya hivi andiko linguine kutoka Mathayo 16:25 likaja akilini mwangu, Mtu anayetaka kuiokoa nafsi yake, ataipoteza, na mtu atakayeipoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona. Kisha nikaiona nafsi yangu ikiuacha mwili wangu tena, na mara hii sikurudi, kwa kuwa mwili wangu ulikuwa umekufa. Sasa nilikuwa huru kabisa kwa sababu ilikuwa mwili ndio iliyopitia mateso na usumbufu huo wote, njaa na kifo, siyo nafsi yangu. Mwishowe niliwekwa huru kwa hivyo ningeweza rudi chini ya mlima kutenda mapenzi ya Mungu bila vizuizi kabisa

Joanna Barratt

Wacha sasa tuangalie sharti la pili ambalo Yesu anampa mtu ambaye ameitwa kuwa mwanafunzi. Chukua msalaba wako . Sharti la kwanza; Jikane, ni kuhusu dunia na jinsi tunavyofaa kuishi ndani yake bila ya kuwa sehemu yake; ni kuhusu hali yetu ya maisha ya nje. Lakini sharti hili la pili ni tofauti kabisa. Ni kuhusu undani wetu, au maisha ya siri.

Msalaba mbaya

Huwa tuna shangaza jinsi hali nyingi tofauti Wakristo wataita msalaba wao. Hapa kuna mifano michache ya kawaida ambayo yamesikika; Nina hakika umeyasikia.

Ugonjwa ambao unaendelea hata baada ya matibabu na maombi. Kwa kukata tama mtu atasema, ”nitastahimili tu unaweza kuwa ni msalaba wangu.”

Mtu aliyeolewa na asiyeamini. Wachungaji wao na marafiki wanaombea mwenzi wao, lakini Hakuna kinachobadilika. Wanafunga na kuomba lakini hawajui nini tena lakufanya, kwa hivyo wanasema” lazima uwe ni msalaba wangu” Nadhani kila mkristo ana moja.

Hali ya kazi mara nyingi huleta “misalaba” yetu. Mwajiri wangu yuko nami kwa sababu mimi ni mkristo. Yeye hungoja nafasi ili kupata kosa kwa kazi yangu. Nimemwomba Mungu anipe kazi nyingine, nimeomba ili bwana aende, lakini sote bado tupo hapo. Lazima uwe msalaba wangu wakuninyenyekeza.

Kawaida kwa mwanadamu

Tunaweza mara moja achana na hii misalaba. Mifano hii yote ni hali zinazohusiana na hali ya kiinje ambayo tungependa kubadilisha. Sisemi kuwa hali hizi ni nzuri au kwamba hayahitaji mabadiliko, ninachotaka kudhihirisha ni kwamba hawana chochote kabisa la kutenda na msalaba

wetu. Nitapeana mifano miwili kuegemeza kauli yangu. Ya kwanza ni hii: ikiwa hali hizi za kiinje ndizo msalaba, basi kila mtu duniani anafaa kuwa na msalaba wa kubeba wakati mwingine maishani mwao, kwa sababu kama vile Paulo anasema katika Wakorintho wa kwanza 10:13, hali hizo ni kawaida kwa mwanadamu.

Hali zinazotendeka kwa wasio- Wakristo pia zinatendeka kwa wakristo kinyume na imani ya wakristo wengi, Mungu hawaahidi kuwa huru kwa shida au maisha mazuri. Biblia haisemi kuwa tutatengwa kutoka kwa hali hizo hizo, mashida na mali ambazo dunia inapata.

Jaribio

Jaribu jaribio hili dogo ikiwa una shaka yoyote. Andika majina ya wakristo kumi. Weka mchungaji wako na mwinjilisti wako bora kisha andika majina ya watu kumi ambao unajua sio wakristo. Weka mwajiri wako kazini na huenda watu wengine.

Sasa linganishwa kwa kweli uzoefu wao wa maisha utapata kwamba Hakuna tofauti. Utapata kuwa wakristo wamepata vishindo vya magari, wamekufa kabla ya miaka ya uzee, wamewapoteza watoto wao wakiwa wachanga, na wamepata mishtuko ya mioyo—vitu vyote ambavyo ni vya kawaida kwa watu wote. Kwa upande mwingine, watu wengine wasio wakristo wanaishi maisha mazuri! Afya, utajiri na uwezo unawafuata kwa yote wanayotenda. Soma

Mhubiri kwa ukadiriaji wa Solomoni wa mada hii. Hii inafaa kuwadhihirisha ya kutosha kwamba msalaba ndio tumeelezwa tuchukue na sio hali yetu ya kiinje.

Chukua msalaba wako

Sababu la pili kwa nini hali kwa hali ngumu au hata yenye huzuni sio msalaba ni hili ambazo nimeeleza zinahusiana na hali ambazo tungependa kubadilisha, na kwa hii sababu inawatoa kutoka kwa yale ambayo Yesu anasema. Nitadondoa kamili Yesu alichosema ili kutilia mkazo kauli hii. Wacha auchukue msalaba wake. Msalaba ambao Yesu anataja ni msalaba ambao tunauchukua, sio ambao umewekwa juu yetu; na hali kuwa kwa ufafanuzi "Weka juu yetu" Jiulize, Je utachagua kuwa na magonjwa, ndoa isio na furaha, au mazingira mabaya ya kazi? Hapana! Kwa hivyo tunaweza weka kando wazo kuwa hali ngumu inahusu msalaba.

Kwa umbali huu tumeangalia tu hali hasi—kile msalaba sio—kwa hivyo lazima tuamue kwa makini ni nini ambalo lazima tu "chukue" halisi.

Ingemaanisha nini kwa Petro na wanafunzi wengine waliposikia maneno haya? Kwao ingekuwa dhahiri kwa kuwa walikuwa chini ya umiliki wa Warumi, na Maelfu ya wavunja sheria walisulubishwa kwenye misalaba ya Warumi.

Fedheha ya wengi wa wajinai ilikuwa kuwa walitakiwa kuubeba msalaba huohuo ambao wangesulubiishwa nao. Wanafunzi walijua kuwa

walikuwa tu sababu moja yeyote angechukua msalaba—kusulubiwa.

Kifo cha mwenyewe

Dietrich Bonhoeffer, katika kitabu chake "Gharama ya uanafunzi" anasema kuwa " Kristo anapomuita mtu, humwambia njoo na ufe" Huu sio uvumishaji au kudai kabisa. Hakuna uchaguzi badilli mwingine, Yesu hakuwa akisema kuwa tunafaa kusulubiwa kimwili, katika injili ya Luka anasema, chukua msalaba wako kila siku, Hata hivyo hakuwezi kuwa na ufafanuzi mwingine wa maneno ya Yesu isipokuwa kifo. Kwa hivyo ni nini kinachofaa kufa kama sio maisha yetu ya kufa? Paulo anaweza kutusaidia kuelewa, kwa kuwa anaongea kuhusu kusulubiwa katika barua zake kwa kanisa.

Warumi 6:6 inasema, utu wetu wa kale ulisulubiwa na Yesu. Paulo katika muktadha wake anazungumza kuhusu ubatizo, lakini inatupa dhahiri uhusiano na "mtu wa kale" Hii ni sawa na mwili, yote kuhusiana na mambo ya dhambi yenye uasi ambayo sote tunaridhi tunapozaliwa na Adamu.

Katika Wagalatia 5:24 mara tu baada ya Paulo alijitambulisha na kazi ya kimwili (mambo ya kitambo) na tunda la roho mtakatifu(mambo mapya ya Kristo) anasema, Na hao walio wa Kristo wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tama zake.

Maandiko haya mawili yanatuonyesha dhahiri kile kinachofaa kusulubiwa kwa mkristo. Sio maisha yetu

ya nje lakini tabia yetu ya kindani. Hii ndio maana kuuchukua msalaba ni tofauti kabisa na kujikana wenyewe. Kujikana wenyewe kunahusiana na tabia yetu ya nje na hali ya maisha; kuuchukua msalaba kunahusiana na tabia yetu ya ndani, mwili. Hii ndio nia yote ya maisha yetu ya Kikristo, kubadilika kutoka kwa tabia za Adamu hadi kwa tabia za mwajiri wetu mgeni, Kristo. Paulo anasema katika Waefeso 4:11, Mungu alitoa wengine kwa mitume, manabii, Wainjilisti, Wachungaji na Walimu ili kuwakamilisha watakatifu… hata kufika kwenye mtu kamilifu, kwenye cheo cha kimo, cha utimilifu wa Kristo.

Tusiwahi jifanya kwa kifo kwa njia yoyote ni ya kupendeza. Katika mwili wetu au tabia yetu ya ndani, uoga wa asili wa kifo ni kawaida kwa mwanadamu kujua na kukabiliana na ukweli huu inaweza kutuliwaza, kwa kuwa msimamizi wetu na kiongozi alistahimili msalaba kwa furaha iliyokuwa mbele yake. Haisemi kuwa alifurahia msalaba, inasema kuwa aliangalia mbele yake kwa furaha iliyomngojea—ufufuko ambao unafanya msalaba kuwa kwenye manufaa.

Kusulubiwa na Kristo

Kama wakristo wangeona zaidi ya kifo cha mwenyewe kwa maisha mapya ukawaida wa Kristo, wangekuwa na msimamo tofauti kwa Ukristo wao. Kile ambacho huweka kifo cha mwenyewe ushindi wenye furaha ni maisha ya kufufuka ya Yesu Kristo

kudhihirishwa kwenye maisha yetu ya kufa.

Uelewekaji wa hii unaweka azimio la Paulo katika Wagalatia 2:20 kuchukua nia moja: Nimesulubiwa pamoja na Yesu: Lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu, na uhai nilio nao sasa katika mwili ninao katika imani ya mwana wa Mungu.

Ni tu wakati wenyewe utakufa ndio Yesu anaweza ishi maisha yake ndani yangu. Hakuna aliye katika mwili anaweza ishi maisha ya mkristo. Ni mnafiki tu anayeweza itenda kwa mafanikio. Ni Kristo tu anayeweza ishi maisha ndani yetu,lakini yeye ndiye maisha, na ataishi maisha yake kwa miili yetu ikiwa tutakufa kwa wenyewe. Huu ni uhuru wa kweli. Paulo alisema kuwa aliishi kwa imani ya mwana wa Mungu. Haikuwa imani ndani ya mwana wa Mungu. Paulo pia hakuishi kwa imani yake mwenyewe! Mtu aliyekufa hawezi kuwa na imani. Aliishi kwa imani ya Yesu ndani yake. Ukweli huu wa ajabu, kuwa ni imani ya Kristo, sio yetu, huenda mara moja na kupambana kwetu na "fikra –kwa- mambo" hali ya imani, ambayo inachagua tu kiburi cha mateso.

Maisha kwa maisha

Kujikana inahusiana na dunia na maisha yetu ya nje inayoonekana ndani yake. Lakini msalaba inahusiana na mwili, hali yetu ya ndani ya kawaida ambayo ni kwa kweli maisha yetu ya siri, haihusiani na maadili yetu ya nje. Inahusiana na moyo, kiti chenyewe cha malengo yetu, nia zetu za siri, na tamaa, vitu ambavyo

vimefichwa kutokana na wake au waume zetu, mchungaji au Rafiki wa karibu na mara kwa mara hata kufichwa kutoka kwetu wenyewe.

Katika Biblia "akili" inamaanisha fahamu zetu za kimawazo lakini "moyo" una maana sana – mawazo yetu yaliyofichika akilini. Ni tama yetu ya kisiri, nia na ashiki. Tunaweza jua kile tunafikiria, lakini tunajidanganya ikiwa tunafikiria kuwa tunaelewa kwanini tunafikiria.

Biblia inatueleza tufanye upya akili zetu kwa sababu tuna uwezo wa huu mtindo wa kufahamu, lakini haituelezi tufanye uupya mioyo yetu. Daudi alimueleza Mungu aujaribu moyo wake na kuuchunguza aone ikiwa kulikuwa na njia yoyote ovu ndani mwake. Yeremia 17:9 inasema Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha, nani awezaye kujua? Huwa mdanganyifu kwamba inakudanganya katika kuamini kuwa ni takatifu.

Nia yangu yote ya kufafanua haya ni kusisitiza kuwa msalaba unaambatana na maisha yetu ya kisiri, na nitaitumia hivi katika sura hii yote.

Wacha nitambue mawazo mengine matamu kuhusu kujisulubisha—mwenyewe. La kwanza ni kwamba kukimbia kutoka kwa dunia na majaribio yake haiwezi jihusisha na mwili. Tunaweza zuia majaribu mengine ambayo yatatuongoza kwa dhambi, kwa kuyaondoa, au kuyazuia kimwili, lakini hii haitawahi husiana na maisha yetu ya kisiri.

Nyumba kubwa ya utawa haiwezi ua miili yetu

Nyumba kubwa ya utawa ni mfano kubwa wa tamaa ya ukweli ya watu kujikinga kutokana na majaribu ya kimwili, lakini hiyo inaweza feli, kwa sababu uenyewe ni maisha ya ndani ambao mtu huchukuwa kwenye nyumba kubwa ya ustawa; Hakuna anayeweza jitorosha mwenyewe. Kwa mfano, tunaweza toroka uovu wa kiinje kwa kuishi ndani ya nyumba ya ustawa, na bado kulala kwenye kitanda kidogo cha jiwe na chakula kidogo mwilini mwetu na kuota maovu na kuwa na tama inayochoma moyoni mwetu.

Nilikuwa mkosoaji sana wa watu ambao waliiacha dunia na kuingia kwenye nyumba kubwa la utawa. Niliwashukumu kwa ukweli lakini nilitambua kuwa nisipoishi maisha ya utawa nikiwa bado sina haki ya kuwahakiki hao watu ambao ujasiri wa kujiona na

Mradi tu bado tukiwa hai wenyewe tutakuwa na shida hii, na kadiri ya hayo Yesu anatupa tiba – kufa kwa kusulubiwa, inavyofaa Hakuna suluhisho nyingine.

Wazo langu la pili ni kwamba chochote na enyewe—kama tangulizi kinafaa kuwa onyo akilini mwetu. Maneno kama kuendelea mwenyewe, kujiheshmu mwenyewe, kujidhamini mwenyewe, kuridhika (ambalo ni njia tu la kusema kujiridhisha mwenyewe), yote ni njia ya kujiweka hai na kuwa na afya. Yesu alisema kinyume ya hayo Jikane mwenyewe. Mwenyewe ni mbaya; lazima liharibiwe .

enyewe inaambatana na kiburi, na ubinafsi, chochote ambacho kinajisifu mbali na Mungu. Lakini inawezaje kana enyewe? Tunawezaje haribu enyewe ambayo tunapenda? Ingawaje inakaa haiwezekani, kwa namna nyingine enyewe lazima iende kwa sababu hii: Mungu hagawi utukufu wake na mwili. Wahusika wawili hawawezi tawala mwili mmoja mara moja.

Kuna kanuni gani ambayo imeenea siku hizi, na wakristo wengi wameikubali bila kufikiria. Njia yao ya kufikiria ni sawa na hii. Yesu alisema mpende jirani yako kama unavyo jipenda mwenyewe, hadi utakapojifunza kujipenda, kwa hivyo hauwezi mpenda jirani yako hadi utakapojifunza kujipenda mwenyewe. Unafaa kuwa na mfano mwema wa mwenyewe na uanze kujipenda kama Mungu anavyo kupenda.

Mantiki iliyozungushwa

Hii inaweka kuzungushwa kwa hali ya kuonekana, lakini Ninaamini ni mantiki iliyozungushwa na hatari sana. Wacha nifafanue kwa nini.

Biblia inasema kuwa kujipenda mwenyewe ni kinyume na kile Mungu anataka, kwa kuwa huwezi kumpenda Mungu na wewe mwenyewe mara moja. Watu wanaposema kuwa wana "jichukia wenyewe" wanadanganyika. Wanafafanua hisia zao kama kujichukia—mwenyewe, lakini kwa kweli ni kujihurumia mwenyewe au kiburi kilichopinduliwa kwa sababu ikiwa waliji— chukia wenyewe

wangefurahi kuwa na sura duni mwenyewe! Kwa hivyo masharti haya ya moyo ni kinyume sana na vile yanaonekana. Kujihurumia ni hali tu ya kujipenda, kwa kuwa wakati wowote uangalifu uko kwetu badala ya Mungu tuko kwa hatari, Yesu alisema tunafaa kujikana, sio kujipenda. Paulo anasema katika Waefeso 5:29, Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake popote, bali huulisha na kuutunza. Yesu anatueleza tujikane wenyewe kwa sababu anajua kuwa sote twajipenda bila kufikiria na kujishawishi kwa tama zetu. Alikuwa anasema kuwa tunafaa pia kuwatendea majirani wetu kwa njia hiyo ya kutojifikiria. Yesu alionyesha katika hadithi ya msamaria mwema kuwa jirani yetu pia ni adui yetu.

Kujisulubisha mwenyewe haiwezekani

Hakuna mtu mwaminifu anayeweza sema utamu wa wazo la maisha yake ya siri kuwekwa wazi na kuaibishwa. Kwa hivyo wazo langu la tatu Unafaa kutupa matumaini. Haiwezekani kujisulubisha mwenyewe. Kusulubisha sio njia iwezekanayo ya kujiua. Mhusika anaweza kuwa anataka, lakini hangeweza tenda kitendo mwenyewe. Atahitaji mikono miwili hata kuupiga msumari wa kwanza kwake mwenyewe. Wazo langu ni kuwa kinachotumika kwenye usulubishaji wa kiinje ni hasa kweli na usulubishaji wa kindani wa mwili: hatuwezi litenda wenyewe.

Ni ya maana kubwa sana kwamba tushike ukweli

huu. Hatuwezi songa mbele zaidi kwa mwendo wetu na Mungu tusipo. watu ambao wanajaribu kukabiliana na maisha yao ya siri wenyewe watapata kuwa hii inaweza isha tu kwa moja ya matokeo mawili, na hakuna kati yao ile ambayo ina athari yoyote kwenye maisha yao ya kitambo. pengine watajifanya kuwa wanakuwa watakatifu, na kujifanya kwa hali ya tabia ya kiinje (ambayo ni unafiki tu) ama watakuwa kweli kwa wenyewe, wakijiona wenyewe kama walivyo, na bado kuhisi kujishutumu, kujihukumu kuwa mkristo wa tabaka la pili, bila matumaini ya kuinuka.

Je ukweli kuwa hatuwezi kujisulubisha inawezaje kuwa matumaini? Wacha nifafanue. Ikiwa hatuwezi kujisulubisha basi lazima itatendeka licha yetu—mtu mwingine atatusulubisha; ambaye ni Mungu.ni kazi yake sio yetu. msisitizo kisha unabadilika, kwa sababu sehemu yetu ni kuwa tunafaa kuwa tayari ili itendeke. Hii ni matumaini kwa kweli, kwa sababu utakatifu wa kweli (kama ilivyo kwenye hali ya heri) lazima iwe isiyo ya kutodhania, utakatifu ambao umejificha ambao hata umejificha kwetu wenyewe .chochote tunafanya wenyewe huwa ni kitu ambacho tunaenda kufikiria, "kitu" ambayo tunaweza ringa juu yake(kwetu kama sio kwa mtu mwingine). Lakini ikiwa kazi haijatendwa nasi, na hatujichungi nayo, utakatifu wetu unakuwa "usio dhania"

Kupambana na maisha ya siri

Nimedhibitisha kuwa Mungu atatufanyia kazi hii

ikiwa kwakweli tunataka, kwa sababu ndio jawabu tu kwa shida yetu ya jinsi ya kuwa mtakatifu. Ni zaidi tu ya Yesu ndani yetu inayo tufanya kuwa kama yeye. Hakuna chochote kinachoweza fanya. mengine yanatoa tu uongo na unafiki.

Hata hivyo, Hakuna shida. Mungu hatatufanyia kazi hii kwa sababu tu tumemuambia. Anahitaji zaidi ya maneno yetu. Kuongea pekee haitoshi. Tunaweza kosa kuamini. Tunafaa kufanya kitu kudhibitisha nia na tama yetu, na hiyo n kuwa mtiifu na vitu ambavyo Yesu anatueleza tufanye, vitu ambavyo si vigumu sana kwetu, vitu ambavyo tunaweza fanya. Tunafaa kufanya vitu hivi, kumdhibitishia Mungu kuwa tunamaanisha kile tunasema, kabla abadilishe vitu ambavyo hatuwezi fanya – vitu ambavyo tumekuwa tukijaribu kufanya lakini yanatupa shida.

Jawabu ya shida ya maisha yetu ya siri ni maisha nyingine ya siri—ninachoita maisha ya siri ya mfuasi. Katika Mathayo 6, Yesu anatueleza vitu vitatu ambayo lazima tufanye kwa siri. Sababu tunafaa kufanya vitu hivi ni kwa mpangilio kudhibitisha nia yetu kwa Mungu, na kwetu wenyewe; kumdhibitishia Mungu kuwa tunaifanya kwa sifa yake pekee, na sio sifa ya wanadamu. Hii ni funguo kuu kwa maisha ya mkristo, na vitu ambavyo Yesu anatuuliza tufanye yote yanawezekana kabisa, hata kwa mbadili dini mgeni.

Wacha tukumbuke kuwa msalaba ni kitu ambacho tunachukua, sio kitu ambacho kinawekwa juu yetu. Lazima tuichukue maisha hii ya siri. Injili ya Luka inasema lazima tuichukue kila siku. Utakatifu

sio tendo au amini; ni njia, na hiyo inamaanisha wakati. hakuna njia ya haraka ya kuwa mtakatifu. Uzoefu na mateso yote ni mojawapo ya nia hii. Paulo anasema katika Timotheo wa pili 3:12 Na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa na katika Waebrania 2:10, kumkamilisha kiongozi wa wokovu wao kwa njia ya mateso. mkristo atakuwaje kipofu kufikiria kuwa baraka pekee yangebadilisha tabia yetu kwa uzuri! Kwa bahati mbaya, baraka yatajaa vichwani mwetu kuliko mioyoni mwetu. Mafanikio huwa haimnyenyekezi mtu sana au kumfanya mtakatifu.

Kutembea katika roho

Nimeridhishwa kuwa ni maisha tu ya siri na Mungu, maisha ya siri ya mfuasi, kufanya mambo ambayo Yesu anaamuru, yanaweza kuzuia maisha ya siri ya Adamu ambayo tumerithi, na ambayo sote tunafaa kupambana nayo kila siku.

Wacha nifunge sehemu hii na maneno ya Paulo katika Wagalatia 5:16 Basi nasema enendeni kwa roho, wala hamtazitimiza kamwe tama za mwili. Hasemi kuwa wakristo hawana tamaa za mwili. lakini anamaanisha kuwa yako, lakini kuwa tukitembea kwa roho hatutayatimiza. Hii ni tofauti kabisa kwa kusema kuwa tama hii. Au hali ya kitambo , haiko kamwe. Paulo anatueleza kuwa tunaweza pata ushindi dhidi yao kwa kutimiza sharti; Lazima tutembee kwa roho—hiyo ni, hali mpya

SURA YA 7

Nifuate

"Nifuate" ndilo agizo la tatu na la mwisho ambalo Yesu aliwapa wale ambao Walitaka kuwa wanafunzi wake. Tumeshaandika kuwa tungetarajia "kufuata" kuwa agizo la kwanza, na mwanzoni mwa mwendo wetu wa Kikristo, sio hatua ya mwisho katika uendeleaji. Lakini lazima tuelewe kuwa "ufuataji" wa kweli ndio tukio tu la kutii maagizo mbili ya kwanza.

Tukio la kawaida

Hii ndio njia ya pekee ya kuwa mfuasi. Mtu anayefikiria anaweza kumfuata Yesu bila kujikana na kuchukua msalaba wake anajidanganya. Mfano mwema ni kiongozi mchanga tajiri, ambaye aliamini kuwa alikuwa akifanya mapenzi ya Mungu hadi Yesu alipomweka wazi. Alirudi kwa huzuni kwa sababu

hakuweza au hakutaka kulipa deni la uanafunzi.

Katika ulinganisho wangu wa maagizo wa maagizo haya matatu na "dunia, mwilini na shetani" kumfuata yesu ni sawa na kuwa na muwasala na shetani. Tunapozingatia kuwa kumfuata Yesu kunamaanisha kuenda alipoenda, kufanya alichofanya, na tunapokumbuka kuwa nia yake ilikuwa ni kuangamiza kazi za shetani, tunaweza elewa kuwa tunapofikia hatua ya kumfuata Yesu, Sisi pia tutaangamiza kazi ya shetani – Lakini tunapokumbana na maagizo mbili ya kwanza.

Taratibu ovu

Uharibifu wa kazi ya shetani inaweza pia onekana kuwa katika mahali pabaya kwenye mfuatano. Kwa hivyo wakristo wengi wanafikiria kuwa ikiwa wameokolewa na kujazwa na Roho Mtakatifu, basi wanaweza anza mara hiyo "kumuangamiza shetani" kabla hata wafikirie kujikana wenyewe au kuuchukua msalaba wao.kwa kweli wanaweza kuwa na uwezo wa kuangamiza kazi za shetani, lakini hiyo haiwastahilishi kuichukua nafasi hiyo kabla hawajakomaa.

Kijana wangu mdogo wa miaka mitano anaweza kuwa na na uwezo wa kuwa Waziri mkuu, lakini hiyo kwa kweli haimstahilishi kwa kuichukua nafasi hiyo leo! Ni ukomafu ndio anakosa na shida hiyo hiyo iko wakati wakristo wanafikiria kuwa wamekomaa kwa sababu tu wameokoka. Ukomafu hauwezi kuja haraka, kwa sababu ukomafu unakuja tu kutokana na

uzoefu, na uzoefu huchukuwa muda.

Karama bila tunda

Katika Wakorintho 12:7 Paulo anasema kuwa karama tisa za Roho mtakatifu ni ufunuo wa Roho. Hii inamaanisha kuwa zinaonekana na kutazamika. karama ya uponyaji haitendeki kwa akili yetu iliyofichika; zinaathiri mabadiliko ya nje ya mwili wetu. Paulo anasema karama tisa zote zinatoka kwa Roho mmoja. Zina dhihirisha nguvu za Mungu.

Kuna, hata hivyo, orodha nyingine katika Wagalatia 5:22-23: Tunda la Roho. Tena kuna tabia tisa, lakini Ninaamini kuwa haya hayana uhusiano wowote na nguvu na udhihirisho unaoonekana wa Mungu. Ishara hizi au ubora huu ndio tabia ya Mungu.

Je mtu anaweza kuwa na nguvu za Mungu bila tabia ya Mungu? Kuiweka kwa njia nyingine, je mtu anaweza kuwa na karama bila matunda? Hatufai kuogopa kuuliza swali hili, kwa kuwa ni la maana. Nina asilimia mia moja hakika kwamba jawabu la Maswali haya yote ni ndiyo na kwa kweli ni mara kwa mara jambo la ufunuo wa kupita akili. Yesu mwenyewe anatoa ushahidi mmoja wa hii, kwa katika Mathayo 7:22 alisema kuwa katika siku ya kiyama , wengi watasema, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo? na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?

Walikuwa wakiuliza Maswali, lakini pia wakilalamikia haki zao kuingia kwenye ufalme. Ni

jawabu gani ambalo Yesu aliwapa? Je alikataa madai yao na kusema kuwa miujiza yao haikuwa kwa jina lake? Hapana, alikubali kuwa maelezo yao yalikuwa ukweli, lakini hata hivyo, jawabu lao lilikuwa kuwa hawajui. Hawakuwa wana wake. Walikuwa kama wafarisayo, ambao Yesu alisema walikuwa wa baba yao shetani. Na walikuwa wakitenda miujiza. Inawezekana kuwa mwana wa shetani na kutenda miujiza kwa jina la Yesu.

Mungu mwenye nguvu yote

Wacha niulize swali nyingine ambalo litatusaidia kuelewa hii.

Je shetani alijiumba? Jawabu lazima iwe la, kwa sababu ni Mungu tu anayeweza kuomba. Tukikubali kama ukweli, basi ni wazi kuwa shetani hana nguvu zake mwenyewe. Hakuna nguvu duniani isipokuwa ya Mungu. Tunaweza itumia vizuri au vibaya, lakini Mungu ana nguvu zote , ambayo inamaanisha hakuna nguvu iliyobaki kwa mtu yeyote. Katika Wakorintho wa kwanza 13, ambapo Paulo anatofautisha karama na matunda, anasema katika mstari wa 2 ninapotumia karama na sina upendo (upendo ni neno moja ambalo linafafanua matunda)basi MIMI NI BURE. Mungu hawezi kututambua iwapo hakuna lolote lenye tabia yake ndani mwetu. Karama zinadhihirisha kuwa tuna nguvu za Mungu; lakini hazidhihirishi kuwa sisi ni wana wa Mungu. Shetani mwenyewe anaweza tumia tu nguvu za Mungu kwa kuwa hakuna

nguvu zingine, na Mungu amempa shetani nguvu za kipimo fulani.

Yesu, akizungumza kuhusu manabii wa uongo na jinsi ya kuwatambua, anasema katika Mathayo 7:20 Mtawatambua kwa matunda yao (sio kwa karama zao). Anawaita hao walio na karama na bila matunda mbwa mwitu ndani ya ngozi ya kondoo. Ni ngumu kuelewa kwa nini kanisa imepuuzia kutumia jaribio hili, ambalo Yesu alitupa kama kinga kwetu.

Kupambana na shetani

Adui wetu, shetani, si mjinga, wala hajagandamizwa na jina la Yesu, Isipokuwa tabia ya Yesu iko ndani ya mtu anaye zungumzia hilo jina. shetani hutumia jina la Yesu mara kwa mara kama kufuru. Hata hivyo, anawaogopa watu ambao hawako katika sehemu ya mfumo wake (dunia), na hao ambao wameusulubisha mwili, haoni, watu watakatifu. Hii ndiyo maana, licha ya kipaji chetu, nguvu zetu za kipentekoste, na makelele yetu yote kwa shetani na kumueleza kuwa ameshindwa, hatujaleta katika jamii yetu ya Ushuhuda. Tunafaa kuzingatia kwa uangalifu jinsi mababu zetu walivyoleta jamii yote kwa kutubu bila vipaji hivi.

Je maneno haya yanadokeza kuwa niko kinyume na vipaji vya roho mtakatifu? Hata hivyo, ninayaamini haya yote, na ninaamini kuwa tunayahitaji katika miaka yetu ya kisasa. Ninaamini katika unabii na maono, kutembelewa na malaika na vipaji vya Roho

mtakatifu haviwezi kuzaa tunda. Zinaweza tu kuzaa nguvu. Kuvumilia kwenye mzabibu ndio kitu pekee ambacho kitazaa tunda.

Nchi yetu haihitaji tena wafuasi wa Yesu; inahitaji wanafunzi wa Yesu. Haihitaji wahubiri wengine; inahitaji watu wengi wa Mungu, wahubiri wengine watakatifu—sio watu ambao wanalilia nafsi kwa sababu wanalipwa kufanya hivyo, au hao ambao wataponya magonjwa kwa sababu italeta umati, umaarufu na fedha, lakini watu ambao watafanya mambo haya kwa sababu wana tabia ya Kristo; watu ambao wako kama Yesu, ambao wamejawa na huruma. Kuna dunia ya utofauti kati ya hizi mbili, na hata kama kanisa haiwezi tambua, adui wetu shetani anaweza.

Masharti ya ufufuo

Wa pili 7:14 inatueleza kuwa masharti manne yanayohitajika kwenye ufufuo, na sio kwamba moja yao inaambatana na vita vya kiroho au kupigana na shetani. Yanaambatana na Mungu, hakimu wa nchi yote. Ikiwa watu wangu watanyenyekea, kuomba na kuutafuta uso wangu, na kubadilisha njia zao ovu… Nitaiponya nchi yao. Ufufuo ni haki ya Mungu na sio haki yetu, na hiyo ndio maana tunafaa kufuata masharti na sio tu kusema maneno sawa ya Mungu au shetani. Soma katika Matendo ya mitume19:13-26 jinsi wana wa Skeva walijaribu, kwa kusema maneno sawa, kufukuza pepo, na matokeo ya kustaajabisha,

shetani aliwaambia “siwajui Ninamjua Yesu, ninamjua Paulo, lakini ninyi ni akina nani?” Kusema maneno sawa au hata kufanya kazi sawa, haitoshi, ni tabia ya nani ambayo unayo ndani yako.

Yesu alisema kwenye mahubiri mlimani kuwa watu wengi watasimama mbele yake siku ya hukumu na kumkumbusha juu ya kazi muujiza ambayo walifanya kwa jina lake. Yesu alikubali kuwa walifanya kazi hii, lakini jawabu lake kwao ilikuwa “siwajui” Hakukuwa na tabia yake ndani yao.

Naipata ya kufurahisha kuwa shetani alisema maneno sawa kama Yesu, “Siwajui” walikuwa wote wakitafuta tabia moja pekee –tabia ya Yesu.

SURA YA 8

Musa

Masharti matatu ambayo yesu anatupa ya uanafunzi ni missing na la kushangaza, chanzo chao sio kwenye Agano jipya. Maadili ya kuishi kiMungu na njia za utakatifu hazibadiliki katika Biblia yote. Katika mifano ifuatayo kutoka kwenye Agano la kale na jipya tutaona kuwa kabla Mungu amuamini na amtume mtu kwa nia zake, lazima kuwe na maendeleo katika hatua zote tatu—Kujikana mwenyewe (kupambana na dunia), Kuuchukua msalaba (Kupambana na mwili), na kumfuata yesu(Kupambana na shetani).

Kutoka Misri

Musa alilelewa Misri, ufalme mkuu wa kiutamaduni, na kuelimishwa kama mwana wa Farao. Ikiwa Misri ni mfano wa dunia, kama vile wasomi wengi wa Biblia wanakubali, Musa alikuwa mkuu na aliyefanikiwa

nchini. Alilelewa na umbuji na majivuno ya nchi hii kuu.

Kwa uchokozi, Musa aliyafanya yaliyo ya kawaida kwa hali yake ya Adamu kutenda. Aliona mmoja wa Wahebrania wenzake akiteswa, akamuua mmisri mkandamizaji, na kumweka huru mtumwa. Hili halikuwa suluhisho la kudumu, kwa kweli, kwa bila shaka msimamizi mwingine katili kama yeye atambadilisha mfu. Ilikuwa tu faraja ya muda mfupi; Lakini Mungu alikuwa na nia kuu – alitumia hali hizi, kwa kuwa Musa alitorokea maisha yake.

Takdiri

Nina uhakika kuwa mtu yeyote ambaye Mungu anakusudia kutumia ana hisia ya Takdiri, na Ninaamini kuwa Musa alihisi moyoni kuwa siku moja atakomboa watu wa Mungu kwa hali yote, hakugundua kuwa hauwezi komboa watu kutoka duniani ikiwa bado uko ndani yake. Thomasi a kempis katika kitabu chake "Uigaji wa Kristo" alisema "Hauwezi kumpeleka mtu mbali na ambapo unataka kuenda mwenyewe" kwa hivyo ilimbidi Musa aiache dunia.

Baada ya kutoka Misri, Musa sasa alianza hatua ya pili ya mafunzo yake na ufanikio wa kiroho. Alienda kwenye jangwa kwa miaka arobaini, na kuchunga kondoo, kazi ambayo ni kirihi kwa wamisri. Haikuwa ya kutosha yeye kuacha Misri(dunia); Alikuwa awe na maisha yake ya kindani igandamizwe, kiburi cha misri

nafsini mwake. Tamaduni zake zote na fikira lazima ziharibiwe maishani mwake.

Mwito wa Musa

Wakati Mungu alimuita, Musa alijitetea kuwa hakuwa muumbuji — kigugumizi. Je hii ilikuwa shida ya matamshi tangu kuzaliwa kwake? Biblia haisemi hivyo. Je ilikuwa kupungukiwa kwa imani, au uoga wa Farao? Siamini hivyo. Ninaamini kuwa Musa alikuwa amejikadiri mwenyewe. Alikuwa amefunzwa itifaki za Misri, na alikuwa amehitimu kabisa kufanya kazi hiyo; hata hivyo, alikuwa amelelewa kwenye kasri ya Farao.

Baada ya miaka arobaini jangwani, Musa sasa alikuwa amejikadiri ya ukweli. Hakuwa na ujasiri wa mwenyewe. Hii ilikuwa hali iliyomrundika, kwa sasa angekuwa tu na ujasiri kwa Mungu. Ufafanuzi wa John Wesley wa Unyenyekevu ulikuwa "kuwa na ukadiri wa kweli mwenyewe". Hii inakufanya mnyonge mwenyewe, lakini na nguvu kwa Mungu.

Jangwa ilikuwa imefanikisha njia hii kwa Musa. Kuzungumza na kondoo kwa miaka arobaini ilimuiba ujasiri wake katika mwili, umbuji wote na kiburi ambao ulikuwa wa kawaida kwa tamaduni za Misri. Baada ya hii, ukadiri wa Mungu ilikuwa kwa Musa alikuwa mtu mnyenyekevu duniani. Ninafikiri ni ya miaka arobaini ni ya maana ya kuwa na majaribio ili kupata sifa kuu kutoka kwa Mungu.

Mungu alikuwa sasa tayari kumtumia Musa, kwa sababu Musa alikuwa sasa tayari kutumika na Mungu.

Sasa alikuwa tayari kwa sehemu ya tatu, ambalo ni tokeo la kawaida la mbili za kwanza—kumfuata Yesu (kuziharibu kazi za shetani). Wakati Musa alikuwa duniani (Misri).nguvu zake zilimkomboa mtumwa mmoja na kumuangamiza mmisri mmoja. Sasa, kuwekwa huru na dunia na kusulubishwa kwa mwili wake, alitumwa kurudi duniani (Misri). Hapo alikuwa kutumiwa na Mungu kukomboa taifa lote, na kuangamiza jeshi lote la Misri kwa oparesheni yote. Ya ajabu sana!

Ukombozi

Je Haitakuwa miaka arobaini ya majaribio, ikiwa baadaye tunaweza weka nchi yetu huru kutokana na chuma la ukanda linalishika? Bila shaka. Jamii yetu yakinifu wanayafurahia haya, kwa sababu tumezoea matokeo ya haraka au hata ya mara moja. Tunaishi kwa jamii ambalo maadili ni " pata mazuri(au baraka) sasa, kisha omba baadaye." Hii ni kinyume na njia ya Mungu. Maumbile yote yanahubiri kanuni za Mungu. Kifo huja kabla ya ufufuo. Usiku huja kabla ya mchana, msalaba kabla ya taji. Kwa nini Ukristo wa kisasa unatumia utaratibu na unaangalia matokeo ambayo yako kinyume na kanuni hizi?

Musa ni mfalme bora na pia muombezi. Alibadilisha akili ya Mungu kwa zaidi ya mara nyingi. Soma katika Kutoka 32 jinsi alivyookoa nchi nzima kutokana na ghadhabu ya Mungu kwa uombezi wake. Wakristo wamekuwa katika njia ya kufikiria kuwa

wanapohudhuria washa chache, kutumia siku kwenye sherehe ya uombaji, kumpigia shetani kelele,na kumueleza kuwa ameshindwa, basi hao ni waombezi. Je inawezekanaje hao kudanganyika sana?

Siri ya Musa ilikuwa nini? Je ni rahisi sana. Musa alikuwa mtu ambaye Mungu angemsikia na kuzungumza naye uso kwa uso. Wakristo wanaweza kuwa na bidii ya kutafuta mkono wa Mungu wa kutoa na kwamba hawautafuti uso wake. Lakini Mungu atamsikia mtu ambaye amejiweka huru na dunia na ambaye tabia yake imefinyangwa kwenye tanuu la mateso. Waombaji wote wana hii kwa usawa. Abrahamu alikuwa Rafiki wa Mungu. Danieli alikuwa mtu aliyependwa sasa na Mungu. Kwa kuomba maombi ya Musa au Danieli haitatufanya waombaji. Mungu haisikii maombi yetu pekee; yeye husikia pia mioyo yetu. Ikiwa haiambatani itakuwa afadhali tusiombe kamwe.

Haitoshi kuliinamisha goti
Na maneno ya maombi kusema
Mioyo yao lazima ikubaliane na akili
Ikiwa si hivyo basi hatuombi

SURA YA 9

Danieli

Katika siku zile mimi, Danieli nalikuwa nikiomboleza kwa muda wa majuma matatu kamili. Sikukula chakula kitamu, wala nyama wala divai haikuingia kinywani mwangu, wala sikujipaka mafuta kabisa, hata majuma matatu kamili yalipotimia… Ndipo Gabrieli akaniambia, Usiogope Daniel; kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipoweka moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako, maneneo yako yalisikiwa, nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako… Lakini mkuu wa ufalme wa uajemi alinipinga siku ishirini na moja.

Danieli 10:2-3, 12-13

Danieli ni mfano mwingine bora wa njia hii ya kujifanya mtakatifu kupitia hatua tatu ambazo Yesu alieleza kwa muhtasari.

Danieli alikuwa mmoja wa watu waliochaguliwa na

Mungu, wenye mbegu ya kifalme, na bado alijipata kwenye Babiloni. Misri inawakilisha dunia kabala Mungu hajatuita , lakini Babiloni inawakilisha dunia baada yetu kuitwa.

Hapa tunaona watu wa Mungu kwenye ufungwa. Inaweza onekana geni kwetu kwamba Mungu anafaa kueleza Israeli wasijaribu kupigana na Babiloni, au kutoroka, lakini kukaa hapo na kutumika. (Yeremia 29:4-7)

Maagizo ya Yesu sio tofauti na hii, kwa kuwa hatuelezi kuhusu kutoroka dunia; hivyo, anatueleza tuwe duniani na kujiweka kwenye mamlaka kwa miili ya utawala ,kwa kuwa Mungu ameziweka wakfu. Hata hivyo, alichosema ni kuwa sisi sio wa dunia. Hii inamaanisha dhamani yetu na fikira zetu ni tofauti na siasa, mtindo, tama na amri za dunia.

Babiloni

Jambo la kwanza ambalo Danieli na marafiki wake walifanya walipojipata Babiloni ni kufanya uamuzi kuwa tofauti, na utofauti huu haukuwa tu kwenye mawazo yao na dini, bali kwa hali yao ya maisha, ni rahisi sana ku "amini kuwa unaamini", bila hiyo kuathiri hali yako ya maisha.

Danieli na marafiki zake walichagua kutokula nyama ya mfalme. Nina hakika kuwa nyama ya mfalme ilikuwa nzuri na yenye afya, lakini wangejichafua kwa kula chakula chafu kama nyama ya nguruwe, ambayo ilikatazwa kwenye

sheria za Musa. Walichagua kutokula nyama yoyote, na badala yake kupitisha chakula cha kawaida, kundi, ambayo yalikuwa sawa kwa maisha ya kujikana na kufunga. Danieli aliumba kwa wazi mara tatu kwa siku. Biblia inaonyesha kwa dhahiri kuwa Danieli alitimiza sehemu ya kwanza ya kujikana. Alikuwa duniani, lakini aliamua hatakuwa upande wake.

Habari dhahiri

Kuna habari dhahiri sana ambayo inaweza fikia hitimisho. Siku moja tutaishi kama wafalme na Yesu atakapokuja kutawala dunia hii; lakini hadi ufalme wake uje duniani, tunaagizwa tuishi kama wahaji na wageni. Mhaji hawezi ishi kama mfalme, na mfalme hawezi ishi kama mhaji. Ni jukumu letu kuamua ni maisha gani tunataka kuishi sasa. Nafasi yetu ya baadaye wakati Yesu anaweka ufalme wake duniani inalingana na uamuzi wetu.

Danieli pia alitimiza hatua ya pili (kusulubisha mwili), kwa taarifa ya Biblia kuwa alifunga mara nyingi. Sijui mazoezi bora ya kiroho kuliko kufunga ya kupambana na hali yetu ya kitambo. Ni amri ya Yesu katika mafunzo yake mlimani, na moja ya matendo aliyosema yanafaa kutendwa kwa siri.

Danieli alikuwa pia mtu wa maombi, ambalo ni lingine la matendo haya ya siri ambayo Yesu anatufunza katika Mathayo 6:1-18.

Uombaji wa kweli

Matokeo ya Danieli kupitia hatua hizi mbili yalikuwa gani? Nguvu na Mungu katika uombaji, na ufunuo mkuu. Malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kumpa Danieli funuo nyingi sana, na habari kuwa alikuwa mpendwa wa Mungu. Maombi ya Danieli yalitoa matokeo kuwa watu wa Mungu kurudi kwenye nchi ya ahadi, ufalme wao, kwa hivyo Danieli alikuwa akiharibu kazi za shetani—kutofanya kazi za Nebuchadnezzar, ambaye ni aina ya mpinga Kristo. Haikuwa Danieli aliyekuwa akipigana na shetani au na malaika wake. Kwa kujinyenyekeza mwenyewe kwa maombi na kufunga, alikubali vita vya haki kupigana katika mbingu – kati ya wafalme (Mikali) na mashetani (mkuu wa ufalme wa uajemi). Unyenyekevu wa Danieli ulitupa haki ya kweli kwenye vita kuanza na kushinda. Sio aliyeshinda, lakini katika nguvu za kiroho katika pande zote. Vita huwa ni vya Bwana.

SURA YA 10

Yesu

Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.

Mathayo 5:48

Yaweza kuwa geni kuwa nimechagua kutumia Yesu kama mfano wa njia hii; kwa nini lazima atapitia njia yoyote ya usawa? Kwa kweli alikuwa tayari sawa na bila dhambi?

Kuelewa jawabu, tunafaa kugundua kuwa, kuwa bila dhambi ni tofauti na kuwa sawa. Paulo anaandika katika barua yake kwa Wahebrania 5:8, Yesu, Ingawaje alikuwa mwana, alisoma utiifu kwa mambo aliyoteseka; na kuwekwa sawa, akawa mwanzilishi wa wokovu ya milele. Tunajua kuwa Yesu hakuwa na dhambi, kwa hivyo ni kawaida kuwa usawa huu hauwezi kuwa lolote kama dhambi. Inaweza tuhusu

kukua kwako kwa kiroho na upevu – njia ya kuwekwa sawa.

Kwa hivyo, Yesu anapokueleza kuwa uko sawa, hawezi kuwa akitueleza kuhusu maisha yasiyo ya dhambi, lakini kwa maisha ya utiifu na upevu. Masomo ya maisha ya Yesu yataonyesha kwa uwazi kuwa alipitia mambo yote ambayo anatueleza tupitie, kwa sababu ni njia ya Mungu kwa kila mmoja, hata mwana wake.

Nje ya Misri

Mathayo 2:14-15 inaonyesha kuwa Yesu alipelekwa Misri na wazazi wake, kutimiza utabiri wa nabii Hosea wa Agano la kale, Nje ya Misri nimemuita mwana wangu. Hosea 11:1 inaashiria Israeli, na tunajua kuwa Mungu aliliita taifa lote la Israeli kutoka Misri, lakini Tukikubali kuwa Misri inaonyesha dunia yote, basi hali hii na unabii itatendeka kwa yeyote ambaye Mungu ataita nje ya dunia. Yesu mwenyewe alitoka Misri, na hii ilikuwa ishara, lakini pia aliyaacha hali yote ya dunia alipoanza huduma yake. Hadi wakati alipoanza huduma yake, inaonekana kuwa Hakuna aliyemfikiria Yesu kama chochote ila "mwana wa seremala". Alipoanza kuhubiri na kufanya miujiza, Marko 3:21 inasema kuwa Rafiki wake walisema kuwa alikuwa kando yake mwenyewe: yaani amerukwa na akili. Ni nini kilichowafanya waseme hivi? Haikuwa miujiza, kwa sababu watu waliorukwa na akili hawafanyi miujiza, Ninaamini

ilikuwa hali yake mpya ya maisha ndio ilifanya wafikirie kuwa alikuwa amerukwa na akili, kuyatupa yote na kuiacha dunia.

Hali mpya ya maisha

Mwenyewe ninaona kuwa wakristo watanikubali utofauti wa maoni katika masuala yasiyo asili, lakini ninapo wapa changamoto na hali tofauti ya maisha, hii huleta pingamizi. Huwa changamoto kubwa sana kuliko kanuni, kwa sababu hali ya maisha ni imani katika matendo, au dhibitisho la kupatikana na hatia. Kupatikana na hatia bila matendo haistahili kabisa. Wakati Yesu alipoanza huduma yake aliyaacha yote, na kuishi kabisa kwa imani, na kuhubiri injili. Hakuna mahali imeandikwa kabisa kuwa Yesu aliwahi kutengeneza meza au kiti, au alifanya lolote ili kupata mshahara alipoanza huduma yake.

Soma Luka 12:13-14 kwa mfano wa Yesu kukataa kuhusika katika mjadala wowote halali. Hakuongea hata mara moja kinyume na kazi ya warumi, mbali na ukatili wake na kutotendea watu haki. Habari yake ilikuwa kwamba ufalme wake haukuwa wa dunia hii, na mafunzo yake yote na hali yake ya maisha yanashuhudia ukweli huu. Utakuwa Ushuhuda mgani kama wakristo wa sasa wataishi kama wageni na wahaji katika dunia hii, na wasitegemee mfumo wake.

Yesu katika jangwa

Yesu anapotueleza kuketi chini na kuzingatia gharama, ni kwa sababu pia yeye ilimbidi ahesabu

gharama mwenyewe. Kwa nini ilikuwa Yesu alijaribiwa jangwani? Ni kwa sababu alikuwa na mwili, hali ya kitambo ya Adamu na hiari ya huru, au maombi yake katika Gethsemani yatakuwa hayana maana yoyote; Kwa udhahiri kulikuwa na vita na vita vya hiari mbili. Maswali ya shetani lazima yawe yamevutia kwa mwili wa Yesu, la sivyo haikuwa jaribio. Angali jaribio la mwisho ili kuangalia jinsi inavyokuwa ya kuvutia kwa Yesu. Shetani alitaka kumpa falme zote za dunia hii na sifa zake ikiwa atamuabudu. Shetani Hakusema "Mkane Mungu" Shetani hajali ikiwa tunaabudu miungu miwili. Ni Mungu anayeeleza bayana kuwa ni yeye pekee anayestahili kuabudiwa.

Ufunuo 5:12 inatuonyesha kile Yesu alipewa baada yake kuwa mtiifu na alichopitia msalabani. Ni matandiko ya nguvu za kidunia; vitu vyote ambavyo shetani alikuwa akimpa jangwani. Yesu anastahili kupokea uwezo na utajiri, na hekima na nguvu, na heshima na utukufu na baraka. Vitu hivi viliahidiwa Yesu, `lakini bila ya gharama ya msalaba. Shetani alikuwa akimuahidi lolote ambalo si chini ya mpinga Kristo. Badala ya Yesu kuteseka na kuchukua dhambi za dunia yote juu yake, shetani akimpa alikuwa akimpa kwa njia nyingine.— kuepuka msalaba na kuteseka kwake, na kutawala dunia kama mpinga Kristo, Alimtaka Yesu kulishawishi dunia mzima kumuabudu shetani, kama vile mpinga Kristo atafanya. Ninaweza kumsikia kwa ukaribu akimdhihaki Yesu " Usiwe mjinga Yesu, kwa nini ufe kwa ajili ya watu hawa? Hao hukosa kumtii Mungu hata hivyo. Mbona ufe

kwa ajili yao? Hawafai gharama hiyo! Hata Mungu anapo wakomboa ni kwa muda tu mfupi kabla niwashawishi tena. Historia imedhibitisha. Yesu hawastahili. Kwa kweli utauridhi dunia utakapokufa kwa ajili yao, lakini Mbona uyapitie hayo ikiwa unaweza ipata sasa bila msalaba?"

Toa jasho kama damu

Kwa kweli ilikuwa jaribio kuu na la ukweli kwa Yesu kupewa vitu ambavyo vilikuwa vimesha ahidiwa, mara hiyo na bila uchungu wowote. Ikiwa una shauku lolote kuhusu uzito na mkazo ambalo hizi zilikuwa kwa Yesu, basi soma jinsi alivyoomba katika Luka 22: 41-44. Kabla aende kwenye msalaba, alipomuomba babake jasho lake lilikuwa kama matone ya damu ikitiririka chini, na akasema, Baba, niondolee kikombe hiki. Mapenzi yangu ni kukataa ni kukataa msalaba ; walakini mapenzi yako yatendeke. Hakuliomba ombi hili mara moja tu bali mara tatu. Adui wetu ni mjanja sana kutupa kitu ambacho hakiwezi kutujaribu. Yeye ni mkuu wa mikakati.

Pambano hili kwenye jangwa ni sawa na lile Musa alikumbana nalo. Ni baada tu ya Musa kufikisha miaka arobaini jangwani ndipo Mungu aliposema kuwa alikuwa mtu mnyenyekevu duniani. Yesu alichukua masiku arobaini kuushinda mwili. Yesu na Musa wote walipitia njia hii kabla waanze huduma yao.

Sio ya mwanafunzi

Unawezaje amini? Kwa wakati moja, fikiria kuwa Tulikuwa kwenye jaribio moja? Ni kiburi kuenda kwenye huduma kabla Mungu haja pambana nasi. Ndio maana kuna misiba kati ya Watumishi wa Mungu. Tunawaona watu wakiwa na tamaa ya mali chafu, au bado na tamaa ya mwili wakiyazamisha chini, tayari kufichuliwa na shetani wakati inaweza kufanya maangamizo kwenye ufalme wa Mungu. Uenyewe au Ubinafsi ndicho kizuizi kikubwa kwa maisha ya kimungu na huduma yenye kufaa.

Huduma ya kweli

Baada ya Yesu kupitia hatua hizo mbili, alitimiza hatua ya mwisho njiani – huduma yake ambayo ilikuwa kuharibu kazi ya shetani. Kama tu

Katika mifano yetu mingine, lilikuwa tokeo la kawaida. Yesu alikuwa sasa tayari kufanya hiari ya baba yake, sio huduma yake au hiari yake. Ni baada tu ya Yesu kubatizwa (ambacho kila sheria kifo kwa hali ya kitambo na ya dunia) na kuusulubisha mwili wake, ndipo alipoanza huduma yake.

Yohana 5:19 inasema, Amini amini nawaambieni, mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona baba alitenda; kwa maana yote atendayo yeye, ndiyo atendaye mwana vile vile. Yesu sasa alianza kuziharibu kazi za shetani. Alianza kuharibu njia ambazo shetani alikuwa ametengeneza

duniani. Aliwaponya wagonjwa, aliwalisha masikini, na kuwapa watu changamoto ya kuwa sawa kama baba yake mbinguni alivyo sawa. Yesu hakutenda lolote kwa nguvu zake mwenyewe au kwa utukufu wake.

Ni mfano ulioje kwetu sote, tunapojitahidi kujitenga na dunia, kushindana na miili yetu, na kuwa tisho kwa ufalme wa shetani.

SEHEMU YA TATU

Vifunguu

Na wafuasi wakaja, na wakamwambia, kwa nini wanena nao kwa mifano? Akawajibu na kuwaambia,Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakujaliwa. Kwa maana yeyote mwenye kitu atapewa, naye atazidishiwa tele; lakini yeyote asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa. Kwa sababu hii nasema nao kwa mifano; kwa kuwa wakitazama hawaoni, na wakisikia hawasikii, wala kuelewa. Na neno la nabii Isaya linatimia kwao, likisema, Kusikia mtasikia, wala hamtaelewa, Kutazama mtatazama, wala hamtaona. Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, Na kwa masikio yao hawasikii vema, Na macho yao wameyafumba; Wasije wakaona kwa macho yao,Wakasia kwa masikio yao, Wakaelewa kwa mioyo yao, Wakaokoka, nikawaponya.

Mathayo 13:10-16

SURA YA 11

Nia Ya Mungu

Tumeangalia gharama ya kuwa mfuasi wa Yesu, na kuona kwamba sehemu tano za kwanza ni kujikana, ambayo inamaanisha kuishi na kufikiri tofauti kuliko dunia. Hili ni jambo ambalo tunafaa kutenda wenyewe. Mungu hatusaidii, kwa sababu ni nguvu yetu itafanya hii. Tunaweza ondoa magazeti yasiyo aminika au kurudisha televisheni yetu tukiamua kuwa inazuia mienendo yetu na Mungu.

Kisha malaika Gabrieli hatakuja nyumbani kwangu usiku mmoja na kuichukua televisheni yangu na barua ikifafanua sababu zake. Tunaweza na tunafaa kufanya vitu hivi peke yetu. Haitoshi kuidondoa Biblia na kusema dunia hii si yetu na kuwa sisi ni wageni, isipokuwa tuishi kama wageni.

Sehemu ya pili ya gharama ni kuuchukua msalaba wetu, na kwa hali yetu ya zamani kusulubishwa.

Tumeona kuwa hatuwezi sulubisha mwili wetu kwa nguvu au hiari, kwa sababu mwili ni mawazo ya kisiri na nia ya moyo wetu, na hatujui mioyo yetu. Ni Mungu tu anayejua mioyo yetu, na kwa hivyo ni Mungu tu anayeweza kupambana na miili yetu. Kwa hali yoyote, hii haimaanishi kuwa tukae tu tukimngoja afanye kazi , lazima tuwe tunatenda. Hata hivyo, njia hii sio dhahiri sana kwetu kwa sababu Kristo anafanya kazi halisi, ili tusitukuke kwenye mwili.

Utaratibu wa njia mbili

Kabla tuangalie namna ya utakatifu na sehemu yetu kwake, lazima tuelewe kuwa ni utaratibu wa njia mbili. Mungu pia ana sehemu ya kutenda katika njia ya utakatifu wetu. Ukristo ni kuhusu mabadiliko, sio tu msamaha. Wakati wanawake na wanaume wamesamehewa dhambi zao wanakuwa wenye haki, hiyo ni, sawa mbele za Mungu, lakini sio watakatifu. Hii inamaanisha kuwa sasa hawatalipa tena adhabu ya dhambi zao, kale, sasa, au hata baadaye. Imani katika damu iliyo lipia kosa ya Kristo imewafunika hadi watakapo pokea miili yao isiyo na dhambi katika ufufuo.

Waefeso 1:4 inatuonyesha kuwa kwa maana moja Mungu hatutengi naye mwenyewe: Ametuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu ili tuwe watakatifu. Lakini kuna maandiko kama Waraka wa kwanza wa Petro 1:15-16 Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni

watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu. Hapa Mungu anatusihi tuwe watakatifu, na hatatufanyia sehemu hii. Ni sura hii ya utakatifu ndio nazungumzia; Inamaanisha Kujitenda na dunia. Inamaanisha kuwa kama Kristo kwa tabia yetu ya nje na ya ndani. Hii haitendeki kwa mara moja tu mtu anaposamehewa. Sio kitendo cha neema ya Mungu; ni hali ya maisha ya kujitolea kwetu. Tunaweza samehewa mara moja, lakini hatuwezi kuwa watakatifu mara moja, na hapa ndipo wakristo wengi wanayumbayumba. Wanataka kuwa watakatifu, lakini kwa kuwa hakuna mtu ambaye amefafanua utaratibu wa utakatifu kwao, wanadhania wamekuwa watakatifu, na kujaribu kujifanya kwa hali ya utakatifu kwa nje. Hii sio utakatifu wa kweli, lakini unafiki.

Wakristo wengi wengine hugundua kuwa licha ya kubadilika kwa tabia yao ya nje, bado wana shida na maisha yao ya siri. Wanakubali kuwa bado wana hasira, tamaa, kiburi, uchoyo, au ubinafsi moyoni mwao, ingawaje wanaongoza matendo yao ya kiinje, na kwa hiyo wanajihisi kana kwamba wao ni wakristo duni. Kwa miaka ishirini nilikuwa mkristo duni, nikihisi kuhukumiwa, nikifunika hali yangu ya zamani na maadili ya kiinje.

Kwa udhahiri hakuna hali yoyote kati ya hizi ambayo inatosha, lakini suluhisho ni nini? Haitakuwa tofauti ikiwa tunaweza kuelewa vitu viwili: Nia ya Mungu maishani mwetu, na njia anayotumia kuleta nia hii.

Nia ya Mungu ni nini?

Nia ya Mungu kwa mwanadamu tangu kuanguka kwa Adamu imekuwa kuonyesha tabia yake tangu kuanguka kwa uumbaji wake. ilikuwa sawa hasa katika Agano la kale, kutoka kwa mwito wa Abrahamu, kama ilivyo sasa katika miaka ya sasa—Mungu anakitafuta kikundi kidogo cha watu, wachache ambao wataonyesha wengi tabia yake.

Nina hakika hii itaonekana mzaha na rahisi kwa wakristo wengi, kwa sababu kanisa limechukua akili ya dunia kuwa "kubwa ni rembo", na kuwa "wengi huwa sawa". Kama vile tangazo husema "Je wake wafanyao kazi ya nyumbani wanawezaje kosa?" Kwa bahati mbaya, virahisi sana. Kwa kweli wengi huwa hawako sawa. Yesu alipeana tathmini wazi ya hali kwa dunia hii. Akiongea na wafuasi wake alisema katika Mathayo 7:13-14, Ingieni kwa kupitia mlango ulio nyembamba; maana mlango ni mkubwa na wachache wataingia mlango huu, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huu.

Wainjilisti wakati mwingine hutumia mstari huu pahali ambapo hapafai na wanaitumia kuhubiria wenye dhambi kama neno la injili :mlango mkubwa na njia pana ni dhambi, njia iendayo kuzimu; njia nyembamba ni neema, na njia iendayo mbinguni. Huu ni utafsiri mbaya wa andiko. Mahubiri mlimani ni wa wafuasi, na upinduzi wake ni ukweli: neema ndio mlango kubwa iliyopo; inafunika dunia mzima. Neema ni pana kama kuzimu kwenyewe.

Yesu alichukua dhambi za dunia yote. zilipigwa misumari msalabani . kitu tu ambacho kinazuia mtu yeyote kusamehewa ni kukataa kwa mtu kuukubali ukweli huu. Neema ni mlango mkubwa sio mdogo. Mlango mdogo na njia nyembamba ambayo Yesu alizungumzia ni njia nyembamba ya ufuasi.

Tume ya israeli

Katika Kumbukumbu la torati 14:2 Mungu alizungumza kupitia Musa na akaambia Israeli, Kwa kuwa u taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako, na Bwana amekuchagua kuwa watu wake hasa, kuliko mataifa yote yaliyo juu ya uso wa nchi. Hili sio andiko la upweke; Mungu alikuwa tayari amewaambia mara nyingi yakwamba ilikuwa watengwe na tofauti. Mambo ya walawi 20:24-26 inasoma, Lakini mimi nimewaambia ninyi, Mtairithi nchi yao, nami nitawapa ninyi kuimiliki, nchi iliyojaa maziwa na asali; mimi ni Bwana, Mungu wenu, niliyewatenga ninyi na mataifa mengine…Nanyi mtakuwa watakatifu kwangu mimi; kwa kuwa mimi Bwana ni mtakatifu, nami nimewatenga ninyi na mataifa ili kwamba muwe wangu.

"Takatifu" inamaanisha kutenga au tofauti. Aje, kwa njia gani, ilikuwa wawe tofauti, au watengwe? Lazima ilikuwa kwamba walikuwa tofauti kwa wengi. Neno lingine ambalo limetumiwa kwenye mstari huu ni "pekee": watu wa kipekee kwake, na ingawaje neno limebadilisha maana yake kwa kiingereza katika

karne, imebakisha kidokezo chake cha kuwa tofauti, dhahiri au iliyotengwa. Ikiwa mtu ni tofauti na, au kilichotengwa na, wengi, wanakuwa " wa pekee". Wakati wengi wanakuwa " wa pekee" basi mlinganyo inabadilika, na wale waliokuwa wa kipekee wanakuwa wa kawaida. Wale waliokuwa wa kawaida sasa wanakuwa wachache. Na hao ndio sasa wale ambao wanaitwa tofauti au wa pekee. Kwa hivyo wa pekee ndio huwa wachache.

Sehemu ya mwisho ya mstari inasema Juu ya mataifa yote yaliyo duniani. Israeli walikuwa wawe tofauti na mataifa mengine yote. Nia ya Mungu kwa watu wake haikuwa kulitiisha dunia. Ni kweli kuwa alimueleza Abramu kutenda haya kabla atende dhambi, lakini tangu dhambi iingie duniani Mungu hajawahi tena kutupa sheria hii. Mungu alitaka mabaki atakaye onyesha na kutangaza tabia yake kama shahidi duniani kote, kwa sababu dunia ilikuwa sasa chini ya hukumu ya Mungu. Mungu hatawahi fanya hukumu yake bila kuwepo na ushahidi wa utakatifu wake—chumvi duniani—ili adhabu hii iwe yenye haki, na ionekanayo kuwa yenye haki, na malaika, shetani, na wanadamu wote.

Kizuio cha israeli

Mungu alimuambia Musa katika Kumbukumbu la torati 11:24 kila pahali mtakapokanyaga kwa nyayo za miguu yenu patakuwa penu; tokea hilo jangwa, na Lebanoni, na tokea mto wa Frati, mpaka

bahari ya magharibi. Hili ni eneo ndogo kuliko Uingereza. Israeli haikuwa na amri yoyote kutoka kwa Mungu kulishinda nchi lingine kama hili. Walikuwa wanaonyesha tabia ya Mungu duniani kote; walikuwa wawe watu wa kipekee, taifa la makuhani, takatifu mbele za Mungu.

Historia ya Biblia inaonyesha kuwa walishindwa kuyafanya haya, na kila wakati walishikwa na tamaduni na miungu ya mataifa yaliyowazunguka. Hawange jitenga wenyewe na kuwa watakatifu. Hata Levi, kabila ambalo Mungu alitenga mwenyewe kutoka Israeli, kabila ambalo ilikuwa liwe hasa la "pekee" na takatifu lilishindwa kabisa. Kuhani hasa, aliyetoka kwenye kabila hii, mara tu walipowekwa wakfu, walitoa moto geni kwa Bwana.

Tume ya kanisa

Ninapata hasa maagizo sawa katika Agano jipya kwa kanisa la leo, ingawaje yanakaa kupingana mafunzo ya kisasa ya watu. Petro katika barua ya kwanza anasema maneno sawa kwa kanisa kwamba Musa aliambia Israeli: Bali ninyi ni uzao teule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa miliki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu. Kanuni sawa za utakatifu na utengano yanafaa kutumika kanisani, na hii ni sawa na mafunzo ya Yesu na watume.

Yesu alikuwa nuru, lakini dunia haikuelewa au

kustahimili nuru, na wakamsulubisha. Kwa maneno mengine, nuru ilizimwa. Aliwaambia wafuasi kwamba ilikuwa wawe nuru, lakini kuwa watarajie upingamizi sawa kama alio kumbana nayo. Katika Yohana 15:20 Yesu anawaambia wafuasi wake kwa uwazi kuwa wasitarajie kujulikana bali kukataliwa. Mtumwa si mkuu kuliko Bwana wake. Ikiwa walinitesa, nanyi pa watawatesa; ikiwa wameyaweka maneno yangu, yenu pia watayaweka.

"Tume kuu" iliyopewa katika injili haituelezi tuichukue dunia kwa Yesu. Haiiulizi kanisa kuishinda dunia, au pia kuiweka Kikristo. Wala haituelezi kuwa popote miguu yetu itakanyaga itakuwa yetu. Hakuwa hata andiko moja linalotueleza kudai miji yetu kwa Kristo; Hasa, tunaambiwa kukung'uta vumbi miguuni mwetu tunapotoka kwenye mji ambao umekataa neno letu. Ikiwa Mungu anaheshimu mapenzi ya mwanadamu, nasi pia tutafaa kuheshimu. Ikiwa watu wanachagua kulikataa injili, hiyo ni haki yao. Tume yetu ni kwa urahisi kulipa dunia lote nafasi ya kukubali au kukataa injili.

Hakuna sababu

Injili ya Marko, ambayo inakaa kuwa dondoo linalojulikana sana la tume ya mwisho, inasema katika sura ya16: 15, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Kanisa halina sababu lisipomwambia kila kiumbe kinaloishi mapenzi ya Mungu na neema yake; lakini sisi sio

wanasiasa, na kwa hivyo hatufai kutumia ukumbi, wito, au mbinu kama hizo kushurutisha au kuchezea watu kwa njia yoyote. Kwa sababu hiari ya mtu lazima iheshimiwe. Mstari wa 16 inasema, Aaminiye ataokoka na asiyeamini atahukumiwa. Kauli rahisi; Mungu ataongezea kanisa watakaookoka. Watu wasipoipokea ujumbe wetu, Mathayo 10:14 inatuambia tukung'ute vumbi miguuni mwetu na kuenda kwingine. Matokeo Haifai kuwa shughuli yetu. Shughuli yetu ni kumueleza kila mtu habari njema.

Mahubiri ya moto wa kuzimu

Wakristo wengi wanafikiria kuwa "habari njema" ni kuwaambia watu kuwa wanaenda kuzimu wasipotubu. Ingawaje mazoea hii ni ya kawaida kwa wainjilisti, hakuna andiko la kuiunga mkono.

Yesu alizungumza tu kuhusu kuzimu kwa wafuasi wake au kwa wale waliodai kuwa katika nuru, wafarisayo. Sipati popote ambapo Yesu aliongea kuhusu kuzimu kwa mtendadhambi. Nyaraka hazitutii moyo kuhubiri kuhusu kuzimu pia. Mungu anataka mapenzi yetu kwa hiari yetu wenyewe. kuamua kumtumikia Mungu kwa sababu tunataka kutoroka kuzimu sio nia mzuri, na sio msingi mwema kwa uhusiano. Ninaamini kwenye ziwa la moto, na Ninaamini kuwa wote walio waasi wataenda huko na shetani na malaika wake; lakini nazungumza hapa kuhusu injili. Injili ni habari njema, sio habari mbaya. Ninaamini kuwa Mungu ni Mungu mwema,

na anafaa kutumikiwa hata kama hakungekuwa na tuzo na adhabu.

Imesemwa mara nyingi kuwa hakuna sababu nyingine ya kuwepo kwa kanisa duniani kama sio kufundisha injili na kuishinda ulimwengu kwa Kristo. Kwa kuangalia tu hii inakaa tathmini nzuri, kwa sababu tumelelewa kwa kanuni hizo, lakini hakuna kitu kwa mafunzo ya Yesu kuunga mkono kauli hiyo. Yesu hakutaja hata mara moja kuwa kutakuwa ufufuo mkubwa duniani, au kuwa kanisa litatawala dunia kabla ya kurudi kwake. Kwa kweli alisema kinyume na hayo alipoulizwa na wafuasi wake kuhusu nyakati za mwisho. Akiwakanya wafuasi katika Mathayo 24:4 alisema, Angalieni mtu asiwadanganye, na akaendelea kuzungumza kuhusu uongo na mateso kabla ya kurudi kwake. Mafunzo ya mitume sio tofauti na hii. Paulo katika Wathesalonike wa pili 2:3 pia inasema, Mtu yeyote asiwadanganye kwa njia yoyote, sawa na vile Yesu alivyosema. Kisha anawashawishi katika mstari wa 15 kusimama imara wakati uongo mkuu na mateso yanakuja.

Tuna kanuni nyingi na utaratibu wa uinjilisti. Lakini uinjilisti wa kweli ni rahisi, matokeo ya kawaida ya utakatifu. hutendeka wenyewe na kwa kujiendesha. Maisha matakatifu yana nguvu zake kuangaza giza. Wakati wakristo wanaifanya uinjilisti kuwa sababu, na sio matokeo kama inavyo paswa kuwa, basi kwa kweli inakuwa kinyume na maisha ya kweli ya mkristo.

Nia ya kweli ya kanisa

Hatimaye wacha nikupeleke katika mistari michache katika Waefeso 4; hapa Paulo anatuonyesha kwa uwazi nia ya Mungu maishani mwetu. Mstari wa11 inaonyesha orodha ya ofisi tano za huduma ambazo zinaonyesha yote yanayotakikana kanisani. Haya ni mitume, manabii, wainjilisti, Wachungaji na Walimu. Je ni maono gani ya kijumla ambayo hawa watu muhimu wanapaswa kuwa nayo wanapohudumu? Mistari michache ifuatayo inaonyesha, kwa sababu inatueleza sababu gani Mungu alipeana ofisi hizi, na matokeo yanavyopaswa kuwa: Kwa kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe.

Matokeo ya haya ni: umoja wa imani; kumfahamu mwana wa Mungu; mtu kamilifu; kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; sio watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu. Hakuna kitu chochote hapa kuhusu uinjilisti. Huduma hizi tano ni kwa pamoja kutoa kitu kilichopevuka na safi—bibiarusi msafi. Hakuna chochote katika nyaraka zote kinachotushawishi ku "shinda nafsi". Maagizo yote ni kuhusu hali ya maisha ya mkristo na utakatifu.

Kuzaliwa kwa kawaida

Lazima nisisitize kuwa ninaiunga mkono uinjilisti (hiyo ni, kueleza habari njema kwa kila kiumbe);

lakini kuzaliwa kwa watoto, kwa kawaida au kiroho, ndio Mwanzo sio mwisho. Mwisho ni kuwaleta katika upekavu. Hiki ndicho kiini cha mafunzo ya Agano jipya – kuleta wakristo kwenye usawa wa Kristo.

Sheria za kawaida na za kiroho zote zinafuata kanuni sawa. Watu wawili wanapo pendana, watoto ndio matokeo ya kawaida ya mapenzi hayo. Wachumba wanaopendana Hawafai kuambiwa kuwa wanafaa kulala pamoja na kuwa wanafaa kupata watoto; wala hawahitaji mawaidha ya njia nzuri ya kutimiza matokeo haya! Kumakinikia njia na mbinu haitawahi kutufundisha upendo na huruma. Kwa nini kanisa inakaa kuihitaji mawaidha mengi katika njia za uinjilisti? Inaweza kuwa tu kwamba hatuna kitu kimoja ambalo ni la maana—uhusiano, upendo wa Kristo na huruma. Tukiwa na haya, watoto wa kiroho watakuwa matokeo ya kawaida na hatutahitaji mafunzo yoyote, njia, au semina. Hatutahitaji motisha yoyote au ushawishi. Itakuwa jambo la kawaida zaidi duniani. Kwa kweli tutataka kulitenda

SURA YA 12

Njia ya Mungu

Choma takataka inayo eusisha moyo wangu
Choma kila kitu kinacho tutenganisha
Choma hali yangu ya zamani, nipe Mwanzo mpya
Choma moto wa Mungu hadi niweke kwa Bwana wangu Kristo.

Joanna Barratt

Ikiwa nia ya Mungu ni kwetu sisi kuwa bibiarusi msafi na aliyekomaa wa Yesu, basi ni njia gani ambayo Mungu Anatupitisha ili kupata tokeo hili?

Mzabibu

Katika Yohana 15, Yesu kwa uwazi anatuonyesha njia ambayo ni msingi na lazima ieleweke na kila mkristo ikiwa watabadilishwa kuwa sura ya Mungu.

Wale ambao hawaelewi njia ya Mungu kila wakati wanajipata wakimlaumu shetani kwa matokeo ambayo Mungu ameleta. Wanaweza kujipata wakipigana na Mungu, wakiamini kuwa wanapigana na Shetani, ambalo ni kosa lizito la kufanya. Mtazamo wetu kwa njia hii itaamua kile ambacho Mungu anaweza au hawezi tenda maishani mwetu.

Katika mstari wa kwanza Yesu anasema, mimi ndimi mzabibu, na Baba yangu ndiye mkulima. Hii ni rahisi kuelewa; lakini mstari wa pili unatueleza njia ambayo Mungu, mkulima, anatupitisha: kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa.

Pointi mbili zinatokea kutoka kwa kauli hii. Kwanza, Yesu lazima anazungumza kuhusu wakristo, kwa kuwa ni wakristo tu walio "kwenye mzabibu". Pipi, inatuonyesha kuwa wakristo wanaweza kuwa hawazai matunda, na matokeo katika mstari wa sita ni hatari: tawi lisilozaa linatupwa, huoza, na huchomwa. Wakristo Hawafai kujipata katika hali hii. sehemu nusu ya pili ya sura ya pili inasema kwamba kila tawi linalozaa tunda Mungu hulipogoa ili lizidi kuzaa. Tukiangalia sana haya maneno ya Yesu tunaona kwamba matendo yote ya mikono ya Mungu ni uchungu. Ama tulitupwa nje na kuchomwa, au tunapogolewa – na kurudishwa kwenye kisiki. Je haikai geni kwamba tunapomfurahisha Mungu, mkulima, na kuzaa matunda, tunatendewa kwa uchungu? Ukweli haufai kuwa geni kwetu, kwa kuwa kanuni ni ndicho msingi katika uumbaji wa Mungu.

Mkulima yeyote anaelewa kuwa ili kutoa matunda mema upogoaji lazima ufanywe, na matokeo yanaonyesha ukweli wa tendo hili.

Kupogoa kwa uchungu

Njia ya kupogoa ni kwa kweli ya uchungu, na kuna maneno mengi ya kibiblia ya kuifafanua, kama vile, majaribu, kusafisha, au moto. Kuna sababu tu yake moja katika akili ya Mungu—kwamba tunafaa kuzaa matunda zaidi. Kwa lugha rahisi hii inamaanisha kwamba wakristo wote wanafaa kukua zaidi kama baba yao kwa tabia. mara nyingi kanisa hujaribu kulifanya mti liwe kubwa, wakati nia ya na kunaweza kuwa mti mdogo na matunda mengi. Lakini Tukitaka kuwa kwenye mapenzi ya Mungu, lazima tuwe na lengo na nia sawa kama Mungu.

Katika anga hii ya sasa ambayo kukiri kwa hakika na afya takatifu ni za fadhila, wazo kwamba Mungu mwenyewe angekubali sisi tuteseke, au kuwa pia anaweza sababu la hali yetu mbaya, haijulikani. Lakini nataka sasa maandiko machache ya mengi ya mada kuthibitisha pointi. Maandiko haya hayatuonyeshi tu kwamba tunafaa kutayarisha vitu hivi, lakini pia yanatueleza ni nini fikra zetu zinafaa kuwa kwao yanapotendeka.

Hesabuni yote kuwa furaha

Katika Yohana 15:11 Yesu anaeleza sababu ya kupogoa mizabibu. Ni kwamba ili furaha yake

iwe ndani yetu (hii ni, hatuipotezi kwa njia hii) na ili furaha yetu itimizwe. Huwa tunaambiwa tuangalie zaidi ya majaribu kwa faida kuu ambayo kwa kweli itafuata ikiwa tutashinda majaribu.

Yakobo anaanza barua yake kwa waamini hivi: Ndugu zangu, hesabuni yote kuwa ni furaha tupu mnapopitia majaribu mengi. Njia ya kigeni sana kuanza barua ya kutia moyo! Lakini hatufai kuachia hapo, kwa sababu Yakobo anaendelea kupeana maelezo mantiki ya maneno yake. mstari ufuatao unaanza, kwa kujua hii.. kujua njia hufukuza uoga. Huu ndio ufunguo wa maagizo ya Yakobo. uoga wa asiyejulikana ni mojawapo ya uoga wa mwanadamu. Adui wetu shetani amepooza na ameshindwa ikiwa tunaweza elewa ukweli huu, kwa sababu inamnyanganya mojawapo ya silaha kuu zake: uoga.

Je ni maarifa magani ambayo Yakobo anataka kutupa? Kujaribiwa kwa imani yetu inatoa uvumlivu.mtu ambaye ni mvumilivu yuko kamili na hodari. Wakristo wengi wanatamani uvumilivu, lakini hawatawahi pata. Kwa sababu wakati Mungu anaanza njia itakayoleta imani kwao, wanakasirika na kufikiria kuwa ni shetani anayewashambulia. Wanamlaumu shetani, na wanamuomba Mungu ukombozi. Wanajiombea wenyewe kutoka kwenye majaribu yatakayo leta uvumilivu kwa na kuwaweka kamili na sawa, wasiokosa lolote.

Ruka na cheza

Katika injili ya Luka sura ya 6:22-23, Yesu aliwaambia wafuasi wake waruke na wacheze kwa furaha. Kilicho cha ajabu ni kwamba Yesu hakuwaambia waruke na Kucheza walipokuwa na furaha au walipojazwa na Roho mtakatifu, aliwaambia kinyume. Ilikuwa waruke na Kucheza kwa furaha wakati watu watakapowachukia, na kuwatenga . hii haitakuwa ya maana kwa mkristo ambaye anaamini kuwa anafaa kutarajia baraka tu kwa Mungu, na hali mbaya kwa shetani peke yake. itakuwa ngumu kuelewa ikiwa wameelezwa kuwa "shetani hatawahi kukusumbua tena ukiwa na imani ya kutosha". Tunaweza tu elewa haya maneno ya Yesu tunapoangalia mbele kwa matokeo na athari. Yesu alisema kuwa tutakuwa kama manabii wa kitambo, watu watakatifu: na tuzo yetu itakuwa kubwa mbinguni.

Tutazidi kuwa na mashida ikiwa macho yetu yako tu kwenye baraka tulizo nazo kwenye dunia hii. Yesu aliwaagiza wafuasi wake kuweka hazina yao mbinguni, na sio duniani. Na Paulo katika Wakolosai 3 anasema, Mkiwa mmefufuliwa na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.

Kutenda kwa mema yetu

Warumi8:28 ni mstari unaojulikana na ambao umetumika sana, na ndani yake tunaona kanuni

sawa kabisa. Paulo anasema mambo yote hufanyika kwa kutupa mema. Hasemi kuwa mambo yote ni mema. Mateso siyo mema. Magonjwa, uchungu, majaribu, na kutoelewana siyo mema. Paulo anasema kuwa tunafaa kuangalia zaidi ya hali kwa faida ya baadaye, na anatukumbusha kuwa pia mambo mabaya yanatendeka kwa nia mema maishani mwetu: kwamba tutafanywa sawa na mfano wa mwana wake. Hili ndilo tunda linalodumu—tabia ya milele ya Mungu. Paulo anamalizia sura hii na faraja kuwa si kifo wala maisha, wala malaika, wala ufalme, wala mamlaka, wala mambo ya sasa, wala mambo zijazo, wala urefu, wala kina, wala kiumbe kingine, wala taabu, wala wasiwasi, wala mateso, wala ukame, wala utupu, wala hatari kubwa, wala upanga, itaweza kututenga na upendo wa Mungu. Paulo anadai kuwa hii ndiyo inayotufanya kuwa zaidi ya washindi—siyo kwamba tunatoroka majaribu na utakaso, lakini kwamba ni ya kufaa badala ya yenye kuleta busara. Tunaweza kuwa na fikra ya ushindi katika majaribu yetu, kwa sababu tunaona manufaa ya baadaye.

Ahadi isiyo ya kawaida

Paulo, katika barua yake ya lipi kwa Timotheo, sura ya 3:10-11, anasema jambo kuhusu hali yake ya maisha ambayo inapatana na sura ya njia za Mungu maishani mwetu. Ushindi wa Paulo siyo kwamba alilindwa kwa majaribu na mateso, lakini kwamba alivumilia hadi mwisho. Anazungumzia sta-

hamilivu, sadaka, subira, mateso, na huzuni. Haya, sasa, ndio alama ya mfuasi wa kweli. Yesu alisema, Jihadhari, wakati watu wote wanazungumza mema juu yako; hiyo ni dalili ya mfuasi wa uongo. Paulo anamkumbusha Timotheo ukweli fulani. Tunaweza iita ahadi: wote waishio katika Kristo watateswa.

Ni rahisi kuona kuwa kwanini hii iwe vile. Je utakatifu wa kweli unawezaje kukubalika kwenye kizazi kiovu na chenye kuzini, dunia yenye giza? Mwangaza pengine ungewaka na kushinda giza, au ungezimwa, kwa sababu dunia inaichukia na haiwezi kuielewa.

Mabadiliko ya fikra za Petro

Petro, alipokumbwa na mateso katika majaribu ya Yesu, alimkana kuwa hamjui. Kwa hii alithibitisha kwamba hakuamini kuwa msalaba ulikuwa wa maana, na kuwa hakuwa amejitayarisha kwa shida yoyote. Hasha, Petro na mitume wengine walikuwa wakiangalia Yesu aubadilishe ufalme uwe Israeli wakati huo, na Petro hata alikimbilia vurugu wakati wa kumshika Yesu katika bustani ya Gethsemane.

Katika barua yake ya kwanza, Petro anatuonyesha kuwa fikra zake kwa mateso na majaribu yalibadilika sana. Hangekuja hata kwenye kinyume ya sura hii. Wacha nidondoe maneno yake katika Waraka wa Petro wa kwanza4:12. Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule jaribu ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni

kiwapatacho. Petro anatueleza tutarajie jaribu la ajabu kama jambo la kawaida; na mstari unaofuata, kama ilivyo na mifano yetu, anaangalia baadaye kama sababu ya kuteseka katika majaribu hayo: lakini furahini, kwamba ninyi ni washirika wa mateso ya Yesu; kwamba wakati utukufu wake utathihirika, utaweza furahi pia na furaha ya ajabu.

Lazima tuhitimishe kuwa fikra mpya ya Petro ilikuwa yenye kukomaa. Mabadiliko yalikuwa sana na ya kawaida ya kupuuza. Maisha ya mkristo na njia si tofauti na mkristo wa sasa. Petro alimkana Yesu kwa sababu hakuutaka msalaba. Kuna hiari mbili pekee—ama tujikane wenyewe au tumkane Kristo. Hii inaonekana kuwa kauli kali sana; lakini sote tunasonga kwa mojawapo ya mielekeo hizi mbili, na hatimaye tutafika kwa mojawapo ya hitimisho.

Baraka ya kigeni

Yesu anaanza barua yake kwa kutueleza kuhesabu majaribu yetu kwa furaha, lakini Petro anamaliza barua yake ya kwanza katika sura ya 5:10 na shawishi hiyo hiyo—baraka ambayo sijasikia kwa kanisa yoyote. Lakini Mungu wa neema yote, ambaye ametuita kwa utukufu wake wa milele kwa Yesu Kristo, baada ya hayo umeteseka kwa muda, kukuweka sawa, weka, tia nguvu, kukutuliza. Njia hii(kuteseka kwa muda) ndio ambayo tunafaa sasa kutarajia kama wakristo, na matokeo tunayofaa kutarajia kwa majaribu yetu ni sawa kabisa na yale tumeona kwa maandiko

mengine. Orodha ya ajabu hii iliyo: sawa, kutulizwa, isiohamishika, na kutiwa nguvu! Inafaa kututia moyo kuruka kwenye moto na kusema, "Mungu, ichome takataka iliyo maishani mwangu"! Ni mara ngapi wakristo hujiweka kwenye madhabahu ya sadaka, wakiamini kuwa wameyaacha yote, lakini huruka Mungu anapowasha moto chini yao!

Kujiweka kwenye madhabahu ya Mungu inaweza hata kuwa haki ya uenyewe uonyeshaji wa mwili, tendo ambalo linafurahisha hali yetu ya zamani, isipokuwa tu tunajihisi kukaa juu yake na Kuvumilia moto. Kuomba wenyewe kutoka kwa majaribu inadhihirisha tu kuwa hatutaki kuachilia chochote kilicho na gharama au kilicho uchungu kwetu.

Kumfuata Paulo

Katika Wafilipo3:17 Paulo anatusihi tuwe wafuasi wake. Tunafaa kusoma muktadha wa maneno yake ili tuelewe maana yake: mstrari wa saba unasema, lakini mambo yote yaliyokuwa faida kwangu, naliyahesabu kuwa hasira kwa ajili ya Kristo. Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama takataka ili nipate Kristo; tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itakayo kwa Mungu, kwa imani.

Ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake. Ili nipate kwa njia yoyote kuifikia kiama ya wafu.

Kuna maandiko mengi yanayokubaliana na machache ambayo nimedondoa hapa. Tumeona kuwa njia ya kusafisha na kupogoa ndio ya kawaida na ya pekee, njia ya kuleta tunda lenye afya na nzuri.

Kuendea dhahabu

Dhahabu ni chuma ya thamani sana na ya kupendeza macho. Tabenakulo na hekalu, mahali ambapo Mungu alikaa na watu wake, yalikuwa yamejaa dhahabu. Dhahabu inaashiria utukufu wa Mungu, tabia yake ya asili, na kwa hivyo inafaa iwe safi. Dhahabu sio safi kwa kawaida ; inahitaji kupitia njia ya kusafishwa. inawekwa kwenye kalibu na kuwekwa ndani ya tanuu. Dhahabu inayeyuka, na uchafu (takataka) huelea juu na kuondolewa. Njia hii hurudiwa hadi uchafu uishe kwenye dhahabu, kisha inawachwa iwe baridi na ngumu ili itumike.

Hii ndio njia sawa ambayo Mungu anataka kutupitisha ikiwa tunataka kusafishwa. Hakuna njia nyingine. Udhaifu wa tabia yetu haiwezi shughulikiwa hadi yakuwe juu.

Kuwekwa wazi

Mungu hawezi na hatatoa tu kwa miujiza ondoa vitu ambavyo vimefichwa moyoni mwetu. Aidha,

Mungu hatashughulika na vitu kutokuwa sawa kwa tabia yetu hadi tukubali kwamba tuna vitu visivyo sawa ndani yetu. Hadi shinikizo na joto itujie, uchafu wetu unaweza baki umejificha hata kwetu. Tunapowekwa wazi, ni uchungu na aibu, kwa sababu wakati udhaifu wetu unaelea unakuwa dhahiri sio tu kwetu, bali pia kwa wenyewe!

Mara nyingi tunaona hii kuwa ngumu na tunalaumu hali ya tabia zetu; lakini hali, mbali na kuwa sababu ya "nje ya tabia" mienendo, inatufunulia tu tabia yetu ya kweli, mtu wa kweli ndani. Hakuna kitu kinachoweza kutoka nje ya mtu ambacho kisichokuwa ndani yake. Shinikizo na joto ya majaribu na taabu yanatumika ku leta uchafu juu; na hili ni jambo mzuri. Ikiwa tutanyenyekezwa basi kwa kweli hii ni mzuri, kwa kuwa Unyenyekevu ndicho fikra ambacho anataka. Ninashawishika kuwa Mungu hatawahi shughulika na lolote maishani mwetu ambacho hatutaki kukubali kiko.

Kwa bahati mbaya, kuna uchaguzi badilli kwa njia ya usafishaji. Tunaweza kupangusa juu ya dhahabu hadi ing'are, na kwa kweli itarudisha mwangaza. Lakini tunapotumia jambo maishani mwetu, uchafu unabaki umejificha ndani mwetu na kwa wale wanaotuangalia. Ni Mungu tu ajuae ukweli ulio mioyoni mwetu. Nitaanguka katika jukumu langu kama mtumishi wa neno ikiwa sitasema kuwa " kusafisha juu" ni jambo la upuuzi kutenda. Inaweza kuwa inatosha katika maisha hii, lakini Biblia inatukataza kuwa kila kazi ya mwanadamu mwishowe itajaribiwa kwa moto na tote

yatadhihirishwa. Ningependekeza kuwa ni afadhali kunyenyekea katika maisha hii, na kuwa wa maana kwa Mungu, kuliko kungojea hukumu ya watakatifu na kupoteza yote.

Kujaribiwa na moto

Paulo katika Wakorintho wa pili 5:10,anasema, Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirisha mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya; na katika Wakorintho wa kwanza3:12, Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo, dhahabu, fedha au mawe ya thamani, au miti au majani au manyasi, kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri: Maana siku ile itaidhihirisha, kwa kuwa yatafunuliwa katika moto; na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani. Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikikaa, atapata thawabu. Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila yeye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto. (ikiwa tuna shauku lolote, Paulo anazungumza kwa uwazi kuhusu wakristo, kwa sababu anasema kuwa wataokolewa. Hangesemaa haya kwa watu ambao hawamjui Mungu.)

Sikiza kile ambacho Roho anasema kwa makanisa, sanasana kwa wale wanaojihisi kuwa matajiri na kujawa na mali, wale ambao hawahitaji chochote cha kimwili au kiroho. Kwa kweli, makanisa mengi katika jamii ya kimwili wana fikra hiyo. Ufunuo 3:18

inasema, Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri; na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona. Na aliye na masikio, na asikie.

SURA YA 13

Tabia ya Mungu

Tunapaswa kufanya nini ili kuwa wakomafu na watakatifu? Je funguo ni gani? Kwa nini wakristo wengine wanaendelea kubadilika na kukua, wakati wengine wanatuama na kuruka? Je utakatifu ni jambo la kupata na kukosa, au je kuna maagizo wazi yaliyowekwa katika neno la Mungu?

Ninaenda kuangalia fumbo hili la utakatifu, njia ya kina ya iendayo chini na isiopimika ambayo mtu hubadilika kwenye kina chao na msingi wa matendo. Kwanza, Niruhusu niseme mengine ya kanuni yaliyo nyuma ya maagizo ya Yesu. Ni rahisi sana kuwa watiifu tunapokuwa na kuelewa. Hakuna faida kwa kuwa na imani kipofu, ikiwa yote tunayahitaji ni kuona kwa kawaida.

Sarafu ya pande mbili

Ikiwa tunaenda kutafuta tabia ya Mungu, basi ni ya maana tujiulize kwanza ikiwa tunajua kwa kweli na tunaelewa jinsi tabia yake ilivyo. Ili kutusaidia kulijibu hili swali, wacha niwape andiko hili ambalo linaweza kutumika katika masomo yetu yote.

Nimepata kwamba wakristo wachache wanajua ukweli huu: Ukweli hauwezi kuja kutoka kwa kauli moja. Fikra zetu za magharibi ziko kwa msingi wa mantiki ya utaratibu, maji sio baridi, kuna uchaguzi badilli mbili, moto au baridi, na yote mbili hayawezi kuwa kweli yote. Moja ndio ukweli, na nyingine lazima kwa hivyo iwe uongo.

Lakini je maji yakiwa vuguvugu? Huo ni mchanganyiko , au yote moto na baridi. Na ni nani anayeamua ni nini moto hata hivyo? Yote yanawiana digrii 70 ni moto ikilinganishwa na digrii 40, lakini vuguvugu ikilinganishwa na digrii 100! Mwishowe Tunapata kwamba "ukweli" wetu wa magharibi yamewekwa msingi na maonyesho ya kiholela ya sayansi, lugha au mantiki. Tunasema hii ni buluu, kwa hiyo si ya kijana; huu ni mti , kwa hiyo si kichaka; lakini yote ni uwezo na ufafanuzi wa mwanadamu, na tunafanya kosa sana kwa kutumia njia sawa na hizo kumjua Mungu.

Tunajaribu kumjua Mungu kwa sayansi na mantiki badala ya kwa uhusiano; tunafasili na kuiwezesha ishara na tabia zake: Yeye yuko hivi, kwa hivyo hayuko vile. Uhusiano huwa haihitaji kujua "ukweli"; uhusiano unahitaji tu uzoefu wa kumjua mtu.

Fikra za kimagharibi

Shida ya mawazo yetu ya kimagharibi ni kwamba Biblia haikuandikwa na fikra za kimagharibi. Wala haikuandikwa kwa fikra wa kimashariki au mashariki ya kati. Biblia inatueleza kwa wazi kwamba iliandikwa jinsi vile wanadamu walivyoagizwa na Roho mtakatifu. Kwa hivyo Biblia ni mawazo ya Mungu. Msukumo ulitoka kwa Roho mtakatifu. Hatufai kujiruhusu kusahau ukweli huu, ama sivyo hatutatafuta ufunuo kwa Roho mtakatifu. Ni rahisi sana kutumia wakati wetu kuchambua Giriki au Kiebraniana kuwa wasomi bandia, na kuibiwa chakula cha kiroho. Biblia haihitaji Uelewekaji au utoaji wa hoja; inahitaji ufunuo. Ndiyo, kuna wasomi wanaoishi maisha yao yote wakisoma mswada wa kale, siwakosoi. Ninasema kuwa tunahitaji mtu aliye andika Biblia kutufunulia Biblia.

Kupinga kwa wazi

Lazima sasa niende zaidi, na niseme kwamba sio tu kwamba ukweli wakati mwingine una pande mbili, huwa ina kupingwa kwa wazi. Ninasema "wazi" kwa sababu kinyume ni pande mbili tu ya ukweli sawa na yanaweza kaa pamoja kabisa. Pengine kielelezo rahisi itasaidia uelewaji wetu wa dai hili.

Kama ningekuinulia Sarafu ili kichwa kiwe kinakuangalia, ni ya kawaida kuwa hautaona mkia. Mimi kwa upande ulio elekea, ningeona mkia na sio

kichwa. Kama ningeuliza kilichokuwa kwenye Sarafu sote tungesema upande tuliyoona na sote tungekuwa sawa, hata kama hatukuelewana. Kuelewa ukweli, ninyi wala mimi hatutabadilisha au kugeuza Sarafu (mfano wetu wa ukweli); tutabadilisha tu nafasi yetu.

Naweza kukaribia kusikia watu wakisema hili ni ombi la masikilizano. Je ninapendekeza kuwa hakuna ukweli kamili, na kwamba kila kitu kinahusiana? je ninamwaga ukweli? hata hivyo, ninaweka ombi la masikilizano. Maelezo yangu yanatuambia kwamba kamili huwa, na kwamba ukweli hauwezi, na hautawahi, badilika. Lakini lazima niweze kuona pande zote ikiwa nataka kuelewa ukweli wote.

Je Mungu anasema nini?

Wacha Mungu aseme mwenyewe. Kila wakati Mungu akisema tabia yake, alitumia kauli mbili ambazo zinakaa kupingana. Katika amri kumi , Kutoka 20:5 inasema: Bwana Mungu wako ni mwenye wivu, anawapatiza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao…

Kauli ya kwanza inaonyesha kwamba Mungu ni hakimu wa kuogopa; lakini kauli inaendelea katika mstari wa6,…Nami nawarehemu Maelfu ya wanipendao, na kuzishika amri zangu. Hapa ni baba anayesamehe na mwenye huruma. Je ni kauli gani inayotueleza tabia ya ukweli ya Mungu? Je Mungu wetu ni mwenye wivu, mwenye kuogofya na mlipizaji

kisasi, au je yeye ni mzuri, mwenye kusamehe, mwenye huruma?

Utukufu wa Mungu

Wakati Musa alimueleza Mungu kujidhihirisha na kumwonyesha utukufu wake, Mungu alimficha Musa kwenye ufa wa mwamba na kusema tabia yake. je Mungu alisema nini kujihusu yeye mwenyewe? Alisema sawa kama katika amri kumi—alisema pande mbili za tabia yake. Kutoka 34:6-7—Bwana Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; Mwenye kuwaonea huruma watu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi…wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe… mwenye kuwapitiliza watoto uovu wa baba zao, na wana na wana wao pia, na kizazi cha tatu na cha nne.

Je ni tabia gani kweli ya Mungu? Yetu ya utaratibu itatuambia kuwa ni moja au nyingine; haiwezi kuwa yote. Lakini ukweli wa tabia ya Mungu ni kauli zote mbili.

Timazi

Wacha nikukumbushe kanuni yetu: Ukweli hauwezi kuja kutoka kwa kauli moja. Hatari huja wakati pande moja pekee ya tabia ya Mungu inahubiriwa na nyingine inatokewa. Ni ukweli wote

tu wote unaotuweka huru. Kabla shahidi aruhusiwe kutoa ushahidi kwenye korti la sheria, wanaelezwa kukula kiapo kifuatacho: “Mimi, ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kusema ukweli, ukweli wote, na ukweli pekee. Kwa nini sheria haisemi tu “ukweli” ? kwa sababu sheria pia inaelewa kuwa kauli moja, au pande moja ya ukweli, haitoshi; inahitaji ukweli wote; zaidi ya kauli moja tu, ili kupata ukadiriaji wa kweli wa jambo.

Mhubiri wa injili lazima ahubiri kuwa Mungu ni mwema na mwenye kusamehe, na kwamba anataka kutubariki. Lazima pia wahubiri kwamba yeye ni hakimu wa kuogofya, na kwamba tutawajibika kwa kila neno lisilofaa tulilonena: kwamba kuteseka, kama vile baraka, ni sehemu kamili katika maisha ya Mkristo. Tusipofanya haya italeta injili iliyopotoshwa na kukashifu tabia ya kweli ya Mungu. Kanuni ni thabiti kwenye Biblia yote, na Uelewekaji wetu kwake itafanya tofauti yote kwa kufahamu kwetu kwa neno la Mungu.

SURA YA 14

Namna Mbili

Katika barua ya kwanza ya Yohana kwa kanisa, sura ya 1:8 inasoma, Tukisema kuwa hatuna dhambi, tunajidanganya wenyewe, wala ukweli haumo ndani mwetu. Paulo anawaambia wakristo waumini. Anawaambia wale ambao wametubu na wamepokea msamaha kutoka kwa Mungu. Itakuwa ya ajabu ikiwa upatanisho wa Yesu ingetuweka bila dhambi lakini kama vile kila muumini wa kweli anajua, si hivyo. Tumesamehewa, na tu wasafi (pamoja na Mungu), na hatuwajibiki tena kwa dhambi zetu, kwa sababu upatanisho wa Yesu ni dhabihu ya milele. Hata dhambi tutakazotenda baadaye yamelipiwa yote; lakini hatuko na hatutawahi kuwa bila dhambi tukibaki kwenye miili yetu iliyo kufa.

Wakristo bado wanatenda dhambi

Dhambi ni chochote chini ya ukamilifu—hiyo ni, chochote chini ya mapenzi kamilifu ya Mungu. Mawazo yenye tamaa, hasira bila sababu, kutia chumvi kwa ukweli ambayo yanakuwa uongo; Hatuwezi ishi hata siku moja bila kutenda dhambi. Paulo anatuhakikishia kuwa hakuna tena shutumu kutoka kwa Mungu, au nguvu zozote za lawama kutoka kwa shetani. Kwa sababu tumeshalipiwa gharama, na tuna huru ya kumtumikia Mungu.

Kama tunavyojua kwamba barua hii imeandikiwa waumini inafanya mstari wa 9 kupendeza sana. Yohana anasema, Tukiziungama dhambi zetu, Mungu ni mwaminifu na wa haki kutuondolea dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. Wacha tudhanie kwamba Yohana alikuwa anawaambia wasio amini. Angeandika tofauti, na kusema, "Mungu ni mwaminifu na wa neema", je uaminifu na haki vinaambatana aje na msamaha? Jawabu ni: hakuna kabisa! Wakristo tayari wameshapokea huruma na neema, na msamaha wao ni kamili, kwa hivyo, Yohana anajaribu kutueleza nini kwa kutumia maneno haya? Anasema kwamba tukiwa waaminifu na kukubali kwamba bado tunatenda dhambi, basi Mungu ni mwaminifu na wa haki kutimiza ahadi yake. Mungu ataendelea kutusamehe, na hatufai kuwa na shida tena na lawama.

Ushahidi zaidi

Si tu andiko moja katika Yohana ambacho kinanidhibitishia hii; maandiko mengine mengi, kwa mfano katika barua ya Paulo kwa Wagalatia na Warumi, inatuambia jambo sawa na hilo. lakini sifai kuihitaji Paulo kunionyesha hali hii. wala sihitaji maandiko mengine kunidhibitishia ukweli kwamba bado ninatenda dhambi. Sifai kuangalia mbali na moyo wangu na maisha yangu ya kila siku. hata kama nina njaa na kiu ya kuwa mwenye haki, na hata kama najua kuwa nimekomaa kwa miaka, ninaweza sema sawa kama Paulo alipokiri kwa kanisa katika Warumi8:19, kwa mema ninayotaka kutenda, siyatendi; lakini mabaya ambayo sitaki kutenda, najipata nikitenda. Bado nina mapigano ya kindani, baada ya miaka mingi, lakini niko huru kabisa kwa lawama yoyote kwa sababu Mungu ni mwaminifu na wa haki kwa neno lake, na mwana wake Yesu ananiombea kila wakati kwa mkono wa kulia wa Baba.

Wakristo hawawezi kutenda dhambi

Katika barua hiyo hiyo ya Yohana, mistari tu thelathini na tano baada ya kauli yetu ya kwanza kuwa wakristo hawawezi kuishi bila kutenda dhambi, sura ya 3:6 inasema, Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi: kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua; na katika mstari wa 9, Kila mtu

aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; kwa sababu uzao wake unakaa ndani yake: wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu.

Yohana ametuambia kwa wazi katika sura ya kwanza kwamba wakristo bado wanatenda dhambi, na bado sasa tuna kauli wazi kwamba mkristo hatendi dhambi ,na la ajabu kwamba hawezi kutenda dhambi.

Kukaribia kwa kukatiza

Mara nyingine, tunaona kauli nililotaja katika sura iliyopitia yakitumika na Paulo: huwa kuna zaidi ya pande moja kwa ukweli. Ukweli huwa na kinyume na kutoelewana. Tusipotambua kanuni hii, tunafaa kuhitimisha kwamba moja ya kauli za Yohana ni ukweli na nyingine ni uongo. Haya ni matokeo ya kile wakristo wengi hutenda.

Kwa hali yote, hawawezi kiri papo hapo, kwa sababu wanatangaza kuamini kwamba Biblia ni neno lililotiwa msukumo na Mungu, na kwa hivyo hakuwezi kuwa na uongo wowote na upinzani ndani yake. Kwa hivyo wanalazimika kukaribia kwa kukatiza: wanachukua upande wa ukweli ambao wanaona ni rahisi kuelewana nayo, kisha wanatetea kuwepo kwa maandiko yanayoweka upande ulioelekeana kwa kusema, “ Najua kuwa Yohana alisema hivyo, lakini kile alichomaanisha ni …” na wanajaribu na kutosheleza kauli lisilo stadi kwenye moja ya mafundisho yao yaliyodhibitishwa ili kujitetea. Badala yake, wanaweza sema kuwa “

hatufai kuchukua barua iliyokufa ya neno, lakini kuelewa roho ya kile ambacho mwandishi alikuwa anajaribu kutueleza"; na kwa njia hiyo kujipa ruhusa kufanya maandiko yaseme yale wanayotaka kusema, kwa hivyo hawakosei mafundisho yao.

Sisemi kwamba hii ni ya kuwa mhakiki au kukejeli kwa njia yoyote, lakini kwa sababu ninatambua ugumu ambao watu wanapitia wanapoamini kuwa ukweli unaweza kuwa kwenye kauli moja. Ninajaribu tu kudhibitisha mashida yanayotokana na imani.

Hakuna upatanisho

Je tunawezaje patanisha kauli mbili zilizoelekeana katika Biblia? Hatuwezi, na kwa kweli hatufai. Kauli mbili yote yanayopingana yatasimama kamili kwa peke yao bila sababu yoyote ya "upatanisho". Kuna jawabu ikiwa tutaangalia Sarafu kwa yote na siyo "kupingana" kwa pande hizo mbili.

Jawabu ya kauli mbili za Yohana ni rahisi, mara tu tunapokubali kuwa yote ni kauli ya ukweli kwa wenyewe. jawabu ni kwamba kila kauli inataja hali tofauti au tabia. Mkristo ni mtu ambaye ana tabia mbili tofauti. Kauli za Yohana zinatosha kwa ukamilifu, kwa sababu moja ya tabia hizi haiwezi kutenda dhambi, na nyingine haiwezi acha kutenda dhambi. Wacha tuangalie tabia hizi mbili kwa undani ili tusiwe na shauku kwa ukweli huu wa Biblia.

Hali ya zamani, au tabia, pia inaitwa hali ya Adamu, kwa sababu ilianza na dhambi ya Adamu. Kila

mkristo anajua kuwa Adamu aliumbwa bila dhambi, lakini wengi hawatambui kuwa aliumbwa pia bila dhamiri.

Mti wa dhamiri

Hii ni kawaida tunapozingatia kwamba mti ambao Mungu alikataza Adamu kukula ulikuwa unaitwa Mti wa kujua mema na mabaya. "Kujua mema na mabaya" ni fasili kamili ya neno "dhamiri"; maneno haya mawili ni yenye kubadilishana. Adamu hakuwa na dhamiri, hii inamaanisha hakuwa na uchaguzi wa maadili. Maadili yanaweza tu kuja kwa kutokana na kujua ni nini chema na ni nini kibaya. Mungu hakutaka Adamu kujua mabaya au mema, kwa sababu alimkataza kuufikia ule mti, njia ya kuupata ujumbe huu. Chaguo la Adamu lilikuwa tu moja la kutii au kutotii, na siyo lolote la kufanya kama fasili ya ni nini chema na kibaya.

Kutii

Mara nyingi haieleweki kuwa kutii na kutotii hayana lolote na dhamiri, maadili, mema na mabaya. au sawa na ovu. Adamu aliambiwa awe mtiifu. lakini hakuwa mtiifu kwa sababu alijua ilikuwa "sawa" au "adilifu" au "mema" kuwa mtiifu, au kwa sababu dhamira yake ilimwambia afanye hivyo. Vivyo, alipokosa kutii, hakuwa anafanya kitu ambacho alijua ni kibaya na ovu. Adamu hakuwa na maadili

"mfumo wa thamani" ya kila kilichokuwa chema na kilichokuwa kiovu. yote aliyokuwa nayo ilikuwa maagizo ya Mungu. "Tii usiasi";hakuna sababu kwa nini, hakuna maadili kabisa. Kutii ni jambo ambalo limetengana na maadili na dhamiri.

Ninajitahidi kusisitiza pointi hii kwa sababu Ukristo wa kweli haiambatani na maadili au dhamiri . huo ni mti mbaya—mti wa kujua mema na mabaya. Ukristo ni kupata mti wa uzima, kutii, na kujitolea kwa mapenzi ya Mungu. Kutii kulimwezesha Adamu kuufikia mti wa uzima; lakini alipokula kutoka kwa mti wa kujua mema na mabaya alizuiliwa kuufikia mti wa uzima. Dhamira, kujua mema na mabaya, ni ya kuharibu Ukristo . Inaingia katika kutii kwa urahisi, kwa sababu wakati mtu anapojua mema na mabaya, hakuna hakikisho kwamba ufafanuzi wao wa mema na mabaya yatakubaliana na kile Mungu anaangalia kuwa mema na mabaya. Warumi 5:18-19 inasema kwamba kwa sababu ya kutotii kwa mtu mmoja , watu wote walihukumiwa adhabu. Hii inamaanisha kuwa tulizaliwa wenye dhambi. Haisemi kuwa tulizaliwa kamili kisha tunaanza kutenda dhambi baadaye tukielewa. Ni tabia hiyo tu tunayozaliwa nayo, na ni urithi wetu kutoka kwa baba wetu wa mwili, Adamu.

Kuzaa

Mafunzo wazi kwenye Biblia yote ni kwamba kila kitu ambacho Mungu aliumba huzaa aina yake. Mti wa

tufaha huzaa tufaha, mbwa huzaa mbwa, na watenda dhambi wawili wakizaa mtoto, hawawezi kuzaa chini ya au zaidi ya wao wenyewe—mtoto mtenda dhambi! ninatumai kuwa hii siyo ya kupendeza kwa sura zetu wenyewe; Hata hivyo, tunafaa kugundua kuwa ilikuwa dhambi ya Adamu, siyo yetu, iliyosababisha hali hii. Tunarithi dhambi kwa kuzaliwa tu.(lazima niseme kuwa tunatenda dhambi pia kwa kujitakia wenyewe, lakini hili ni jambo lingine.)

Dhambi ni ya kiasili

Kila mzazi atathibitisha kuwa mtoto hahitaji masomo ili ajue jinsi ya kuwa na tamaa, mchoyo, au mkaidi. Haya yote yanakuja kwa asili! tunachohitaji kuwafunza watoto wetu ni kwamba wanafaa kuwa wasio wachoyo na watiifu. Inahitaji kutia adabu ili kutekeleza mabadiliko ya lazima. Hii inakuwa mtindo wa chini na chini katika jamii yetu ya kibinadamu, na tunavuna matokeo ya kizazi cha wazazi waliofikiria kuwa watoto wao wata "pata kiwango chao" cha tabia bila hitaji lolote la mwongozo na nidhamu. Kwenye agizo letu la kwanza na nidhamu kama mtoto, tunajifunza kuongoza hali hii ya Adamu kwa kutengeneza sheria, na adhabu ya kuvunja sheria hizo.

Tamaa

Ningependa kutumia tamaa kama mfano. Tamaa ni kutaka kitu ambacho si chetu. Ni asili kuwa na tamaa.

Watu wengi wangeiba ikiwa hakungekuwa na sheria, adhabu, na hakungekuwa na aibu iliyoambatanishwa na kosa. Ingekuwa jaribio kubwa sana.

Tamaa ni kawaida kwa mwanadamu, na hakuna aliye huru kwake. Jamii inatusaidia kuikatiza tabia hii kwa hulka yetu kwa kutengeneza sheria na adhabu. Mara nyingi ni uoga wa kupatikana ndio humzuia mtu kuiba, au uzinzi, au kutimiza tamaa nyingine ya mwili.

Ikiwa kile ambacho nimeandika kinakaa chenye kuhumu na kigumu kwa asili ya mwanadamu, basi lazima niwapeleke kwa andiko na kwa orodha ambayo Paulo anapeana ya "kazi za mwili" (ambazo ni sawa na hali ya zamani). Wagalatia5:19-21 inasema, Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi. Kukubali kuwa bado tuna asili ya zamani ni kukubali kuwa tuna uwezo wa kila kitu katika orodha ya Paulo.

Mioyoni mwetu

Kazi ziko mioyoni mwetu na tabia, lakini udhihirisho uko katika matendo yetu ya nje. Mtu anaweza kutawala matendo yao, lakini inamshughulisha Mungu kidogo ikiwa kitendo bado kiko moyoni mwao. Kwa sababu ni moyo ndio ambao Mungu huhukumu. Kwa bahati mbaya, wakristo wengi bado wanajaribu kutawala asili

hii ya zamani kwa mapenzi yao. Hili si jawabu. Hiari yenye nguvu haiwezi kubadilisha tabia yetu; Inaweza tu kandamiza vitu ambavyo tuna aibika kudhihirisha kinje. Enyewe haiwezi badilisha enyewe

Tunaweza kufaulu kutawala matendo yetu ya nje, kama vile inavyowezekana, na kudhania kuwa mioyo yetu ni safi na kuwa sisi ni watakatifu kwa tabia. Lakini hii haitatatua shida, kwa sababu enyewe bado atakuwa moyoni, na hiyo bado haijatawalwa.

Biblia inatupa tu jawabu moja ya kupambana na maisha enyewe: lazima ife, kwa kuwa haiwezi kutawaliwa au kusafishwa.

Ikiwa tutasahau kuhusu ya ndani na kujihukumu kwa matendo ya nje, hii ni unafiki, ambalo ndilo dhambi la Wafarisayo.

Nyingine zaidi ni watu ambao ni waaminifu kwao wenyewe, na kugundua kuwa maisha yao ya siri iko mbali sana na utakatifu. Kwa kawaida, hii huwafanya wajihisi kujishutumu. Kwa miaka ishiri nilianguka kwenye hili kundi la pili. Ingawaje nilikuwa mzuri sana wa kuwadanganya watu wengine, sikupenda kujidanganya, na kwa hiyo nilijihisi mkristo wa tabaka la pili. Sikuwahi kuwa huru na hatia. Ningeomba na kumsihi Mungu anipe hiari yenye nguvu ili niweze kushinda tamaa zangu na niwe na nguvu juu ya kiburi change, uchoyo, na tamaa; lakini sikuwahi kupokea nguvu ya kushika hizi tamaa za siri.

Asili mpya

Baada ya miaka ishirini ya kungangana ilinijia kwamba Mungu hatengenezi asili ya kale; anatupa mpya. Nimekuwa nikijua kwamba Biblia inazungumzia kuzaliwa upya, lakini sikuwa na ufunuo wake wa binafsi.

Kama, nilipozaliwa kwa mwili, niliiridhi tabia ya Adamu, ni kawaida kwamba nilipozaliwa tena kwa roho, niliirithi tabia ya Kristo. asili tofauti hii iliyo! Paulo anatueleza kuihusu katika Wagalatia 5:22na anaiita "tunda la roho": tunda la roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili uaminifu, upole Juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. Tabia hii iko ndani ya kila mtu aliyezaliwa kwa Mungu. Haiwezekani kwetu kutoirithi tabia hii ikiwa Mungu ni baba yetu.

Miti miwili

Sasa tunafaa kuelewa jawabu la kauli hizi zinazopingana ambazo Yohana alisema. Asili ya zamani ya Adamu haiwezi kukombolewa . imeanguka na itazidi kuanguka. Kama vile Yesu anasema katika Mathayo7:18, Mti mwovu hauwezi kuzaa matunda mazuri. Asili ya Adamu ni mti mmbaya na itazidi kutenda dhambi. Hii kwa kweli ndio habari mbaya, lakini habari njema ndio hii: Mungu, kupitia Yesu anatupa asili yake mwenyewe. Sasa huu ni mti tofauti. Siyo mti wa kujua mema na mabaya, lakini mti wa

uzima, na ni sawa na haiwezi kutenda dhambi. Yesu pia alisema katika mstari huo kwamba Mti mzuri hauwezi kuzaa matunda mabaya.

Suluhisho rahisi

Paulo anasema katika Warumi 8 mstari wa 2 Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. Hizi ni sheria zinazoongoza asili zetu mbili. Jawabu rahisi sana na za huru—na bado kwa maono yangu ninajihisi kwa kweli kwamba wengi wa wakristo wanatumia nyingi ya nguvu zao wakijaribu kutawala asili ya Adamu, wakiamini kuwa inaweza kutengenezwa au kutawalwa, badala ya kusahau juu yake na Kumakinika kwa kulisha asili yetu yao mpya.

Tembea katika Roho

Mafunzo ya Paulo katika Wagalatia 5:16 ni kwamba Basi nasema Tukitembea kwa (Roho asili yetu mpya), wala hatutazitimiza kamwe tamaa za mwili (asili yetu ya zamani). Weka maanani kwamba hasemi kwamba kwa wakristo tamaa ya mwili hupoteza tu. Anasema hatutazitimiza. Je hii inamaanisha nini? Mstari ufuatao unatuonyesha kwamba kuna vita ya kila siku: Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka.

Mtu akikubali ukweli kwamba asili yoyote

tutembeayo ndani yake itadhihirika mwishowe katika maisha yetu ya nje. Kisha inafuata kwamba tunaweza tembea tu kwa asili ambayo tunapalilia na kula. Hii ndiyo siri ya maisha ya utakatifu ya bila mawazo—kupambana na mizizi. Lazima tuinyime chakula asili ya kitambo na kuilisha asili yetu mpya. Tabia yetu itakuwa tokeo la kawaida la hii bila hitaji lolote la kupambana au kutumia nguvu ya kutaka.

Fikiria baba akiwafunza watoto wake kuhusu kukua kwa kuwaagiza kujaribu na kunyosha na kuwa makini na kutia kila bidii. Hatungefikiria baba yeyote angekuwa mjinga. Yote anayotakiwa kufanya ni kumlisha mwanawe kila siku, na kukua kutakuja peke yake. Kwa bahati mbaya, wakristo wengi wanang'ang'ana kukua kiroho, waking'ang'ana kuwa watakatifu na kukomaa, wakati yote wanayohitaji ni chakula cha kiroho cha kila siku abacho ndicho kitu wanachopuuzia! Hii ni ya huzuni kabisa; lakini hawapuuzii tu kulisha asili mpya, wanaendelea pia kulisha asili ya zamani.

Katika miaka yote wanasoma kanuni zaidi; wanasema fomyula mpya, na njia za nguvu na za kutimiza mahitaji yao—lakini hawakui kitabia kama baba yao aliye mbinguni.

Kulisha asili ya zamani

Vitu ambavyo vinalisha asili yetu ya zamani vinaweza kukaa vya kawaida kwa wakristo—kusoma ponografia, kwa mfano. Hata hivyo, tunaweza kuzoea

maisha yetu ya kila siku, hata tusijue jinsi tunavyolisha bila kujua asili ya zamani kila siku. Wacha nichukue kitu ambacho hakitendi dhambi chenyewe, kama gazeti. Kuna kwa kawaida nafasi kubwa kutoka kwa ushafu hadi kusoma kuzuri, lakini nyingi ya habari za kila siku zinatangaza maovu, uhakika, uvumi, au uongo mtupu tu. Mara nyingi kwa kweli huwa na msingi wa siasa, na karatasi moja pekee haiwezi kumpa msomi ukweli. Kwa njia yoyote, kwa nini mkristo angetaka kusoma siku kwa siku kuhusu mauaji, ubakaji, mizozo ya siasa, utendaji mabaya kwa ujasiri, wakati Biblia inatueleza katika Wafilipo 4:8 kuyafikiria mambo haya : mambo ambayo ni ya kweli, staha, haki, safi, yenye kupendeza, na yote yenye sifa njema? Sifa hizi huwa hazipatikani kwenye magazeti!

Athari ya vyombo vya habari

Kwenye matelevisheni mifululizo ya drama ya mivutano ya kijamii yamewekwa kwenye misingi ya tamaa isiyoridhika ya watu ya masengenyo na kashfa. Televisheni ndio mashine kubwa ya propaganda ambayo dunia hii haijawahi kujua. Hubadilisha mawazo ya bara yote, nani ni stadi sana, kwa sababu infanya kazi kwa marudio na kwa miaka nyingi. Kwa sababu ya wingi wa vyombo vya habari, mabara mzima sasa yanaona matangazo sawa na maonyesho sawa, na mwimo sawa na tunapoteza Kumbukumbu yetu ya kilicho sahihi katika macho ya Mungu.

Jamii kwa jumla zimewekwa kwenye programu

kwa wakati sawa, na kwa bahati mbaya jambo sawa linatendeka kanisani, huku makanuni ya kigeni yakifunzwa sawia kwa wakristo duniani kote wakitumia vyombo vya habari vya kisasa. Dunia imeingia kwa pande nyingi za kanisa ya sasa, kwa sababu wahubiri na waumini wamekuwa wakilisha asili yao ya zamani. Wameamini kwamba uenyewe unaweza kupatana na akili ya Kristo , na polepole injili imepotoshwa na kuwa yenye maana, badala ya makosa na upanga.

Nimepeana vyombo vya habari kama mojawapo ya mifano, lakini tukitathmini wakati tunayotumia tukitenda mambo ya kidunia (Ninasema tena siyo mambo ya dhambi na wakati tunapotumia kuilisha asili mpya, siyo ya ajabu kuwa mwimo adilifu ya wakristo imedidimia kwa uwiano sawa na ya dunia. Ikiwa kanisa itadumisha mwimo wake kwa miaka mia moja iliyopitia, pengo kati ya dunia na kanisa itakuwa kubwa sana kwamba italeta dhihaka na mateso—matokeo yale yale ambayo Yesu alisema msalaba utapata kwenye jamii.

Wacha kujaribu

Ninataka kum Zeal_of_Enoch@msn.com alizia sura hii kwa kusisitiza shida ambayo wakristo wengi wanayo wanapokumbwa na changamoto na mahitaji ya utakatifu. Wanataka kukubali kwamba bado wana mawazo ya tamaa na mawazo ya ashiki ya maisha, au kwamba ni wachoyo, au wanaona ugumu wa

kusamehe maadui zao. Shida, kama wanavyoiona, ni kwamba hawana hiari ya nguvu. Ikiwa tu wangekuwa na nguvu ya kutaka, wanafikiria kwamba wataweza kushinda makosa haya ya siri.

Ninaamini kuwa shetani amefurahi sana na utambuzi huu—kwa kweli Ninaamini aliwapendekezea kwa mara ya kwanza. Atawatia moyo wakristo na mawazo kama: " jaribu zaidi, Mungu atakusaidia", au, amwambie Mungu akupe hiari yenye nguvu". Siamini kwamba shetani ana huzuni unapomwomba Mungu, ikiwa unaitisha jambo ambalo Mungu hawezi kukupa. Shetani anajua kuwa kung'ang'ana kwako kuwa mtakatifu itakufanya tu kuwa na kiburi, na kushutumu wengine, au ukianguka, kukushutumu. Kwa njia yote, anafurahi kwa sababu ameuficha njia ya ukweli kwa utakatifu.

Ninaenda kugawa katika sura ijayo ninachoamini na nimepitia maishani mwangu, na kuona mengine yasiyohesabika: ukweli rahisi kwamba haihitaji hiari ya nguvu kwa utakatifu. Sisemi kwamba kulima hiari ya nguvu ni jambo mbaya . Ni vizuri kuwa na nidhamu. Ninachosema ni kwamba hiari yetu siyo mzizi wa shida, na tamaa ya Mungu ni kwamba tupambane na mizizi. Njia nyingine itashindana na kuzalisha kwa maisha ya kweli ambayo Mungu ametupangia.

SURA YA 15

Yote Kwa Akili

Basi nasema neno hili, tena nashuhudia katika Bwana tangu sasa msienende kama mataifa waendavyo, katika ubatili wa nia zao; ambao akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu uliomo ndani yao; ambao wakiisha kufa ganzi wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanya kila namna ya uchafu kwa kutamani. Bali ninyi, sivyo mlivyojifunza Kristo; ikiwa mlimsikia mkafundishwa katika yeye, kama kweli ilivyo katika Yesu: mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu.

Waefeso 4:17-23

Ikiwa mkristo hahitaji hiari ya nguvu kubadilisha

tamaa zake na nia, au kuzuia malengo na tamaa, basi anahitaji nini? Jambo moja ni hakika: tabia yetu ya kawaida haitajibadilisha yenyewe. Uenyewe unahitaji kifo kwa kusulubiwa ili asili ya Yesu kutawala miili yetu, ili tukaweze kudhihirisha tunda la roho, na siyo matendo ya mwili. Ninaamini kwamba siri haiko kwenye hiari yetu bali kwenye akili yetu. Mabadiliko ya matendo hutokana na mabadiliko ya fikra.

Ni nani anayehitaji hiari ya nguvu?

Warumi 7 mstari wa 15-21inaonyesha vita ambavyo sote tunavyo na asili zetu mbili. katika mstari wa 19 Paulo anasema, kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi ;bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo. Kama hiari ya nguvu ingemfanya mtu mtakatifu katika maisha yao ya siri, ningeridhishwa kuwa Paulo angeifanikisha, na hangehitaji kuikiri. ikiwa mtu yeyote angejiadhibu mwenyewe kwa hiari yake ilikuwa Paulo mfarisayo, aliyekuwa amesoma kulingana na barua kali ya sheria. Lakini lazima akiri kwamba hangeweza kuitenda.

Paulo kisha anasema katika mstari wa 22 na 23 kwamba katika asili yake mpya anapenda sheria za Mungu, lakini kuna sheria nyingine kwenye matendo katika asili yake ya zamani inayopigana na sheria ya akili yake. Mstari wa 25 inamalizia: kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi .

Inaanza akiliini

Siyo rahisi kukubali kwamba utakatifu huanza kwenye akili, lakini ni siri ya utakatifu wa kweli---na kinga dhidi ya haki ya mwenyewe, kwa sababu tukifaulu kuzuia matendo yetu ya nje kwa utashi, tuko kwa hatari ya kuwa watakatifu- wenyewe na kuridhika wenyewe; enyewe inatukuka.

Watu wengi wanakubali kwamba tuna fahamu na akili iliyo fichika. kuna mstari katika Waebrania4:12 ambo utatusaidia kueleza wazi tofauti hii. Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

Nafsi na roho

Kuna migawanyiko mitatu ambayo neno la Mungu hufanya, ambayo wakristo wanaona ugumu kuyaelewa. Ya kwanza ni mgawanyiko kati ya nafsi na roho. Ni mijadala mingapi imekuwa kali sana kwa miaka mingi kati ya ni nini ya nafsi na ni nini ya roho! Hata baada ya karne ya uchunguzi wa kanuni, migawanyiko haiko wazi kabisa kwa muumini wastani.

Viungo na mafuta

Mgawanyiko wa pili ni kati ya viungo na mafuta.

Mganyawanyiko wa kigeni gani huu! Tunapotoka kufika kwenye mwisho wa jambo huwa tunasema "wacha twende kwenye mifupa ya maneno", na tunamaanisha kwamba tutafichua yote yanayofunika ukweli. Lakini neno la Mungu linaweza kuenda zaidi ya hii, kwa sababu tukitoa kila kitu hadi kwenye kiunzi cha mifupa, bado kuna vitu ambavyo hatuwezi kuyaona. Mafuta yako ndani ya mfupi wenyewe. Mifano miwili ya kwanza yanatuonyesha kanuni lakini ni mfano wa tatu unaotuhusu hapa.

Mawazo na makusudi

Neno la Mungu linaweza kuamua kati ya mawazo na makusudi ya roho. Hii inamaanisha kwamba kuna tofauti kati ya tunayofikiria kwa ufahamu na nia yetu na makusudi yetu ni gani, katika akili yetu iliyofichika. Hii ni tofauti kubwa sana, na moja ambayo lazima tuelewe ikiwa tunataka kukua katika utakatifu.

Akili au moyo

Ni ya maana tuelewe tofauti kati ya akili na moyo. Ninatambua kuwa kuna maoni mengi kwenye mada huu. Mara nyingi tofauti ya maoni ni kwa kweli tu ya masharti na ufafanuzi, na jinsi tunavyoeleza vitu kwa msingi wa maarifa ya usuli wetu. Kila mtu huwa anakuja kwa pembe tofauti. Ni sharti kwa hivyo ili kwanza ukaelewe ufafanuzi wangu, ili ukaweze kufuata hoja langu.

Ninaamini kuwa akili ni maumbile, na kwa urahisi hiyo ndiyo kompyuta ya kibiolojia ya mwili. Hii inamaanisha kwamba haiwezi kufikiria yenyewe. Lazima iprogramiwe. Kufikiri na kuprogramu , basi inatoka kwa roho yetu, sehemu yetu isiyokuwa ya maumbile. Hapa ndipo nia zetu, malengo, tamaa, na mihemuko hutoka.

Fahamu au akili iliyofichika

Ninataka sasa kutofautisha kati ya wazo la fahamu na akili iliyofichika, na Ninaamini ni rahisi kutenda hivi kutoka kwa Biblia.(Ninafaa kuweka wazi ukweli wa kawaida kwamba mwili na roho zimeunganika, na kwa hivyo huwa zinafanya kazi kama moja, kwa hivyo ingawaje utofautishaji wangu ni rahisi kusaidia kuelewa kwetu, ninagundua kwamba ufafanuzi zaidi unahitajika kuchunguza dhamira hii).

Wakati Biblia inazungumza kuhusu "akili" Ninaamini huwa inaashiria kujitambua, mawazo ya fahamu. Kwa mfano, Paulo katika Wafilipi anatutia moyo kuyafikiria mambo haya: mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza. Kwa kawaida tuna fahamu ya vitu tunavyofikiria tunapotii maagizo ya Paulo.

Moyo

Wakati wowote Biblia inapozungumza kuhusu

"moyo", inaashiria katikati yetu, mizizi yetu, mawazo ya akili yetu iliyofichika. Hapa ndipo tamaa yetu iliyofichika na nia yetu ya siri zipo, na hii pia ndio sehemu ya uongo yetu—sehemu ambayo mume wetu, mke, mwajiri, au mhubiri hajui. Imefichika kwetu pia.

Sote tunajua kile tunafikiria, lakini hatuwezi kuwa na uhakika kwa nini tunakifikiria. Ikiwa wa wakati wowote unahisi kuwa nia zako ni safi na kwamba unajijua, basi tafakari maneno ya Yeremia 17:9—Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua? Moyo huwa mdanganyifu kwamba itatudanganya kwa kufikiria kuwa ni safi! Daudi alimuuliza Mungu kuujaribu moyo wake (siyo akili) na aone ikiwa kuna njia yoyote ovu ndani yake. Hii inamaanisha kuwa hakuujua moyo wake. Soma maandiko mwenyewe na utapata kwamba moyo huwa mahali ambapo nia yetu na tamaa yetu hutoka.

Mimi ni kile Ninafikiri

Kila mtu anajua kwamba tunachokula hulishizwa mwilini mwetu, na kwa hivyo tunakubali msemo kuwa "sisi ni kile tunachokula". Lakini watu wachache wanagundua kuwa kuna kiroho isiyo sambamba: " sisi ni kile tunachofikiria" kiroho. Sizungumzi hapa kuhusu "kukiri halisi", ambayo inatufunza kuwa tunaweza kuwa kile tunachozungumza, kile tungetaka kukuwa. Hiyo ni kutia kasumba, mara

nyingi ni sawa na kueleza uongo, na ina mizizi yake kwenye mizungu. Kujaribu kubadilisha maumbile na hali ya nje kwa nguvu za kifikiri halisi(kutengeneza ukweli wetu) na tendo la hatari sana. Hata hivyo, hii haifai kutuogopesha kutoka kwa uelewaji wa kweli wa kile kinachomaanisha kufanya upya akili zetu. Mithali 23:7 inasema kwamba Afikiriavyo mtu moyoni mwake, ndivyo alivyo. Inasema kuwa kile mtu anafikiria moyoni mwake –nia yake ya akili iliyofichika na tamaa—ndiyo mtu wa kweli, na siyo anachofikiri kwa kichwa chake (fahamu yake). Mara nyingi tunafikiria, kwa vichwa vyetu, kwamba sisi ni kile tungetaka kukuwa; lakini Mungu huwa anaona mioyo yetu. Siwezi kuwa mtu zaidi au ndogo na jinsi nilivyo moyoni mwangu.

Utakatifu wa nje

Mistari miwili ya kwanza ya Warumi sura ya 12 itatusaidia zaidi kuona umuhimu wa kazi ya nafsi inayofanya katika njia ya utakatifu. Mstari wa 1 unasema kwamba tuitoe miili yetu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yetu yenye maana. Mstari unataja "takatifu", lakini Paulo anaashiria tu hapa kile tunachoita utakatifu wa nje, kwa sababu anasema " itoeni miili yenyu". Utakatifu wa nje ndicho wafarisayo walichokuwa nacho—maono ya nje ya sheria, ya utakatifu, ya utengano kwa dunia.

Ni ya maana kwetu kutambua kwamba hakuna kitu

kibaya na hii ikaambatana na utakatifu wa ndani. Yesu hakuwahi kuwahakiki wafarisayo kwa matendo yao ya nje. Aliwahakiki kwa unafiki wa kuwa watakatifu kwa nje, na wachafu, wenye tamaa, na utakatifu wa wenyewe kindani. Tunafaa kuwa watakatifu kindani na kinje ikiwa tutakuwa wakristo wa kweli.

Nyumba

Paulo hasemi kuwa akili yetu na roho inafaa iwe dhabihu, lakini miili yetu ndiyo nyumba pekee ambayo uenyewe wetu wa kweli ka roho au naishi. Anazungumza kuhusu jinsi tunavyo jiweka duniani—utakatifu wetu wa nje. Paulo anasema jambo geni hapa: ni ibada yako yenye maana. "yenye maana" inaonekana kuwa neno nyonge, na lenye kutia matatani—hakuna chochote maalum. Kwa kweli Paulo angesema "ni jukumu letu halisi", au msemo mwingine wenye nguvu?

Yenye maana tu

Nina masababu mawili kwa nini utakatifu wa nje ni "yenye maana" tu, kutarajia tu. La kwanza ni kwamba wanafiki wanaweza fanya hii. Siyo ngumu sana na hiari ya nguvu kushinda tabia yetu ya nje—kwa mfano, kutoiba na kukufuru kushikilia hasira yetu na kuwa wazinzi kwenye mienendo yetu ya nje, kufunga kuomba na kuwapa masikini. Mifano hii yote ni tabia yetu tu ya kiinje, na kutarajika kwa yeyote anayedai

kuwa mkristo. Hata Wafarisayo katika siku ya Yesu walitenda mambo haya yote ; na bado Yesu aliwaita wana wa shetani.

Tukifanya haya matendo yote ya kiadilifu, hatufai kutarajia sifa yoyote au zawadi kutoka kwa Mungu. Ni ya maana tu kwa watu wanaojiita wakristo wanafaa kuishi hivi, mara tu wanapokuwa kwenye mwangaza na wanamjua Mungu kibinafsi. Ikiwa hao ni watoto wa Mungu, ni ya maana tu kwamba waangalie tabia hii kwa tabia yao ya nje.

Sababu la pili kwamba utakatifu wa nje ni ya maana tu ni kwamba hata wasio wakristo wanatarajia kiwango cha utakatifu cha nje kutoka kwa wakristo. Mtu anaposema kuwa amekuwa mkristo, watu wanaanza kuangalia tabia yao ya nje mara hiyo kuangalia ikiwa matendo yao inaambatana na maneno yao. wakimwona mkristo akipeleka penseli nyumbani kutoka kazini, watasema mara hiyo, "Huoni uizi— nilifikiri kuwa wakristo hawaibi". Haijalishi ikiwa kila mtu kwenye kampuni alipeleka penseli nyumbani—wanatarajia kiwango kikuu cha maadili kutoka kwa mkristo.

Shahidi mbaya

Mara nyingi wakristo watathibitisha matendo yao wanaposhtakiwa na kusema, "Sisi si kamili, unajua—wokovu ni kwa neema". Lakini hii ni shahidi mbaya iliyoko ambayo wangepeana! Badala yake wanafaa kumshukuru mtu huyo kwa kufunua

makosa yao kwao, na wasikubali litendeke tena. Wasio wakristo wanaangalia kuona ikiwa matendo yetu Yanaambatana na Biblia, kwa kuwa hata wakanaMungu wanajua kwamba wakristo wanafaa "kuwapenda adui zao" na "kupindua shavu lingine".

Huwa tunafanya kiroho mafunzo ya Yesu katika mafunzo mlimani, au tunatumia vibaya matumizi yake, kwa sababu tunaogopa kwamba hatuwezi kuifuata. Hata hivyo, wasio wakristo hawatosheki na hii; wanatarajia kwa ukamilifu kwamba Yesu alisema aliyomaanisha kabisa.

Utakatifu wa nje ni jambo la kudhibiti matendo yetu kwa hiari ya nguvu. Hii ni kile kila asiye mkristo hutenda tu, kunao watu wachache wasiozuia asili yao ya zamani. Kwa mfano, mwanabiashara anaweza kutaka kuwa na uhusiano wa kimapenzi na kila katibu anayevutia kazini mwake. Anaweza kujizuia, siyo kwa sababu tamaa yake imekuwa adilifu, lakini pengine kwa sababu ameoa, au ana heshima yake kulinda, au pengine ana uoga wa kukataliwa au kuhakikiwa.

Mfano mwingine inaweza kuwa mke wa nyumbani anayetamani fanicha au nguo ambazo hangeweza mudu. Moyo wake unatamani vitu hivi, na kwa hivyo ana tamaa moyoni mwake, lakini hataiba vitu hivyo anavyotamani, au kudanganya katalogi ya ununuzi, kwa uoga wa matokeo na hukumu ya wengine. Anakaa kwa heshima, lakini hali ya moyo wake inakaa vivyo hivyo—na tamaa. Amedhibiti tamaa yake ya kutaka zaidi, asili aliyoridhi kutoka kwa Adamu, kwa hiari ya nguvu.

Wakristo hawajasamehewa

Mifano hii inaweza kuzidishwa kwa idadi kubwa kutosheleza hali yoyote. Hakuna mkristo anayewekwa kando kwa tamaa hizi. Ni za kawaida kwa maisha yetu ya kila siku kwamba yanatendeka kwa kufichika; na wakristo wataogopa ikiwa watapeana sababu ya tamaa zao badala ya matendo. Sote tunataka kujitetea kulingana na matendo yetu, siyo kulingana na tamaa yetu ya ndani na kutaka.

Watu waliona hiari nyonge watashindwa na tamaa za mioyo yao, na kwa hivyo ama wanatetea matendo yao au wajihisi kushutumiwa na wanyonge. lakini hii siyo njia ya kusonga mbele ya mkristo, lakini kujitetea kwa mwenyewe na kujishutumu yote ni mbaya. Ukweli rahisi ni kwamba hiari yetu siyo msingi wa shida yetu, na Mungu huwa anapambana na mizizi na Mwanzo.

Hakuna tendo linaloweza tendeka bila akili yetu kuhusika. Wazo huwa mzizi, kitu cha kwanza, na baada tu yetu kutumia akili yetu ndipo hiari yetu hutendeka. Na tunaamua juu ya matendo ya mienendo ya nje. tunaweza shinda au kushindwa kwa matendo yetu, kulingana na ikiwa tuna hiari ya nguvu au nyonge; lakini mzizi wa njia siyo hiari yetu, ni mawazo yetu. Nina hakika hakuna atakaye shindana na ukweli huu wa kawaida, lakini ni msingi kwa uelewaji wetu wa njia ya utakatifu, kwa sababu tusipoanza Mwanzo, tutaishia kwa unafiki. Wakati matendo yetu na mawazo hayaambatani,

tunajidanganya na watu wanaotutazama.

Badilisha Mtazamo wako

Kuna methali ambayo Ningependekeza kila mkristo achonge moyoni mwake: ikiwa hauwezi kubadilisha hali yako, badilisha Mtazamo wako. Mitazamo zinaambatana na akili yetu—jinsi tunavyofikiri—naikiwa tutapambana na hii, hali zetu basi siyo za matokeo.

Katika Warumi 12:2 Paulo anatuonyesha kwa dhahiri jinsi tunavyoweza kubadilisha kufikiri kwetu: wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu. “kufuatisha” inamaanisha kuja kwa laini na, au “kubanwa kwenye kuvu”.

Mfumo wa dunia umeshambulia kabisa akili zetu na falsafa yake na kufikiria kwa kila mada ya kubuniwa kutoka kwa mitindo au siasa, kutoka kwa udhabiti wa uzazi hadi mielekeo ya mazingira ya jinsia. Vyombo vyote vya habari vime yaweka wazi—akiba ya matangazo makubwa kwenye kando ya mitaa ambayo mtu hawezi kosa kuona, televisheni na redio, magazeti na majarida kwa kila mada, tamaa au mada ya ufundi—haya yote yanakabiliana na akili yetu na manufaa yetu kila siku. Ujumbe hizi za vyombo vya habari yanakabiliana nasi yenyewe kwa dunia hii ikiwa tunakubali wenyewe kujionyesha.

Siyo tofauti

Mtazamo wa jumla kwa wakristo wa sasa

itadhibitisha ukweli huu, kwa mitindo yao ya mavazi, mapambo yao ya nyumbani, mapumziko yao na burudani siyo tofauti na yale ya mtu mwenye maadili kwenye nchi yao. Tunaona matangazo sawa, tunaona mabango sawa, tunasoma magazeti sawa, na kwa bahati mbaya tunaathiriwa kwa njia sawa.

Kufanya upya akili

Paulo anatuonyesha kwamba njia moja tu ya kushinda hii makombora ya akili yetu ni kupambana ni pia kupambana na akili yetu. Anatueleza kuwa tunafaa kugeuzwa, kubadilishwa kwa njia ya kufanya upya. Njia hii, kama ya dunia, pia inafanya kazi kwa kurudiarudia. Dunia inatufuata, mara nyingi bila idhini yetu. Ninapata kutangaza kwa pahali pa umma ya kuudhi na kuchukiza kwa sababu sina uamuzi wa kuona mabano hayo au la. Sina njia ya kubadilisha hali hii, kwa sababu ninasafiri sana kwenye miji mikubwa. Lazima nione mamia ya mabano kila siku nikiwapeleka watoto wangu wawili shuleni. Watoto wangu pia wanatawalwa na picha zinazoonyeshwa kwenye mabano, na siwezi badilisha ukweli huu.

Ujumbe unaorudiwarudiwa ya matangazo ni njia ya kutia kasumba, kwa sababu haiko kwa idhini yangu. Lakini marudio kwa idhini siyo kutia kasumba, lakini kufanya upya—hiyo ni, ubadili wa akili ulio na fahamu na ulio dhabiti ambayo itasambaa mwishowe kwa matendo yetu. Hii ndiyo siri, kwa sababu hapo matendo yetu yanakuwa yasiyo jitanguliza, na uadilifu

wetu haukuwi tena uadili wa wenyewe ambao unakuja kutoka kwa nguvu zetu wenyewe; hatujaribu tena kufuata matendo yetu kwa kanuni za maadili mema.

Kuanza njia

Nimeridhishwa kwamba ikiwa tunaweza kubadilisha kufikiria kwetu, ambayo inamaanisha Mtazamo wetu, basi hatufai kufanya lolote zaidi. Tumeanza njia ya utakatifu, na itakuwa na matokeo yake kwa wakati upasao. Warumi 12inataja idadi ya kushangaza ya Mitazamo ambayo tunaweza kuchukua kwetu wenyewe nimetaja mitazamo thelathini kama hayo kutoka kwa sura hii kwenye pambizo ya Biblia yangu; lakini nyaraka zote zimejaa maagizo ya jinsi mitazamo yetu inapaswa kuwa kwa Wachungaji wetu, familia, au hali ya kazi. Hapa kuna mifano michache, ambayo yanatuonyesha kuwa maandiko haya yanatueleza kimsingi jinsi ya kufikiria.

Usijifikirie zaidi ya jinsi unavyo faa, lakini fikiria na busara kama
Vile Mungu amempa kila mtu kiwango cha imani.
Wacha upendo uwe wa kweli.
Uwe mkarimu na mwenye moyo wa kupenda wengine, kwa
heshima ya kustahabu kila mmoja.
Usiwe mvivu kwa kazi yako
Uwabariki wanaokulaani.
Uwe wenye akili moja mmoja kwa mwingine.

Usiwe wenye akili ya juu, lakini kuja chini kwenye kiwango cha
watu wa hadhi ya chini.
Usifikirie sana juu ya maoni yako.
Usilipize kisasi.

Mistari hii inakaa sana kama ibada ya kubarikiwa kwa Yesu. Ni rahisi kufikiria Unyenyekevu au upole kama "sifa" ya kugusika au sifa ya tabia ambayo tunahitaji kumiliki, lakini siyo. Ni Mitazamo tu—njia ya kufikiria. Unyenyekevu au upole siyo vitu ambavyo tunafanya (matendo yetu) lakini njia za kufikiria, kwa sababu unyenyekevu na upole ni uamuzi, uchaguzi, akilini mwetu.

Akili ya Kristo

Ukisoma katika nyaraka utashangaa kupata ashiria nyingi ya akili, na Paulo mara nyingi hutumia Yesu kama mfano ya jinsi kufikiri kwetu kunapaswa kuwa. Katika Wafilipi 2:1 Paulo anauliza swali ambayo kila mkristo anafaa kujibu ndiyo. Je mmepata faraja yoyote katika Kristo, matulizo yoyote ya mapenzi, ushirika wowote wa roho, huruma yoyote na rehema ? Paulo anajua kwamba tumempata kwa kweli vitu hivi vyote kwa mkombozi wetu, na kwa hivyo anaweza kutupa changamoto na kauli yake ifuatayo katika mstari wa 2: Ijalizeni furaha yangu, ili muwe na akili moja, wenye mapenzi moja, wenye roho moja, na akili moja. Katika mstari wa 3 anaendelea kueleza jinsi tunavyo paswa

kifikiri. Haifai kutendeka kwa kushindana wala kwa majivuno, bali kwa Unyenyekevu wa akili, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. Mstari wa 5 unasema, Iweni na akili hiyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; kisha tunapofikiria kuwa haipatikani, anatusaidia kwa kutueleza jinsi Kristo alivyofikiria. Inaonyesha, kwa kuwa inatuonyesha kwamba Unyenyekevu wa kweli ni Mtazamo—iko kwa vile tunavyofikiri. Mstari wa 6 inatuambia kuwa Yesu alifikiri kuwa uizi kuwa sawa na Mungu. Hii si kauli ya mtu mwenye kiburi, kwa katika maisha ya Yesu ilikuwa ukweli mtupu, ukadiriaji wa kweli. Mstari wa 7 unatuambia kwamba Alijinyenyekeza hadi kwenye kifo msalabani. Kujinyenyekeza ni hali tofauti sana na kukubali kunyenyekezwa. Mtu mwenye kiburi anaweza kunyenyekezwa, lakini hatanyenyekea kwa hiari yake, kwa sababu kujinyenyekeza kunahitaji Mtazamo wa unyenyekevu , njia ya kufikiri. Hali inaweza kumnyenyekeza mtu, lakini hali haiwezi kubadilisha njia yao ya kufikiri. Wanaweza kunyenyekezwa au kuaibishwa, lakini bado wanaweza kubaki na kiburi moyoni mwao.

Fikiria kama Kristo

Mara nyingi tunamwambia Mungu abadilishe hali yetu, lakini Mungu huwa anahitaji kubadilisha kwa Mtazamo akilini mwetu kabla afanye hivi.kwa kweli, mara nyingi tunapobadilisha Mitazamo yetu,

Tunapata kwamba tunaridhika na hali yetu ya nje. Hii inadhibitisha tu kuwa shida haikuwa kwenye hali, lakini kwenye Mtazamo wetu kwao.

Ikiwa kama wakristo tunaweza anza kufikiri kama Kristo alivyofikiri na kukomesha akili yetu kutawaliwa na fikira ya dunia, njia ya utakatifu itaanza. Wacha nisisitize tena kwamba ni njia, na ahadi ya milele; lakini hakuna aliye na sababu ya kutoanza njia hii.

SURA YA 16

Sababu Na Matokeo

Haki ya Mungu imedhihirishwa toka imani hadi imani, Mwenye haki ataishi kwa imani. Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa mwanadamu, waupingao kweli kwa uovu; kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia. Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake hata wasiwe na udhuru.

Romans 1:17-20

Paulo anatueleza katika mistari iliyo juu kwamba ghadhabu ya Mungu juu ya watu waovu itadhihirika kabisa. Hakuna atakaye kuwa na udhuru , kwa

sababu sheria ya Mungu katika uumbaji wake inadhihirisha tabia yake. Hii ni ukweli kwa kila nafsi. Sote tunadhihirisha tabia yetu kwa jinsi tunavyo pamba nyumba zetu, jinsi tunavyovaa na maisha yetu yote ya kila siku. Siziiti sheria hizi "sheria za sayansi", kwa kuwa kwa ukweli hakuna kitu kama hicho.

Sayansi inatambua tu sheria ambazo ziko katika uumbaji wa Mungu. Hakuna tofauti kati ya "sheria ya kiasili" inayodaiwa ya hesabu, kemia, na fizikia, na sheria za kiroho. hakuna "sayansi ya kiasili" ama "ulimwengu". Dunia iliumbwa kwa kupita akili. Uumbaji ni tendo la Mungu, siyo uendeleaji au mageuko. Ni fikira za mwanadamu kuona kila kitu kuwa sababu ya asili.

Sheria zote za uumbaji ni za kiroho

Kwa nini, kama wakristo, ni ya maana kuelewa kanuni hii? Nitafafanua. Tukifikiri kwamba " sheria ya sayansi" ni sheria ya asili tu na haina jambo lolote na tabia ya Mungu, basi hatutaitumia kwa maisha yetu ya kiroho, na tutakosa utambuzi mwingi, maagizo na mwelekeo yanayokumba maisha yetu ya kila siku. Itabidi turudi kwenye kanuni zilizotungwa na mwanadamu za mawazo ya kibinadamu kwa maagizo ya hali ya maisha yetu ya kila siku.

Niruhusu nichukue sheria rahisi ambayo kila mtu husoma shuleni—sheria ya "sababu na matokeo". Tunakubali kuwa hakuwezi kuwa na matokeo bila ya kuwa na sababu kwanza. Ikiwa tutagundua kwamba

hii ni sheria ya kiroho basi tunaweza kuitumia kwa ukimbizaji wa utakatifu.

Matokeo

Kama wakristo tamaa yetu ni kuwa watakatifu. Hili ndilo tokeo tunalotamani. Masababu ni tofauti na matokeo. Kanuni ni kwamba ili upate tokeo, unahitaji tu sababu; unatafuta sababu ndipo tokeo. Tokeo litakuwa tokeo la asili la sababu. Kwa hivyo, jambo la mwisho ambalo tutafanya ni kujaribu kuwa watakatifu wenyewe. yote tunayahitaji kufanya ni kutafuta sababu ya utakatifu.

Kujaribu kuwa watakatifu haiwezi kutufanya watakatifu. Itatufanya tu kuwa wanafiki. Kwa kuwa tukidhania kuwa tumefika kwenye lengo letu kwa kutimiza utakatifu wa nje, yote tutakayo timiza ni tokeo-bandia bila sababu, na hii sasa inakuwa uongo, kujifanya , kujisingizia – ambayo ni maelezo halisi ya unafiki.

Sababu

Wakristo wengi wanajaribu kuwa watakatifu, na wanagundua kwamba wanashindwa. Ni waaminifu kwa wenyewe na wanakubali kuwa matendo yao haiambatani na Mtazamo wao wa ndani; na hii inaweza tu kuleta kuvunjika moyo na kushindwa, kwa kuwa sababu ya sheria ya kudumu ya sababu na tokeo inasema kwamba lazima twende kwa sababu

tukitaka tokeo. Enyewe haiwezi kubadilisha enyewe. Kwa hivyo hatufai kujitahidi kwa utakatifu, kwa sababu itakuwa “utakatifu-wenyewe” – ambayo siyo zaidi kuliko haki ya mwenyewe. Badala yake tunafaa kutafuta sababu ya utakatifu—vitu vinavyotuweka watakatifu. Hii italeta uhuru mkubwa, kwa sababu vitu ambavyo vinatusababisha kuwa watakatifu ni vitu ambavyo tunaweza kufanya.

Wakristo waliovunjika moyo

Wakristo wengi wanaojaribu kuwa watakatifu huvunjika moyo na wanabaki wakihisi kuwa utakatifu hauwezi kupatikana, kwamba inakuwa na kutenda mambo ambayo hayawezi kutendeka. Lakini sababu la utakatifu iko na vitu vinavyopatikana kwa urahisi ambavyo tunaweza kufanya. Siyo ngumu kuvifanya ikiwa tunataka kuvifanya.

Manufaa mengine makubwa kwa kutafuta sababu na siyo tokeo ni kwamba utakatifu wetu sasa inakuwa tokeo la asili , kwa sababu uangalifu wetu imelenga sababu ya utakatifu, siyo kwa utakatifu wenyewe. Matokeo ni kwamba tunakuwa watakatifu, lakini hatujafahamu utakatifu wetu. Hakuna kitu kibaya kwa mtu kama ufahamu wa utakatifu wa uenyewe—kila wakati wanapofanya kitu kizuri au chenye haki, wanakifahamu: tendo lingine takatifu, wanajitambua kwa utakatifu wao, kwamba hao na kila mtu wanaijua. kisha inakuwa njia rahisi ya kuvuta nadhari kwao wenyewe. ni kujidai, na sio kuwa haki kwa imani

kamwe.

Tukifuatilia sababu badala ya tokeo, utakatifu wetu siyo fahamu yenyewe, n kutodhania. Hii ndio utakatifu wa kweli pekee, utakatifu ambao umefichika ndani mwetu. Watu kisha wanaona matendo yetu mema na hawatutukuzi bali Baba wetu aliye mbinguni; na hii inatulinda kutokana na kiburi na utakatifu wa uenyewe.

Utukufu wa Mungu

Wacha tuangalie Wakorintho wa pili3:18 na tuone jinsi sheria hii ya sababu na tokeo inatumika kwa huu ukimbizaji wa utakatifu. Paulo anasema, Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano huo huo, toka utukufu hata utukufu, hata kwa utukufu utokao kwa Roho ya Bwana.

Kuna maneno ya kuzingatia katika maandiko yoyote, na tunafaa kuyaelewa kabla mstari wote uelezwe. Kwanza nataka kuuchunguza neno "utukufu". kutoka utotoni nimeisikia na kuisoma Maelfu ya mara, na bado nikiulizwa niieleze ningeaibika, kwa sababu sikuielewa. Niliihusisha na Shekinah kwenye Tabenakulo au mwangaza mtakatifu kama ilivyoelezwa kwenye taswira ya kigiriki. Nimesoma tangu siku hizo kuwa vitu hivi ni maonyesho tu ya utukufu wa Mungu, na kwamba utukufu wenyewe inaweza kubadilisha na neno tabia.

Utukufu ni asili na hali ya Mungu.

Kuegemeza maelezo haya wacha tuangalie maandiko haya yanayotumia neno hili. Musa katika Kutoka 33:18 alimwambia Mungu, Nionyeshe utukufu wako. Mungu alimficha Musa kwenye ufa wa mwamba na kisha akatangaza tabia yake. Sura ya 34:6-7 katika Agano jipya, katika Yohana 17, Yesu aliomba kwa Baba yake na akasema, Nimekutukuza duniani; nimeimaliza kazi ulionipa nifanye. Je Yesu alimtukuzaje Mungu duniani? Kwa kweli ilikuwa kwa kudhihirisha tabia ya Mungu kwa mwanadamu.

Tukibadilisha neno "tabia" kwenye andiko tutaelewa kitu ambacho Paulo anaona. Lakini sisi sote kwa uso usiotiwa utaji, tukirudisha tabia ya Bwana, tumebadilishwa kuwa sura sawa kutoka kwa tabia hadi tabia.

Je inaweza kuwa rahisi? Je ni ukweli kwamba kwa kuangalia tabia ya Mungu, tunaweza kubadilishwa hadi kwa tabia hiyo? Inakaa ya rahisi sana. Tumezoea kupambana na hiari yetu ya kuwa watakatifu.na haikai ya kweli kwamba inaweza kutendeka bila nguvu zetu nyingi. lakini tusisahau kwamba Paulo haoni tu tokeo bali sababu. Anatuonyesha mizizi ya utakatifu.

Kidogo kwa kidogo

Jambo la pili ninalotaka kuangalia kwenye maandiko haya ni njia ambayo Paulo anatuonyesha, kwa kuwa anasema kutoka utukufu hadi utukufu – kutoka tabia hadi tabia. Hii inamaanisha kwamba

utakatifu hajui tu kutoka kwa tendo moja ambalo linazaa majibu ya mara moja, lakini ni njia ambayo inatendeka kwa viwango; kidogo kwa kidogo tunakua kwa neema. Tendo linaweza kuwa na matokeo ya mara moja, lakini njia huchukuwa wakati; na utakatifu ni njia.kwa hivyo hatufai kutarajia matokeo ya haraka au mara moja. Tunafaa kugundua kwamba kukua kwetu kwa utakatifu kutakuwa polepole, na mara nyingi siyo ya kugundua kwa sababu ya kima polepole cha ongezeko. Lazima tuangalie nyuma kwa muda wa wakati ili tuone mafanikio; lakini matokeo yatakuwa, na tunaweza kuwa na ujasiri kwamba ikiwa tuna sababu, basi matokeo yatakuja yenyewe. utakatifu utakuwa kwa kweli sehemu yetu asili.

Kioo

La tatu na neno la mwisho ambayo nataka kuangazia ni "kioo", ambalo linamaanisha "kioo". Paulo anasema kwamba tukiona tabia ya Mungu na uso usio na utaji (hiyo ni, uaminifu, au na matarajio) kama kwenye kioo, tunabadilishwa kuwa sura kama hiyo.

Ni kwa nini Paulo alitumia msemo huu? Ni nini hufanyika tunapoangalia kwa kioo? Tunaona sura, maono, picha ya kile tunachokiangalia. Lazima tukumbuke hapa kwamba tunafaa kuangalia tabia ya Kristo kana kwamba ilikuwa sura, kitu ambacho tunaweza kuona, kitu ambacho kinakuwa wazi kwenye maono yetu. Tunapoona kitu chenye picha,

basi hatuna shauku tena na mfano wake.

Kitu chochote kinachotoka kwetu ni picha ya chochote ambacho kiko ndani yetu. Hakuna kitu ambacho kinaweza kutoka miilini mwetu na akilini mwetu ambacho hakikuingia kwanza. Sote ni matokeo ya mazingira yetu, hiyo ni kusema kwa athari yetu ya nje ambayo imetuingia maishani mwetu. Upembuzi wetu maneno na tabia yetu ya tamaduni yote yanadhihirisha athari yetu ya nje. Kwa hivyo ili kubadilisha tabia yetu ya nje lazima kwanza tujiweke wazi kwa athari zingine tofauti. Hizi lazima ziwe athari za nje pia, kwa kuwa hatuwezi kujibadilisha wenyewe kwa wenyewe; enyewe haiwezi badilisha enyewe.

Kuona na kuelewa

Tunafaa sasa kuanza kuelewa jinsi sheria ya sababu na tokeo inavyoweza kutumika ukimbizaji wetu wa utakatifu. Ikiwa tunaweza tu kuangalia kwenye tabia ya Mungu na kuona kwa uwazi ni gani, basi picha hiyo inayokuja kwenye ufahamu wetu itaonyeshwa maishani mwetu. Haiwezekani kwa hiyo kutotendeka.

Ugumu wetu kwa utakatifu haiko kwa hivyo kwa kujitahidi kuwa watakatifu kwa tabia ya nje, lakini kwa kuona na kuelewa tabia ya kweli ya Mungu ni gani. Hii ndiyo pointi ya kukwamia, pointi ambayo wakristo wengi wanashindwa kuelewa katika ukimbizaji wa utakatifu.

Tunaweza pia kubadilisha mlinganyo na kusema

kuwa watu ambao sio watakatifu kwa nje ni watu ambao hawaoni kwa uwazi na kuelewa tabia ya kweli ya Mungu, au utakatifu.

Yesu mfano wetu

Yesu katika mfano wetu wa utakatifu. katika injili ya Yohana sura ya 12:44-45,Yesu aliweka kauli ambacho kinatuonyesha kwamba yeye, pia, alionyesha tabia ya Baba yake na siyo yake. Alisema, Yeye aniaminiye mimi, haniamini mimi bali yeye aliyenituma. Naye anitazamaye mimi amtazama yeye aliyenituma. Kwa uwazi, Yesu alikuwa anasema kuwa alikuwa tu picha ya Baba yake aliye mbinguni. Huu ni ufunuo wa kusisimua, kwa sababu inamaanisha kuwa tukimakinika kwa athari zetu badala ya kwa hali zetu, basi tutaonyesha athari hizo sawa maishani mwetu. Itakuwa kawaida na rahisi.

Tukilinganisha kwa uaminifu muda wa wakati ambao wakristo wengi wanatumia wakiathiriwa na mfumo wa dunia na muda wa wakati wanaotumia wakiathiriwa na ufalme wa Mungu, matokeo yanaaibisha. Chukua, kwa mfano, wakati unaotumiwa kwa kusoma ufundi, mitindo, habari, na masomo ya viburudisho, ikilinganishwa na wakati unaotumiwa kusoma neno la Mungu. Watu wengi watakubali kwamba wakati unaotumiwa kusoma neno la Mungu ni sehemu ndogo tu ya wakati unaotumiwa kusoma vitabu vingine. Kanuni yetu ya sababu na tokeo inatuambia kuwa tunaweza na tutaonyesha tu mizani

hii ya athari katika maisha yetu ya kila siku na tabia yetu ya nje.

Athari

Vyombo vya habari sasa vinachukua nafasi ya uzima na ya kunengua katika mifumo ya dunia yetu, siyo tu kwa viburudisho lakini siasa, biashara, na dini. utaratibu wa propaganda ni wa kuogofya kwa uwezo wake na athari zake. Sayari nzima inatawalwa polepole ili kukubali hali ya maisha na nanma ya kufikiri kwa njia ambayo ingekuwa ngumu miaka sabini zilizopita.

Kwa jambo la ubasha, kwa mfano: miaka sabini zilizopita ubasha ulikuwa umedharauliwa na jamii yote kama upotovu ovu. Lakini sasa ukimuuliza mtu aliye na miaka sitini au sabini wanachofikiri kuhusu ubasha, watasema kwa uwazi kuwa lazima tuwe wavumilivu, wenye akili wazi na kwamba watu wengine wamezaliwa na unyonge wa ubasha na ni sehemu ya utaratibu wa jenetiki. Pointi yangu siyo kwamba ikiwa uvumilivu ni njema au mbaya, lakini kwamba polepole mabadiliko yamechukua nafasi, na yametendeka kwenye mizani ya dunia nzima isiyowahi kutokea kwa sababu ya athari ya vyombo vya habari.

Kumbukumbu yetu pekee

Ikiwa tunataka kujua tabia ya Mungu, Biblia ndiyo sehemu yetu ya pekee ya Kumbukumbu, na

tunaidharau kwa hatari yetu. Vitabu vya kanuni na teolojia haziwachwi kando kwa neno la Mungu. Mahubiri ambayo ni ya maana kwetu, bado pia haiwekwi kando kwa kutumia wakati peke yetu na Mungu. Uhusiano wa kibinafsi lazima ikuzwe kwa msingi wa moja-kwa-moja, na hii haiwezi kufanyika kwa mikutano ya dharura au watu wengine wakiwa.

Ikiwa tutaangalia tu tabia kamili ya Mungu, na utakatifu wake, basi maisha ya nje itaathiriwa kwa wakati wake, na itakuwa utakatifu bila unafiki, kwa sababu itakuwa picha, siyo ya uwezo wetu, lakini ya maisha ya Kristo.

Ikiwa kulikuwa na sehemu moja ya Biblia ambayo inafanya muhtasari wa tabia ya Mungu kwa mfuasi wa kisasa ni mahubiri mlimani katika Mathayo 5,6,na7. Ninaamini kwamba barua zote kwa makanisa kutoka kwa Paulo, Petro, Yakobo, Yohana na Yuda yanafafanua tu na kueleza zaidi mahubiri mlimani. Pia nimeridhishwa kwamba sheria zote na manabii wamejumuishwa na kutimizwa kwa mafunzo haya mengi ya Yesu kwa wanafunzi wake.

Kitabu kitakachofuata cha kiini cha Ukristo kitaanza somo la mafunzo ya ajabu kutoka kwa Bwana mwalimu mwenyewe. Imepindua maisha yangu mwenyewe kwa kupitia kanuni hii tumeangalia sababu na tokeo. Nilipogundua kanuni hii, kujitegemea kwa athari ya tabia ya Mungu zaidi ya vile ningeweza kwa kusoma Biblia, kuomba, kufunga, kutumia wakati peke yangu na Mungu, nilipata kwamba nilianza kubadilika kiinje licha ya mimi mwenyewe.

Mabadiliko niliyoona kwangu mwenyewe mara nyingi yalinishangaza, kwa sababu sikuwa ninajaribu kuwa mtakatifu tena, niliwacha kujaribu kuwa mtakatifu, na bado nilikuwa ninatimiza sababu ambayo nilitamani kwa muda mrefu—kuwa mtakatifu.

Ninazungumza kuhusu muda wa zaidi ya miaka ishirini, na kwa hivyo ninazungumza kutokana na uzoefu ninaposema kuwa hii ni njia ambayo haiwezi kupatikana mara moja, au hata kwa muda mchache. Subira na uvumilivu ni aina za njia.

Nimeridhika kuwa kushindwa kwa wakristo wengi ni kwamba hawafiki mwanzoni mwa njia hii. Wacha nimpe changamoto kila mtu anayesoma kitabu hiki wajishinikize na mahubiri mlimani hadi ianze kufanya kazi kwa mazoezi maishani mwao.

Badilisha macho yako kwa Yesu
Angalia kikamilifu kwenye uso wake wa ajabu
Na vitu vya dunia vitakua gizagiza ya kigeni
Kwenye mwanga wa utukufu wake na neema.

Maurice Barratt

Maurice Barratt

Maurice Barratt alilelewa chini ya huduma elimumwendo ya kipentekoste ya baba yake Bill Barratt, sehemu ya huduma ya Barratt na Williams katika miaka 1950 na 1960.

Alikuwa mkristo katika mwaka wa 6,na kwa ujana wake aliishi maisha yenye desturi na kipaji cha Ukristo. Lakini alipofika miaka thelathini aliathiriwa sana na mafunzo ya babake ya mahubiri mlimani kwenye kanuni ya ufuasi wa kweli wa Kikristo—kinachomaanisha kwa kweli kumfuata Yesu. Kutoka wakati huo alianza kubadilika kutoka kwa mkristo wa "kawaida" wa desturi hadi kwa mtu aliyeridhika kuwa kinachokosekana kwa wakristo wa leo siyo nguvu za kimiujiza au vipaji lakini tunda, tabia ya Yesu.

Kwa miaka ishirini iliyopitia Maurice amejitia kwenye mwito wake—kufunza kanisa kanuni ya matendo ya ufuasi. Amefunza kwa makanisa, makundi ya nyumba, majela, mashule na mashule ya Biblia, kote Ulaya na Marekani.

Mengi ya ujumbe ya Maurice Imerekodiwa kwenye kaseti, ikiwemo mfuatano mkuu, kwenye mahubiri mlimani inayofunika makaseti hamsini na tano, ujumbe wa mada mengine yanayohusu maisha ya mkristo na mwenendo wake.

Maurice Barratt anapatikana kwenye huduma na anaweza kuwasilishwa kwenye anwani mkabala.

Kuhusu huduma ya Barratt

Huduma ya Barratt ni shirika la Kikristo lililo na msingi wake Manchester lililoanzishwa mwaka wa 1985. Wakurugenzi Maurice na Joanna Barratt wana huduma ya kimataifa ya kufunza na kuhubiri. Joanna ni mwimbaji na ana albamu tisa za muziki za nyimbo zake, zikiwemo miradi miwili mikubwa ya maandiko kwenye wimbo – Zaburi 119 na Mahubiri mlimani. Joanna pia anahubiri kwenye magereza na ushirika wa akina mama.

Huduma ya Barratt ni huduma yenye vyombo vingi vya habari, inayohusika na uchapishaji wa vitabu na fasihi, kurekodi kwa albamu za muziki ma makaseti ya mafunzo, utoaji wa video na vipindi vya redio ya Kikristo,

Huduma ya Barratt huchapisha changamoto, kijarida la makala ya mafunzo ya Maurice na Joanna Barratt, kila baada ya miezi miwili. Inapatikana bure na kuletwa bila malipo unapoitisha.

Barratt Minbistries
114Daisybank Road
Manchester M14 5QH
England, UK